CKRC

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

CHANGAMWE CONSTITUENCY HELD AT QUEBEC PRIMARY SCHOOL

ON

## TUESDAY 2ND MAY 2002

# CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, CHANGAMWE CONSTITUENCY, ON TUESDAY, 30TH APRIL 2002 HELD AT QUEBEC PRIMARY SCHOOL

**Present**

1. Com. Pastor Zablon Ayonga
2. Com. Salome Muigai
3. Com. Paul M. Wambua

**Absent with Apologies**

1. Com. Prof. H W O Okoth - Ogendo

**Secretariat in Attendance:**

1. Eunice Gichangi - Programme Officer
2. Phillip Mollo - Asst. P/Officer
3. Regina Obara - Verbatim Recorder
4. Nancy Mwangi - Sign Language Interpreter

**The meeting started at 8.35 o'clock with Com. Zablon Ayonga in the Chair.**

**Silvia:** Nachukua fursa hii kuwashukuru nyote, kwa kuja hapa asubuhi ya leo; ijapokua kuna manyunyu. Mbele yenu leo tuko na Com. Salome Muigai na Com. Pastor Zablon Ayonga. Kwa hivyo kabla hatujaanza mjadala wetu wa leo, nitamuuliza moja wetu atuongoze kwa maombi.

**Prayer**: Kwa jina la Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, mwenye kurehemu, mema na mazuri hapa duniani. Twakuomba ewe Bwana Mungu, utuongoze katika kikao hichi, tuweze kufikia maazimio tulio kusudia. Na pia uturudishe salama, kule tunako toka. Ewe Bwana Mungu twakuomba utuongoze salama. Amina.

**Silvia:** Asante sana, nataka ni wakaribishe Commissioners wetu ili tuendelee na mkutano wetu.

**Com. Salome**: Asante sana Silvia, asante sana kwa kufika mimi jina langu ni Salome Wairimu Muigai, na kama mlivyoambiwa mwenzangu hapa ni Com. Pastor Ayonga; na tuna furaha kubwa kufika hapa Changamwe. Ningetaka kukitangaza hiki kua Kikao cha Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Kenya. Sisi huanza kikao chetu saa mbili asubuhi, na kumalizia thenashara. Leo tumechelewa kidogo, kwani watu tayari wanajiandikisha, lakini shughuli zetu huanza saa mbili na kumalizia thenashara. Wakati

mwingine ikifikia saa sita unusu, sisi tutakivunja hiki kikao, na kukiairisha ili watu waende maombi; halafu ikifikia saa nane tutakianza tena. Sisi kwa kikao chetu kwa kawaida, tunatumia lugha mbili, tunatumia lugha ya Kiswaili, na pia tunatumia lugha ya Kingereza. Kama vile mnavyotuona hivi, tunatoka Bara, Kiswaili hatukielewe vizuri kwa hivyo mtatusamehe tukivunja vunja; lakini pia waingereza wanaposikia tukizugumza lugha yao; pia wao wanakua na samahani kubwa na ya kutuachia tuzugumze, mradi tuelewane. Kwa hivyo leo hatukizungumzi Kiswaili vizuri ipasavyo, lakini twakizungumzia kwa minajili ya kuelewana. Kwa hivyo ikiwa mnatuelewa, mtusamehe kwa kukosa kuzungumza vizuri. Tutajitahidi vilivyo lakini, ili tuweze kuwasiliana. Lakini ukiweza kutumia lugha yeyote ya Kenya ni sawa mradi tu utueleze kabla ili tuweze kutafuta mtu anayeweza kututafsiria ile lugha.

Leo unaweza kuja hapa ujieleze wewe binafsi, na maoni yako. Pia unaweza kuja hapa kukisimamia kikundi chako kilicho sajiliwa. Isitoshe, ikiwa wataka kusimamia kikundi chochote kile kingine; hata kama hakijasajiliwa, pia tutakupa nafasi ya kuyatoa maoni yako, ndio isaidie Katiba yetu ya Kenya. Ukija hapa tutakupa muda fulani wa kujieleza kwani tunataka kumsikiza kila mtu. Ukiwa wewe una maandiko, yaani una memorandum utatuachia. Tutakupa dakika tano ili kumulikia yale makubwa kwenye maandiko yako. Sio kusoma neno kwa neno, kwani hiyo itachukua muda mrefu, na tungetaka kukuhakikishia kua tukiyapeleka haya kwenye Tume; yatasomwa neno kwa neno. Lakini wakati huu tukikupa dakika zako tano, naomba uelezea tu yale makubwa makubwa, yale mengine yatasomwa na Tume.

Ikiwa huna maandiko yeyote nitakupa dakika kumi, ili uweze kujieleza. Ukisha maliza kupeana maoni yako, nitawaomba wana Tume kukuuliza maswali na wewe uyajibu. Hayo maswali ni ya ufafanuzi tu ili tukuelewe vyema. Hatutakuuliza maswali ya kuingia kwenye mjadala, ya kukubaliana au kutokubaliana nawe. Pia nitawapa nyinyi mlioketi huko nafasi ya kuuliza swali, lakini pia hilo swali litakua la ufafanuzi tu, ukiingia kwa swala la mjadala, kumpinga mwenzako au kukubaliana naye; mimi kama mwenyekiti, sita kuruhusu uendelea na hayo maswali. Huu sio wakati wa mjadala, huu ni wakati wa kusikiza kila mtu na maoni yake. Ikiwa wewe hukubaliani naye basi utampa nafasi yeye atoe maoni yake, utampa heshima zake; nawe wakati wako wa kuzungumza ukiwadia utapeana maoni yako naye pia atakupa nafasi yako, na heshima zako. Ukishamaliza kuzungumza utajisafirisha kwenye hiyo meza ukiwa na maandiko utampa yule, baada ya kujiandikisha. Ukiwa pia na ukanda wa tape, kama umenasa habari zako kwenye diskette au kwenye tapes, pia hiyo tutakubali. Kwa hivyo yale yote umeleta kwenye Tume tafadhali usirudi nayo. Hata ukiwa haujapata nafasi ya kuzungumza, unaweza pia kupeana memorandum yako, itaenda kwa Tume naitasomwa. kusomwa. Na kwa hayo basi ningetaka kumpa nafasi mzungumzaji wetu wa kwanza Mohamed Faki. Pahali pa kuzugumzia ni pale, hiyo desk pengine itakukumbusha siku zaki darasani. Unayo memorandum?

**Mohamed Faki**: Ndio, niko na memorandum. Na utaniwia radhi, kwa sababu kuna mambo mawili matatu ambayo ningependa kuyazungumzia. Kwa jina kwanza naitwa Mohamed Faki, mimi ni wakili kikazi; na ni mwenyekiti wa Changamwe Muslim Association. Na furahi kwanza kupewa fursa hii kuweza kutoa maoni yangu na maoni ya ndugu zangu, kwa Tume hii ya kurekebisha Katiba.

Kabla ya uhuru eneo la Pwani yaani Ten Mile Coastal Strip, iliokuwako si koloni ya Uiengereza. Ilikuwako ni protectorate ya Muiengereza ambayo alikua anasimamia kwa niaba ya Sultan wa Zanzibar. Kosa la kwanza lililotendeka ni kwamba sisi, babu zetu, na ndugu zetu, waliokuako wakati ule hawakushauriwa, kama tuweze kubakia katika Sultani ya Zanzibar; ama tuweko katika Kenya mpya. Lakini serikali ya Uingereza ilifanya bidii, na ikaleta Tume ile ya James Wolfensen Commission; ambayo katika report yake ya 1961, ilieleza mambo matano ambayo, sisi kama wakazi wa sehemu hii, tulizungumzia juu ya Kenya mpya.

Mambo haya yalihusiana kwanza na uhuru wa kuabudu. Wakazi wa eneo ili wengi wao walikua ni Waislamu kwa hivyo uhuru wao wakuabudu ulikua ulindwe. Pili, ilikuako inahusiana na mali za Waislamu na taasisi zao. Tatu ilikua inahusiana na administration, yaani utawala. Wakati wa Uhuru sisi tulikua na mfumo wetu wa utawala. Tulikuako na madiwali, tuko na mudiri na wote hawa walikua ndio watala wetu, katika kila sehemu, katika ukanda wa Pwani. Jambo la nne lilikuako ni elimu yetu.

La tano lilikuako ni mahakama za Kadhi. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba baada ya uhuru, mambo haya yote yalipuuzwa, na kwa kupuuzwa ni kua, mpaka sasa katika district ya Mombasa; hatujakua na DC Muislamu, isipokua Ali Korane. Na Ali Korane aliletwa, sio kwa sababu, sisi tulipenda, aliletwa kwa sababu kulikuwako na mkubwa fulani katika serikali, ambaye alipendekeza yeye aletwe. Jambo la pili ni kwamba, PC mpaka sasa tumekua an mmoja peke yake Muislamu, Yusuf Haji, ambaye vile vile aliletwa, sio kwa mapenzi yetu sisi, lakini kwa mapenzi ya kiongozi Fulani, sehemu fulani. Jambo lingine pia la kusikitisha ni kwamba, kufikia sasa katika Pwani, tuna mtu mmoja peke yake, ambaye ameteuliwa kama Judge wa mahakama kuu: Justice Mbogoli Msagha peke yake. Miaka thelathini na nane, thelathini na tisa ya uhuru, sisi watu wa Pwani, ambao tulikua tunautawala wetu ta kila mambo yetu, tumekua tumeweza kutoa Judge mmoja peke yake, kwa mahakama kuu, hilo ni jambo la kusikitisha sana. Jambo la tatu ni kwamba sisi hatujapewa nafasi ya kuhubiri au kuendeleza dini yetu, kulingana na dini yetu inavyosema.

Tumepata nafasi wakati mwingine, ya kuleta wahubiri kutoka sehemu zengine, lakini wahubiri wale wamefukuzwa na serikali. Ardhi za Waislamu ambazo zilikuwako zilindwe na Katiba mpya, kwa mfano Mazrui Trust Land, serikali imerudi nyuma na kupuuza sheria, na kutaka kuzigawanya ardhi zile; kwa watu tofauti tofauti. Hayo ni mambo ambayo yote tulikubaliana wakati wa Katiba 1961. Report ya Wolfensein, nafikiri mumepewa nakala, yote hayo yalikubalika. Vyombo vyetu, kama vile Mombasa Polytechinic, ambavyo ni vyombo vya Kislamu, kuendeleza elimu ya Waislamu, pia zimechukuliwa na serikali. Hivi sasa Aga Khan Foundation, yachukua skuli zake kutoka kwa serikali. Na sisi kama wakazi wa Pwani, tunaomba kwamba, vyombo vile vya elimu kama vile Mombasa Polytechnic, Hamisi Secondary, na vinginevyo, vyote tuiregeshewe wenyewe. Kwa sababu zile ni mali yetu, zilikuako zimejengwa hususan kutusaidia sisi Waislamu.

Sasa katika maswala ya ardhi pia, tumeona kwamba ardhi zetu nyingi zimenyakuliwa na serikali, na kupewa watu kutoka sehemu za bara. Hatusemi kwamba ni vibaya, lakini nafasi zile kwanza ilikua tupewe sisi. Schemes kama hizi za Mikindani, ambako babu zetu na ndugu zetu walikua wakiishi, hivi sasa wote wameondoka, wanaishi maporomokoni huko chini. Scheme kama hizo zilikua zinapaswa kutufaidi sisi mwanzo. Court za Kadhi ambazo zilitambuliwa wakati ule, hivi sasa hazitabuliwi; ziko

tu kwa kua ziko, lakini hazina nguvu yeyote. Kwa mfano sisi kama Waislamu twajua mambo yetu yanapoamuliwa na Kadhi, yanatakikana kua ni mwisho. Lakini utapata kwamba kuna maswala mengine ambayo Kadhi hana uwezo wa kuyasikiza, kwa mfano mambo ya guardianship of infants, kuhusu kulea watoto kukuza watoto; inasemekana kwamba sheria ya Kiingereza, English Law, applies in preference to Muslim Law. Hilo ni jambo ambalo sisi kama Waislamu hatulikubali, na lazima liangaliwe.

Tunaona pia kwamba, katika maswala ya sheria vile vile pia, kumeletwa, married women's property act, ile inahusiana na ugawanyaji wa mali, kati ya bibi na Bwana wakati wanapoachana. Sisi Waislamu tuna sheria yetu na kuachana kuna haki ambazo bibi anapewa na sheria; kwa hivyo haki zile ziheshimiwe vile vile, kama Koran inavyosema na sura za Mtume zinavyosema. Lakini, married women's property act sisi haituhusu; ilianzishwa katika Uingereza miaka mingi uliopita, haituhusu. Tunataka tuendeshe mambo yetu kulingana na sheria yetu za Mwenyezi Mungu inavyosema.

Kwa hivyo katika kuyaeleza, na kuyatatua matatizo haya, tumependekeza kwanza kabisa. Mahakama za kadhi ziongezewe nguvu. Hatutaki Rufani za kutoka kwa mahakama ya Kadhi ziende kusikizwa na Judge ambaye si Muislamu. La pili, ushauri wa Kadhi hauheshimiwi. Tungependa kuwe na moja kwa moja, mahakama ya Kadhi ambayo itashughulikia rufani za Kadhi; zisimamiwe na Waislamu wenyewe. Hali iliyoko sasa ni kwamba ma-judge wa high court ambao wanasikiza rufani za kutoka mahakama ndogo za Kadhi, ni wachache sana Waislamu ambapo haiwezekani kupewa nafasi za kusikiza rufani zile. Kwa hivyo iwe mahakama kando ya high Court, ya Waislamu kusikiza arufani kutoka kwa Kadhi, na koti zingine za Waislamu.

Jambo la pili ni kuhusu swala la ardhi: Twapendekeza kubuniwe Tume ya Kikatiba, kushughulia maswala ya ardhi katika Pwani. Kuwe na permanent Constitutional Commission, kushughulikia maswala ya ardhi katika Pwani; na hii itashughulikia mambo yafuatayo. Kwanza kabisa, kusimamia ardhi ambazo ni za public. Pili, kuangalia maswala ya kutumia ardhi ambayo haifanyiwi ulikulima. Tatu, kutatua matatizo tofauti baina ya landlords na tenants. Hii nitasisitiza kwa sababu, kwa mfano eneo la Mvita, kuna wakati fulani serikali ilitoa agizo kwamba, ardhi zile zigawanywe, na wauzie wale watu wenye majumba. Hapa Mombasa tuna system ambapo, mtu anaweza kumiliki nyumba, lakini hamiliki ardhi. Yaani you own the house, you have a house without the land. Na ile imekua ni mfumo, kwa sababu wetu wengi wameweza kujenga nyumba, na wanaishi katika sehemu kama hizi. Lakini sasa kumetokea matatizo. Unasikia wanasiasa wanasema, sijui landlord ambao wana-charge kodi perpetually. Lakini tukiangalia, ni kama lease, ambazo serikali wanapeana kwa wananchi. Unapewa standing premium, kikwetu inaitwa mkate, baadaye unalipa kodi kila mwezi. Kama ni mia moja mia mbili. Kwa hivyo ili ni tatizo, limekua tatizo, kwa sababu wako baadhi ya watu ambao wanasema kwamba ardhi zile sasa zigawanywe watu wapewe, wale wenye majumba. Kwa hivyo hilo ni jambo moja ambalo litaweza kuangalia.

Jambo la nne, ambalo litashughuliwa katika Tume hii ni ku-transfer ardhi kutoka kwa watu wa Pwani, kwenda kwa watu wa kutoka nje. Foreigners au labda watu wakutoka Bara, hilo ni tatizo kwa sababu kuna sehemu zingine ambazo sasa hivi zimefanywa na vile vile hazikuweza kuwaridhisha watu.

Swali lingine ambalo ningependa kupendekeza pia ni kwamba, Wakfu Commission, kuna ardhi ambazo ni Trust land, Kiswaili inaitwa Wakfu ni trust land ambazo sisi Waislamu wanatoa kwa maswala Fulani, either kusaidia elimu, kusaidia jamaa zako, ama kusaidia maswala fulani. Kwa sasa kuna Wakfu Commissioners Act, lakini Wakfu Commissioners act: mwenye kuchagua Ma-commissioner ni PC, na PC si Muslim, tumekua na PC Muislamu mmoja peke yake katika Pwani. Kwa hivyo hii Wakfu Commissioner, lazima iwe overhauled; kwa sababu ardhi nyingi za Wakfu zimeweza kupotea, zingine, zimekodishwa watu wanaofanya biashara ya tembo, kinyume na matakwa ya wale ambao walitoa ardhi zile, kusaidia Waislamu na kusaidia miradi ya elimu, na mambo kama hayo.

Kwa hivyo kuna mambo fulani ambayo sisi kama watu wa Pwani na Waislamu yako very perculiar kwetu sisi, kwa mfano lugha ya Kiswaili, ni lugha yetu. Lakini ukienda kwa mfano katika mahakama ya Mombasa hivi sasa, hakuna judge Muislamu au hakuna hakimu Muislamu hata mmoja. Hii nalitia tatizo kwa sababu, sisi imani yetu kwa watu kama wale, ni chache sana; kwa sababu twawaona ni kama ambayo wamekuja hapa kututawala. Kwa hivyo jambo muhimu ambalo twataka kusisitiza ni kwamba, utawala uregeshewe sisi wenyewe. Wakaazi wa sehemu wapewe utawala, either wa kuchaguliwa, political leadership, ama administrative leadership.

Kwa ufupi ma-commissioner ni kwamba twapendekeza kwamba mfumo ujao wa kikatiba nchini uwe wa Majimbo iwe ni federal system. Sisi viongozi wetu watoke pale pale, DO, PC, na PC ambaye twapendekeza, si PC wa sasa ambaye achaguliwa kutoka Nairobi. Viongozi kama wale tuwachague sisi wenyewe. Regional Commissioners, kwa mfano Uganda wako Reginal Commissioners, ambao wanachaguliwa na wananchi.

Hatusemi pia katika kupendekeza mfumo wa Majimbo kwamba kuna watu fulani watufukuzwa la!, tumeishi kwa usalama na watu hawa, isipokua mambo machache ambayo yalitokea labda 1997, lakini twapendekeza kwamba, wale ambao wameishi hapa, wataendelea kuishi hapa hapa. Lakini uongozi wa Kiserikali, uongozi wa Kimajimbo, lazima uregeshewe wenyeji wa Pwani. Hivyo ndivyo tutaweza kuleta usawa, na justice katika jamii yetu.

Tulipata nafasi ya kuanzisha chama cha kisiasa 1991, ili kuweza kutatua matatizo yetu haya. Lakini serikali ikatufungia mlango, ikasema, hakuna kuandikisha Islamic Party of Kenya, kwa sababu ni chama cha kidini; ijapokua kilikua si chama cha kidini, ni chama kama vyama vingine. Kwa hivyo tunaomba Ma-commissioner, tupewe uhuru wetu yale maswala ambayo yalipendekezwa na Wolfensein Commission, 1961 yaregeshwe katika Katiba mpya. Ili tuone kwamba usawa, na haki, inatendeka kwa jamii zetu. Kwa hayo machache salaam aleikum. Asanteni.

**Com. Pastor Ayonga**: Bwana Faki, umesema DC ambaye ni Muislamu alikua-anaitwa nani?

**Faki:** Ndio.

**Com. Pastor Ayonga**: Je, ulitaka kumaanisha DC kutoka Pwani, au DC Muislamu yeyote nchini Kenya? Kea maana ninajua DC wengi ambao ni Waislamu.

**Com. Salome**: Inaudible.

**Faki:** Kwa hakika mimi naona kwamba ili ni tatizo la Pwani zaidi, kwa sababu tumeona kwamba, katika sehemu zingine labda utapata kwamba PC anatoka, within the Rift Valley Province. Lakini Ma-DC wanatoka sehemu zingine katika jamhuri ya Kenya. Moja ya mambo ambayo tulikua tunapigania, wakati ya IPK ilipokua inaomba kuandikisha: ni kwamba tupate watu wetu wawe viongozi. Wakati ule ilitafsiriwa kwamba, twataka Waislamu au watu wa Pwani, wawe viongozi wetu; na ndio sababu tukaletewa Ali Korane kuwa DC, immediately baada ya General Election ya 1992, Ali Korane aliletwa hapa kama DC wa Mombasa. Halafu Francis Mbaya, akaletwa pia kama mkuu wa mkoa wa Pwani. Lakini baada ya muda mchache waliondolewa wote. Ali Korane akapelekwa Kisumu, na Mbaya akapelekwa sijui Rift Valley; baadaye amefanywa Permanent Secretary. Kitu ambacho twasema ni kwamba, watawala wawe ni wenyeji wa sehemu zile. Kwa sababu hata wewe hivi sasa, kwa mfano umepewa transfer, kutoka Kisumu, au Nairobi, umekuja Mombasa. Huwezi kutafuta mtumishi kutoka Mombasa kwa sababu Kisumu au Nairobi, kwa sababu yataka upate mtumishi ambaye atajua mboga nzuri inaweza chukulia soko gani, sehemu gani kuna mahali pazuri, sehemu gani usalama wako utahakikisha, na mambo kama hayo.

Kwa hivyo utawala, yaani administration, itokamane na wenyeji wa sehemu hii. Kwa sababu ile ndio italeta uhakikisho kwamba wale wenyeji wana uhuru; na wao pia wakufanya mambo kama yalivyo. Kwa sababu hivi sasa, kwa mfano police aliyeko Changamwe, labda si Muislamu na Waislamu labda wanakwenda wakapewa Ramadhani wanaweza kukaa nje mpaka saa sita za usiku. Unapata watu wanakuja kuzolewa na msako, wanapelekwa kituoni, asubuhi wanashitakiwa na makosa ya ulevi. Kwa hivyo hayo ni baadhi ya mambo ambayo yametendeka, na yaendelea kutendeka; ambayo twahofia kwamba, siku zijazo, labdo hali itakua ngumu zaidi. Nafikiri maswali yenu yamejibika.

**Com. Salome**: Asante sana Bwana Faki, tafadhali jiandikishe pale. (the rest inaudible) Sasa ningetaka kumuita Dr. Kibwana Jhafu aje atuzugumzie kama yuko hapa nasi. Dr. KiBwana umekaribishwa. Na pia ningetaka kutangaza kua ikiwa kuna mtu ameketi karibu na mtu asiye sikia, wala hazungumzi; tuna yule mwenye kuzungumza kwa ishara. Kwa hivyo tafadhali ukijua unaketi karibu na mtu asiye azungumza ama hasikii, utujulishe kwani tuna mtu mwenye kutafsiri kwa ishara.

**Com. Pastor Ayonga**: Si yule mtu wa ishara asimame afanye yale maneno, yule mtu anaweza kujitambua peke yake.

**Com. Salome**: Ama mwenye kuzugumza na ishara wewe uamuke umweleze mwenzako kule, kua wewe uko hapa, ili wasikie. pengine waweze kuhusishwa. Kwani kuna mtu wa kutoa hizo ishara. Asante Bwana dakitari unaweza ukaanza.

**Dr. Kibwana Jhafu**: Asante Mamishena, mimi jina langu ni Dr. Kibwana Jhafu, ni dakitari katika hospitali kuu ya Makadara (Coast Province General Hospital); na ni patron wa Changamwe Muslim Association. Na furahi sana kwenu, kwa kutupatia fursa hii leo, ili nasi tutoe maoni yetu kuhusu ubadilishaji wa Katiba mpya. Wazee wangu, ndugu zangu, Salaam Aleikum. Kwa ruhusa yenu Makamishena ningependa kidogo kuzugumzia kuhusu sera na taratibu za uchaguzi. Sina memorandum lakini nitatoa maoni kuhusu mjadala huo.

Sisi baada ya kuketi na kushauriana, tumeona ni muhimu kuwe na Tume ya uchaguzi. Tume hii isiwe na Makamishena zaidi ya kumi. Nao Makamishena hawa, wawe ni watu wa heshima, watu wa busara, watu wazima, wawe na umri baina ya miaka arobaini, na sabini, si zaidi ya sabini. Nao wawe wakiteuliwa na Rais wa nchi, lakini wawe wakisajiliwa na bunge. Bunge liwe lina wadhfa wa mwisho, wa kuwakubali au kuwakataa, katika hekima yao, na busara yao Makamishena hao.

Tunapendekeza kwamba uchaguzi wa Madiwani, na wa bunge uwe utakatikiwa kulingana na wingi wa mwenye kupata kura awe ndio amepata viti hivi. Yaani tunasema Parliamentary and Civic Elections shall be decided by a simple majority. Lakini tunapenda kupendekeza kwamba, uchaguzi wa Rais, uwe utapatikana, kwa mwenye kushinda kura zaidi ya hamsini kwa mia elfu. Yaani 50% of the votes cast, iwe ndio atakua ni Rais. Na iwe Rais yule ataweza kupata kura zaidi ya provinces 2/3 ya nchi ya Kenya. Yeye ndio awe atakubalika kwamba ndiye Rais baada ya ku - garner 50% of the votes cast, na awe 2/3 of the provinces of Kenya watakua wamempigia kura zile.

Tunapendekeza kwamba wagombeniaji ubunge, au udiwani, wasikubaliwe kubadilisha vyama muda wanapokataliwa na vile vyama vyao, ambavyo wamekua wakitangaza sera vya vyama vile. Kwa sababu haileti maana yeyote, unapokua umeenda kwa nomination umekataliwa, unabadilisha, unagobania kiti kile kile, katika kura zile zile, kwa tikiti ya chama kingine. Hiyo isiwe ikakubaliwa na Katiba. Na lau chama kitakacho itikiwa ku-disolve; au ikiwa mtu au mbunge anataka ku-defect: ni lazima viongozi wale warudi tena kwa wananchi, kwenda kupata tena nguvu mpya. They have to go back and seek the mandate of the people afresh. Wasivuke tu kama tulivyoona juzi ulivyofanyika, Katiba iwe itaweza kusimama wima, na kusema, atakaye kua amefanya hivyo; ni wajibu kurudi kwa wananchi kupata mandate mpya.

Nominated seats. Viti vya kuteuliwa, either za kidiwani, ama za kibunge, viwe vitawekwa kwa special groups za kueleweka. Ambako pia viti vile vya kuteuliwa viwe vitapasishwa na bunge. Kwa sababu tunaona nguvu za ofisi ya Rais saa zingine zinachagua watu kwa mapenzi ya kuwalipa, kwa kazi nzuri labda waliomfanyia wakati wa campaign. Tunapendekeza pia kwamba kura za Rais, kura za ubunge, na kura za Madiwani, zifanywe siku bali bali. Kwa sababu ukiangalia Katiba yetu leo, yasema huwezi kua Rais kabla ya kua mbunge. Lakini ikiwa kura ya Rais na mbunge inafanywa siku moja, tunahakika gani kwamba yule atakaye kua Rais, atapata kura za kutoka katika eneo lake la wakilisho wa bunge?

Natunaomba, ifanywe ki Katiba kwamba, siku ya kura kuu, iwe imewekwa kamili katika Katiba: inajulikana Kenya nzima kwamba ikifika tarehe fulani, ya mwezi fulani, baada ya miaka fulani, itakua ndio kura na uchaguzi mkuu wa nchi itafanyika. Na

pia katika Katiba iweko kwamba siku ya ku-handover, from the previous government, to the incoming government, iwe imesajiliwa kikamilifu, katika Katiba. Tunapolala na kwaamka, tuwe tunajua, siku ya kura ni siku fulani, mwezi fulani, tarehe fulani. Na siku Fulani, tarehe fulani, mwezi Fulani, ndio siku ya serikali mpya kuchukua wadhifa wake mpya. Na tunasema kwamba kura zote za kiraisi, za ubunge, za ki-mayor, ziwe zinafanywa kupita kwa watu wote wa Kenya. Wananchi wote wawe watapiga kura. Isiwe kwamba ni baadhi ya watu fulani kama inavyofanyika hivi sasa, katika kura za Ki-mayor. Ma-councillor wanaketi na wanankata shauri, kwamba wanataka mtu Fulani, awe Mayor; halafu wakiwa hawamtaki kama tunavyoona wanamg'oa, ambayo ni kinyume ya haki za kibinadamu.

Ningependa kidogo Makamishena kutaja juu mambo ya campaign, sababu tunaamini fujo nyingi na uharibifu, na kugawanyana kwa wananchi, unatokea wakati wa campaign ya kura. Tunapendekeza, kwa sababu tunaamini wengi, au baadhi ya viongozi tulionao hivi leo, wananunua uongozo. Hawapati uongozi kwa kua wananchi wanawapenda. Tunapendekeza kwamba, wabunge au wagobania viti vya bunge, kuwe kuna kima fulani cha utumizi wa fedha zao nyingi walizo nazo. Na tunapendekeza kwanba wabunge wasikubaliwe kutumia zaidi Kenya shillings million moja, wakati wa kufanya campaign zao. Tunapendekeza kwamba madiwani, wasiruhusiwe kutumia, zaidi ya laki mia mbili na hamsini, kwa minaajili na madhumuni ya kufanya campaign. Lau ikiwa itadhihirishwa kwamba wamepitisha kiwango hicho, iwe ni hatia, na inaweza hata kuwakosesha viti ambazo wameviwai.

Jambo lingine ambalo tunapendekeza, ambalo linasikitisha ni kwamba, kuna mtindo ambao unaendelea hapa kwetu Pwani. Kuna watu tunawaita mercinary voters. Wapiga kura wanaenda kurokotwa nje, ya makao yale ambao wabunge wanagombania ubunge. Imported votes imekua ni trend, katika nchi yetu, ambayo inakosesha wale wenyeji, wakaazi wa eneo lile, kuchagua mbunge, au kiongozi ambaye wao wenyewe wanampenda. Watu wanakuja kutoka nje wanakuja wanapiga kura, halafu wakisha maliza kupiga kura, wanarudi makwao, hawajali tena mwenendo, au maendeleo yatakayofanyika kwa eneo lile ambalo haliwausu wao. Kwanza wanakosesha wale wenyeji pale kuchagua kiongozi wa kisawa sawa. Pili wanajikosesha wao wenyewe binafsi zao, haki zao, za kuchagua kule wanakoishi, kiongozi ambaye wangekua wanampenda. Kwa hivyo ikiidhihirika kwamba kiongozi, au mgombania kiti, amefanya ili, iwe ni hatia: amehusika mwenye kupiga kura awe atashitakiwa kama amefanya hatia ya kiuchaguzi, na yule mgombania kiti kile, pia naye ataweza kushitakiwa na kuangaliwa sheria inayostaili, itimizwe.

Kuna taabu fulani tunaziona, ni kwamba chama kinacho ongoza, kwa hivi sasa tunajua ni Kanu, labda hatujui baada ya kura ijayo itakua ni chama gani. Lakini kuna matatizo kwamba chama kinacho ongoza nchi siku zote hakiwezi kujikata, au kujitoa na mwenendo na sera ya serikali. Mfano ni kwamba utakuta chama kinacho tawala, kinatumia fursa za kiserikali, kufanya mambo yake. Tunaomba Katiba itilie umuhimu jambo ili kwamba, serikali iwe ni serikali, na mwenendo na sera za serikali ziwe hazitaingiliana na chama chochote. Vyama vyote viwe ni sawa kwa serikali. Kusiwe na kubagua, vyombo vya serikali vinatumiwa vibaya. Kwa mfano administration, security, na chama kinachotawala. Kwa hivyo tunaomba kuwe na delinking process, baina ya party, whether in leadership; or not in leadership pamoja na Civil Service.

Jambo la mwisho Makamishena ambalo ningependa kusema ni kwamba, kumekua na fujo jingi, kwamba wadhfa wa Rais usizidi terms mbili, za miaka mitano mitano. Sababu zimetolewa na hivi sasa, nafikiri Katiba tulionayo ndivyo inavyo simamia. Tunapendekeza sisi kwamba, isiwe hukumu hii inasikika tu, kwa wadhfa wa Rais, tunapendekeza kwamba, hata wabunge, hata madiwani, hata ma-mayors, wasizidi miaka mitano mitano mara mbili, yaani they should not go beyond five years two terms in the office. After that ninapendekeza wananchi ni wengi, vijana wanakuja wengi, viongozi wa kesho, wamekua ni viongozi wa kesho, kwa miaka mingi. Wakati umefika viongozi wa kesho, wa-take over, wawe ni viongozi wa leo. Kwa hivyo baada ya two terms, five years in office; wawe watawacha, wapate fursa watu wengine kuongoza nchi hii. Kwa hayo machache makamishena tunawashukuru. Asanteni sana, na kwetu sote, tuwe na uchaguzi mwema.

**Com. Salome**: Asante Bwana dakitari keti hapo hapo, tuangalie kama kuna mtu mwenye swali kwako.

**Com. Pastor Ayonga**: Bwana dakitari umesema maneno mengi mazuri sana. Nimekua nikingojea kama ungeweza kusema kidogo juu ya mambo ya afya. Watu wanasumbuka, hakuna madawa, mara hakuna madakitari ambao wanahudumia watu. Ningalipenda katika msemo wako ungaliweka uzito mwingi juu ya afya ya kimsingi, na kuendeleza maisha ya watu kwa njia inayofaa, katika utawala wowote. Afya is a basic right ya kila mtu. Ningalipenda kukuliza ungeweza ku-improve hiyo memorandum yako, ukaongeza mambo ya afya. Itasikika vizuri sana kwamba dakitari amelalamikia afya ya watu kwamba sio mzuri, na watu hawapati huduma za kutosha. Neno lingine hilo sitaki jibu kwa maana huna, ni maoni tu nami nimetoa kwangu, yakukuambia tafadhali ungeendeleza upande huo pia. Kitu kimoja ambacho pengine pia si kuelewa vizuri, na nataka tu uniambie ndivyo au sivyo; umesema katika matumizi ya campaign, mtu asitumie zaidi ya laki mia mbili hamsini au mbili unusu.

**Dr. Kibwana**: Nimesema kwa wale wagombaniaji ubunge.

**Com. Salome**: Ungegonja kwanza, subiri dakitari mimi pia nina maswali, ndio ukayajibu pamoja; pengine ungeyaandika chini. Kwanza ningetaka kusema mwana Tume mwenzangu hakuniomba nafasi ya kutoa maoni yake; kwa hivyo hiyo tunaweza ku-delete lakini, the spirit ya kua tungetaka kusikia maoni ya dakitari kwa hali ya afya ni nzuri. Lakini hilo swalilazima ujibu. Bwana Tume ataniomba nafasi atoe maoni yake, halafu tutayachukulia hapo. Mimi ninaswali moja, umesema kila mtu akishatumika kwa vipindi viwili vya miaka tano kila moja, wote watolewe. Na mimi kama naona nchi kila kiogonzi sasa ni mpya. Bunge imeanza leo, hakuna mwenye anajua standing orders, wote ni wapya, hakuna mtu anajua inafanywa nini, kila mtu ni mpya. Ama madiwani wote wamekuja wapya, continuation process. Mlipofikiria haya, mliona kuwa tutawakilisha vipi kua hakuna kila mara kua na destraction ya kua ile mambo tulifanya jana, yote yamesaulika, kwani kila mtu ni mpya, twanzia upya. Najua baada ya miaka fulani wengine watakuja, na hawajamaliza miaka miwili; lakini ile ya mwanzo tutaianzia vipi? Na pia ningetaka kuomba kama sakafuni kuna mtu mwenye swali kwa dakitari, lakini swali la ufafanuzi tu, sio la mjadala. Hebu mpe microphone tafadhali. Njoo huku mbele nikupe microphone yangu.

**Mohamed**: Asante sana Kamishena, mimi ni Mohamed, ningetaka ufafanuzi kwa dakitari, pale aliposema watu wasiruhusiwe kuhama vyama vyao vya kisiasa. Ningependa atueleze, ni muda gani wakae, kabla ya kuruhusiwa na chama kipya, kushiriki katika uchaguzi.

**Com. Salome**: Dakitari nitakupa nafasi uyajibu yenye unaweza kujibu, yenye utafikiria baadaye basi tuandikie kwenye memorandum yako tafadhali.

**Dr. Kibwana**: Leo nilitaka kuongea juu ya sera na utaratibu wa uchaguzi; siku nyingine tukijaliwa labda tukikutana labda tukikutana tutazungumza habari ya afya. Jambo la pili ulikua wataka ufafanuzi kuhusu gharama ambazo wapiganiaji viti, vya ubunge na madiwani, watatumia. Sisi tumependekeza tu kwa sababu tushafanya budget, kwa kwa uhakika; tuliketi tukaangalia ni gharama gani zinatumika, tukaonelea kwamba mpiganiaji ubunge asiruhusiwe kutumia, kwa mambo ya ki-campaign, zaidi ya Kenya shilling million moja. Na mpiganiaji udiwani, tumeketi tukaafikiana kwamba, asiruhusiwe kutumia zaidi ya laki mbili na nusu. Nafikiri nimefafanua hilo. Jambo lingine ambalo Com. Salome ameniuliza, nikuhusu two term five years in the office. Nafikiri nusu amejaribu kulijibu yeye mwenyewe, kwa kusema kwamba kutakua na intersection. Intersection ni kwamba, wale wanaoingia mwaka; huu kuna wengine wataketi kwa terms mbili, kuna wengine labda baada ya term moja watatoka, wengine watakuja. Na nafikiri ndivyo ilivyo, sitaraji mimi kwamba itatokea wakati, sio kwamba haiwezekani, kwamba ati lile kundi lilikua limeingia lote, litatoka wakati wake litolewe lote, lingizwe lingine lote. Nataraji kila wakati kutakua na intersection; kuungamana baina ya viungo hivi ili kazi za ubunge, ama za baraza ya manispaa yawe yakiendelea.

Mbali na hivyo Makamishena mimi naamini, kazi; implementation of policies of the government, as well as the municipality ama county council: if by the Executive arm, which comprises the town clerk, the town treasurer, wao ndio wanaendesha. Tunajua mara nyingi, elective post, hua ni almost ceremonial. Even Ministers, lakini permanent secretaries, officers in the ministries, are the ones who run the ministries.

Swala nililoulizwa na ndugu yangu, Bwana Muhamed Maitha, ni kwamba, kuwe na muda gani; baada ya kuambaiwa hatakubaliwa yule kuteguka kuingia katika chama kingine. Ni wakati gani ataruhusiwa aingie kule na kujihusisha tena kikamilifu katika uchaguzi? Pendekezo letu ni kwamba, kwa kura zile zinazohusika, kwa sababu tumeona hii ni hila, viongozi in common wanalo; wakishakataliwa katika chama kimoja, ambacho wamekua wakizungumzia meme yake wakati wote, ikifika wakati wa nomination wakikataliwa, wanaruka bridge, wanaingia kwa chama kingine. Kwa hivyo kwa wakati ule wa kura, wasiruhusiwe ki Katiba kugeuka kwenda kwenye chama kingine, wangojee kura zifanyike ziishe, wacha yeye sasa alalie huzuni zake. Kura zikishamalizika, zile ambazo zilikua zimeelekea, sasa akitaka kugeuka, akiingie chama kingine; kulingana maana kile alichotaka kitakua kimekua baridi: ataweza kufikiria mara mbili mbili sasa. Awe ataweza kugeuka kujiunga na chama kingine, na kile chama kitakua na sera yake ya kusema, ukishaingia kwa chama chetu, unatakikana uwe ni kiongozi wa kiasi gani, kukubaliwa kupigania kura. Sijui kama nimeweza kujibu hilo nalo. Asante.

**Com. Salome**: Asante sana Bwana dakitari, jiandikishe kwenye hio deski nyingine, na tunakushukuru kwa maoni yako. Sasa ningetaka kusema pia, nitaita moja kwa moja, vile watu walivyojiandikisha. Lakini mbali na hayo tunataka pia kumsikia kila mtu, mkaaji wa kikao hiki cha Changamwe. Kwa hivyo wakati mwingine nikiona nimesikiza watu wa umri Fulani, nikaona kuna mzee miaka yake mingi zaidi, basi nitampa nafasi hata ingawa. Ama nikipata kuna mtu mwenye ulemavu, ama kuna mama au mtoto ambaye angetaka kuchangia; basi nitakuruka wewe, nikampa nafasi huyo mzee, huyu mama, ama huyu mtoto. Kwa hivyo ukiona nimekuruka mara moja, jua tu nitakurudia wakati mwingine, lakini nataka kuwapa watu wa miaka tofauti na wa maoni tofauti, kwa ajili ya maubile ama nini; nafasi tafadhali. Na kwa hayo nitarukia watu Fulani, nikampa nafasi Bwana Mbaruk Atik.

**Mbaruk Atik**: Madugu Ma-commissioners na waliohudhuria hapa. Mimi naitwa Mbaruk Atik. Ni mkaazi wa Bokole. Niko na memorandum, lakini saa ingine naweza kuzungumza mawili matatu kwa ufupi.

Katika mapendekezo, tulio pendekeza sisi, ni kwamba, serikali iwe ni ya Majimbo. Na katika haya Majimbo, mkuu wa Jimbo awe atachaguliwa na wananchi halisi, wa lile Jimbo. Sio wahamiaji, au wakazi tu waliokuja kukaa katika lile Jimbo; wale wakae vile vile, lakini wasiwe na uwezo wa kuchagua mkuu wa Jimbo, wala mkuu wa wilaya. Na katika kila Jimbo, liwe litamchagua mtu moja, ambaye atakua ndiye Rais wa Kenya. Yule Rais wa Kenya, awe atapendekezwa Majimbo yote yalioko Kenya, na muda wake yule Rais usizidi miaka mitano. Ikiwa atakua na tabia nzuri na hali nzuri, hana mambo ya ufisadi wala ya uonevu. Akiwa na mambo kama hayo, basi kamati za Majimbo zikae chini, na simuuzulu; hata kama amekaa kwa mwaka mmoja, au mwezi mmoja. Ikiwa tabia yake si nzuri, aondolewa. Asiwe yeye ndiye anayeuzulu watu. Na urais uende kutegemea Majimbo. Majimbo ikiwa ni kumi, basi ikiwa alopendekeza Jimbo la kwanza, ndio ametoka Rais, baada ya miaka mitano lipendekezwe Jimbo lingine. Mpaka Majimbo yote yale yalioko yawe yamepata Rais. Hii ni kwa sababu ya yale makabila mengine makubwa, yasiyamalize yale madogo. Yale madogo yawe nayo yataweza kupata nafasi ya urais.

Na katika uandikishaji wa mambo ya kazi, mkuu wa wilaya, aunde Tume maalum, ambayo Tume ile, itakua ni ya wakazi halisi, wa ile wilaya. Tume ile ikiwa ni uandikishaji kazi, kama ni wa polisi, wa jeshi, au mashirika, au makampuni; ile Tume iwe ndio itakayosimamia uandikishaji wa kazi hio. Isiwe tu kua mkubwa wa kampuni ile, ni fulani basi fulani yule, akaangalia msuruuo wa upande wake ikawa wote ndio walio na haki ya kuandikwa kazi.

Jambo lingine la tatu, nafikiri litakua la mwisho, upande wangu, ni habari ya elimu. Katika mashule, ya soma watu au wanafunzi wa kabila mbali mbali, au madhehebu mbali mbali. lLkini utaona ikiwa ni Baniani, ndio mwanafunzi akija na ubinda wake, kama dhehebu lake, hana hatia, Kalasinga akija na kilemba chake, hana wasi wasi. Mkorino, au Mkristo, akiingia darasani na msalaba wake, hakuna wakumuuliza. Lakini Muislamu akiingia na kofia, ni hatia kubwa, itambidi hata arudishwe nyumbani, msichana akiwa amevaa ijabu ni makosa. Kwa hivyo jambo kama ili, tunaomba mkuu wa elimu, awe atalisimamia na kuliangalia, kwa nini liwe hivyo. Basi kwa kua pamesemwa mengi, mengine nikama kuyarudia hayo hayo tu, naona hayo

yatosheleze upande wangu.  Asanteni.

**Com. Salome**:  Asante sana kwa maoni yako Bwana Mbaruk. Kuna  mtu anaswali kutoka safafuni, kwake?  Mimi nina swali moja mzee Mbaruk, wewe umesema Tume ya kuajiri watu kazi ifanywe na ifanywe, na watu wenye kutoka wenye Jimbo, ama wakaaji wa huko.  Sasa kazi tofauti kama Bwana dakitari akitaka kuajiri yeye akitaka matakwa yake ya kiufundi: ama Bwana wakili akitaka ya kuajiri, ama pengine hotel ikitaka kuajiri, itakua na yale matakwa yake ya kiufundi kwenye hiyo kazi.  Sasa ungetaka ili Tume liundwe ama hiki kikundi cha kuajiri, kitakua wenyewe ni wafundi ama niwakaaji  tu?

**Mbaruk:**  Ile Tume, ikiwa katika uchaguzi wao, wamekosa mtu wa aina ile basi wawe na uwezo wa kuazima, hata kama nikutoka Ulaya, au kutoka nchini.  Ikiwa ile kazi walionayo pale hawana mfanyi kazi wake, au hawanamjuzi.  Basi wawe na haki ya kuazima mjuzi kutoka sehemu nyingine.

**Com. Salome**:  Asante kwa hilo jibu, lakini niliuliza wenyewe wenye hao watu, watakua wana Tume, ama wenye shirika lile la kuajiri.  Wenyewe watakua wafundi wa kazi tofauti, ama watakua tu wenyeji wa kutoka huko?

**Mbaruku**:  Wale watakua ni watu tu waliochaguliwa, na yule mkuu pale: sikua ni mafundi, au ma-engineer au nini.  Wao watakua wanachagua tu.

**Com. Salome**:  Asante sana.  Sasa ni nafasi ya Swaleh Hamisi.  Ni wewe?  Karibu.

**Swale Hamisi**:  Bwana Commissioners, mimi ningependa kuzungumzian governance.

**Com. Salome**:  Tutashika hayo maneno kwenye kanda kwa hivyo kila mtu mwenye kuja hapa aanze na majina yake.

**Swale Hamisi**: Jina langu naitwa Swaleh Hamisi.  Mimi ni  forensic scientist.  Sasa mimi naomba kuzungumzia kuhusu governance.  Nafikiri, miongoni mwa maoni ambayo nimepata kutoka kwa baadhi ya watu ambao nimezungumza nao; nikua hicho kiti cha Rais, the Executive Arm of the Government, ina uwezo mkubwa sana, ambao mpaka unafanya, the other arms of the government, hasiwezi kutoa  effective checks and balances.  Kwa hivyo tunaomba, madaraka ambayo anayo Rais kwa sasa yapunguzwe.

Halafu vile vile serikali ambayo tuko nayo sasa, labda ni marriage ya two systems of governavance; tuna parliamentary system ambayo hii hua haiandamani na presidential system of governance.  Kwa hivyo tungeomba iwe redefined tuwe na clear cut system of government.  Na vile vile kuna matatizo katika uongozi wa maeneo, kwa sababu, wako wale ambao wamechaguliwa na wananchi katika sehemu za ubunge na za udiwani.  Katika sehemu hizo hizo, hua tuko na very strong provincial administration.  Na sema katika maeneo ya ubunge kuna wale ambao tumewachagua kama wabunge, na madiwani, na sehemu

hizo hizo, tuna very strong provincial adminitration, mpaka roles za hao watu, saa zingine, zinakua confused. Unapata DO ambaye ameletwa na serikali, anauwezo zaidi, kuliko mbunge ambaye amechaguliwa na wananchi, katika maeneo fulani. Kwa hivyo katika mapendekezo, twapendekeza kua, kuwe na Federal government, na kuwe na Rais kama head of state; and there shall be a bicameral system of government, with a senate, and house of representatives. Na vile vile twapendekeza kuwe na federal government, kwa ufupi Majimbo. Na tuna propose kua Rais kwa sababu sasa kidogo haifahamiki vizuri, Rais asiwe mbunge, kwa sababu kabla haijajulikana kama amepata kiti cha ubunge, ama bado, hua tayari amepewa nafasi, ya kusimamia kiti cha Rais. Kwa hivyo sisi twaona katika mapendekezo yetu: Rais isiwe ni lazima yeye awe mbunge.

Na kuogopea, kama mambo ambayo yametokea 1997, kua mpaka baada ya mwaka mmoja hatuna Makamu wa Rais; huyu Rais awe na running mate: kwa sababu kama Rais angekufa baada ya miezi mitatu kutoka uchaguzi, na kulikua hakuna Makamu wa Rais, mpaka baada ya mwaka mmoja, sijui Kenya ingeingia katika hali gani. Kwa hivyo tungependekeza katika uchaguzi, lazima Rais awe na running mate, ili wakati wa kutawazwa kama Rais, wakati huo huo pia Makamu wa Rais awe tayari anajulikana.

Halafu kwa sababu ya hali yetu ya kiuchumi katika Kenya, na kwa sababu ya uwezo mkubwa ambao anao Rais; tunaona anachagua ministries nyingi, kwa sababu tu ya kutaka kuwahonga watu Fulani, ambao wamemfanyia kazi ya campaign. Kwa hivyo tunaomba katika Katiba mpya, tuwe na wizara kumi na tano peke yake. Hizo ziorodheshwe katika Katiba. Rais asiwe na uwezo wa kuamua kuongeza, ama kupunguza wizara ngapi katika serikali. Kwa hivyo tungependekeza wizara ya kwanza itakua ni health na environment, na ya pili itakua ni finance and economic planning. Ya tatu itakua ni land housing and settlement, wizara ya nne ya education, wizara ya tano ya transport and communication, wizara ya sita, itakua energy and natural resources, wizara ya saba itakua Labour, wizara ya nane Water Development, Wizara ya tisa, culture and social service. Wizara ya kumi, foreign affairs and international relations, wizara ya kumi na moja defence and internal security, wizara ya kumi na mbili, itakua ya local government, wizara ya kumi na tatu itakua tourism and wildlife. Wizara ya kumi na nne, itakua agriculture, na wizara ya kumi na tano itakua ni Justice ministry.

Na katika huo mfumo wa Majimbo, kutakua na regional government based on the current provincial boundaries. And the regional governement shall be headed by a governor, who shall elected by the people, and he shall possess the following qualifications. kwanza lazima awe ni Mkenya, na awe ni mwenyeji wa Jimbo lile. Kisha umri wake usiwe chini ya miaka thelathini na tano. Na itakua uzuri akiwa atakua ana degree, na vile vile awe ana proven leadership experience. Lazima awe ashawahi kua kiongozi, kabla ya kutetea kua governor, lazima awe ashakua kiongozi sehemu Fulani, na awe na very high moral integrity. Hizo ndio qualities za governor ambaye tunataka.

Katika local government, tutakua na local authorities, ambazo zitakua cities zinazongozwa na mayors; na towns na county councils zitakazongozwa na ma-chairman respectively. Na mayor tumependekeza, na fikiri hii nitakua marudio, awe anachaguliwa na watu, sio madiwani. Kwa sababu twaona sasa ni rahisi sana kumweka, na kumuondoa mayor, na hua ni

maoni ya watu wachache sana. Kwa hivyo tunaomba awe mayor anaweza kuwekwa, na anaweza kuondolewa na wananchi wenyewe wa sehemu hile. Na vile vile asiwe chini ya miaka thelathini na tano, na awe na university degree, na pia awe ashawahi kua kiongozi; sio wiki hii wewe nimfanyi kazi wa Port, wiki ijayo usimamie kua mayor na hujakua hata shop steward katika union ya Port. At least lazima uwe unaushahidi wa kua ushawahi kua kiongozi. Na town council na county council chairmen, pia na wasiwe chini ya miaka thelathini na tano, na kwa sehemu hizo tunasema, at least mtu awe amefanya O-Level, with a C grade, minimum. Na lazima pia kabla hujakua chairman wa county council, ama town council, lazima kuwe kuna ushahidi, kuwa wewe ushawahi kua kiongozi, tena ambaye amefaulu katika mambo yake, katika sehemu fulani. Na katika mfumo huo wa Majimbo kutakua na Federal Parliament kama vile nilivyo waambia itakua ni bicameral. Kwanza tutakua na senate, ambayo sisi tumependekeza, hao senators will be elected by the regional assembly.

**Com. Salome**: Jaribu kumalizia kwa dakika moja nyingine.

**Swaleh:** Kwani ulikua umenipa gapi?

**Com. Salome**: Una memorandum, sivyo?

**Swaleh**: La sivyo? Kwa hivyo bado gapi?

**Com. Salome**: Moja.

**Swaleh:** Samahani kidogo. Kea hivyo tumesema hizi regional assembly, ndio watagua wakichakua senators, na twa-propose, kila reginal assembly, itachagua senators wawili. Qualifications zao ziwe, ni watu wasio chini ya miaka thelathini na tano, na senator lazima awe na degree, na awe vile vile, ana high moral integrity. Si mtu ambaye anajulikana kwa mambo wa corruption, na nini na nini. House of Representatives itakua vile vile ni kama hivyo, na regional assembly; ambazo hizi ndizo zitakua bunge za hayo maeneo, watakua kila constituency ambayo iko sasa, tunachagua members wawili, ambao watakaa kwa reginal assembly, na watakua na sifa kama za hawa representative wengine.

Na uwezo na majukumu ambayo watakua nayo hao senators, ni kua: they will have the powers to impeach the President, the Vice President, and the holders of the Constitutional offices. They will also approve bills from the house of representatives, and they will vet and approve presidential appointments. Hayo ndio majukumu ya senators. Na house of representative: they will introduce motions and bills, including amendments to the Constitution. And they will discuss and approve the budget. Regional assemblies, majukumu yao, kumalizia; itakua ni kujadili mambo kuhusu maeneo yao, na vile vile ku-discusss regional budget. Nafikiri hapo nimefikia mwisho.

**Com. Salome**: Are you going to leave us that memorandum?

**Swale**: Nitaacha.

**Com. Salome**: Lakini nilikuuliza kama una memorandum, nikupe dakika tano. Kama hauna memorandum, nikupe dakika kumi. Umesema tayari huna memorandum, sasa umemaliza na una memorandum. Tukubaliane ili tuwe tunazungumza habari ya Katiba mpya. Sio langu kupendelea memorandum, ama kukosa kupendelea; langu ni kuchukua kila memorandum nitakayopatia. Kwa hivyo, utanipa memorandum? Kwa hivyo nimekupa dakika kumi, na una memorandum? Asante sana Bwana Swaleh Hamisi. Kuna swali sakafuni? Haya kuna swali kwako.

**Question:** Asante mwenyekiti. Labda katika sifa za viongozi, ambao unapendekeza wawe ni ma-senator, ama hawa wa house of representatives, unataka wawe na sifa gani? Asante.

**Com. Salome**: Hiyo alikua tayari ashasema. Alisema sifa anazotaka ziwe hapo. Naomba kila mtu asikize, huyu ni Bwana wakili, anajua asiposikizwa vile kunaendelea kotini. Hakuna mtu atakaerudia kwa niaba yake. Kwa hivyo tayari ningetaka kukushukuru sana kwa hilo, lakini nimemkaribisha asome memorandum. Ningetaka kumkaribisha Hassan Mzee. Wewe ndio Hassan Mzee? Hautaki kuzungumza? Okay sasa kuna nafasi maalum; nitampa Mheshimiwa aje atueleze maoni yake. Karibu.

**Hon. Ramadhani Seif Kajembe**: Kwanza presiding officer ningechukua nafasi hii hasa kuwashukuru kwa kufika katika constituency yangu, nimeona mipango iliopangwa, ni kwamba muendeshe kazi yenu vizuri.

**Com. Salome**: Tafadhali Mheshimiwa aanza na majina yako kamili, kwani tunaweka record. Ingawa kila mtu anakuchua.

**Hon. Ramadhani**: Mimi naitwa Ramadhani Seif Kajembe, ni mbunge wa Changamwe. Box yangu ni 88031 Mombasa. Naichukua nafasi hii, kuwashukuru kwa kuja kuchukua maoni, katika sehemu hii kama ilivyopangwa; na nimeona kuna umuhimu nije, kwa dakika chache tu, kwa sababu saa nane nitahudhuria kikao cha bunge huko Nairobi. Basi nikaona nipite kidogo, nami nijulikane nimefika, niombe msamaha, na nielekee Nairobi.

Basi nikichukua nafasi hii, kwanza napenda kusema kwamba, sisi tukiwa chama cha Kanu kwa jumla, tutatoa ratiba yetu, mapendekezo yetu kuhusu vile ambavyo, tungependelea Katiba mpya iwe. Lakini hiyo pia, nikiwa mwananchi wa Kenya, nikiwa mbunge pia, nina wajibu wa kutoa maoni yangu, kulingana na ule uhuru ambao uko. Basi katika maoni yangu mimi nasema kwamba, katika Katiba mpya, ni muhimu turudishe Katiba ya 1963, ile ambayo ilitungwa Lancaster House. Ambayo Katiba hiyo ya mwaka wa 1963, inatoa haki sawa katika sehemu za mikoa. Inatoa mambo ya regional assembly, inatoa mapendekezo kadhaa, ambayo yanafaidi wananchi, katika sehemu ambazo wako. Ikifanyika hivyo, pia juu ya ugawanyaji wa rasmali, uchumi wa kila sehemu. Lazima kuwe na mpango kwamba, pesa zinazokusanywa kwa kila mkoa, kuwe na kima maalum, ambacho kinabakia katika mkoa, na sehemu fulani kwenda katika serikali kuu. Basi mapendekezo yangu katika

Jambo ili ni kwamba, sitini kwa mia ya pato, linalopatikana kwa kila mkoa, libakie katika mikoa. Arubaini kwa mia, ipelekwe kwa serikali kuu. Basi arubaini kwa mia ambayo inakwenda katika serikali kuu, iweze kufidia zile wizara kama, defence ambayo inachukua majeshi yote, foreign affairs na pia ku-subsidize yaani ile mikao ambayo haina mapato ya kutosha, ili kwamba serikali kubwa, iweze kuwashikilia wale wengine, kutokana na ile arubaini ya kila mia inayokwenda huko. Kwa hivyo nafikiri Katiba ya mwaka wa sitini na tatu, vile ilivyoondolewa na serikali, iliondolewa ki mabavu, kwa sababu ilikua ni bunge la sukumwa, la pelekwa huko, wakati wa chama kimoja. Na ikiwa Katiba ya mwaka sitini na tatu, itawekwa iwe ni sehemu ya Katiba mpya, itapunguza ule wakati ambao, nyinyi Mamishena, mnaona itachukua muda wa kumaliza shughuli hii.

Basi katika structure ya serikali; mapendekezo yangu ni kwamba, tuwe na Rais ambaye ni ceremonal. Tuwe na makamu wake wa Rais ambaye pia ni ceremonial; wawe wakishughulikia torati na mambo kama hayo ya kitaifa. Lakini pia tuwe na Waziri mkuu, ambaye shughuli zake zitakua ni kupeleka serikali yenyewe. Na chini ya waziri mkuu, basi tuwe na two Deputy Prime Ministers, mmoja akiwa ni wa administration, na mwingine anashughulisha na mambo mengine, kama ya bunge, na mambo kama hayo. Pia kuna umuhimu juu ya wizara zile zitakazo kua zimekubalika, lakini wakati wa ku-appoint all senior positions, mawaziri, manaibu wa mawaziri, makatibu, na maofisa wakubwa wa serikali: basi wawe vetted na Parliament. Parliament ndio iwe nauwezo wa kua-vet, ilikwamba waendelea na kazi zao. Pia mapendekezo yangu ni kwamba, ikiwa mtu amechaguliwa ni wa wizara Fulani, kwa mfano kama wizara ya afya, unakwenda chukua major general, au major what; retired major unamweka minister for health, at least yule waziri naye, awe anaujuzi angalau kiasi Fulani, juu ya ile wizara ambaye anaipeleka.

Juu ya uwezo wa Rais, nafikiri kuna haja upunguzwe. Nanikuzungumzia kuna haja ya upunguzwe ni kwamba sasa Rais asihusike na mambo ya bunge. Bunge liwe na uhuru wake sasa. Awe, yeye kama ceremonial president, anaweza kualikwa na bunge, kwa mambo mengine; lakini awe hana uwezo wa kuvunja bunge, au kulifungua bunge. Hiyo ni kusema bunge enyewe, liwe na ratiba yake. Liwe na ratiba kusema, katika miaka tuliochaguliwa; basi bunge litafungwa hapa, litapelekwa hivi, litafanya mambo kama hayo.

Na kunakitu ambacho kinaendelea sasa kwa mfano wakati huu tuna nyinyi mnatuongoza katika kutengeza Katiba. Lakini Parliament wakati huu, haswa wabunge wa opposition, haswa, twasema hivi: wanaleta motions Fulani, Fulani, ambazo zinaabatana na mambo ya Katiba. Nafikiri wakati tunafanya kuunda Katiba motion hizi ambazo zitakua zina-influence commission, au zitaingilia mambo ya utengenezaji wa Katiba, ziwe simuhimu, kuweza kutekelezwa na wabunge, kwa wakati huu; kwa sababu pia zinakua ni matatizo. Hiyo ni kusema kwamba, ingawaje tunasema katiba inaweza kubadilishwa na 2/3 majority: basi ni lazima kabla kifungu chochote cha katiba hakijabadilishwa, kuwe na mashauriano ya kutosha, haswa kutoka kwa raia. Kubadilishwa kwa kifungu cha Katiba, lazima kuwe kuna referendum. Kumekua na ushauri kwa wananchi, halafu ndio wabunge waweze kupelekewa, ndio wapitishe katiba kwa two third majority. Badala ya sisi kukaa pale bunge, na kusema, tumefika two third majority, tubadilishe. Hiyo ni kusema tunaweza kufanya jambo, ambalo haliwapendezi wananchi.

Juu ya maisha ya bunge. Nafikiri maisha ya bunge, ikiwa ni miaka mitano, basi yafike pale miaka mitano. Kwa mkataba ulioko kati ya wabunge na wananchi, ni miaka mitano. Sasa ikiwa wabunge wanaweza kukaa bunge, na tuseme tumeongeza mwaka mmoja, au miwili, na katiba ya sasa inasema tunaweza kuongeza mwaka mmoja; ikifika mwisho tukaongeza wapili, lakini isizidi miaka mitano. Ikiwa kuna vita, au kuna njaa, nafikiri, whatever the case, kabla bunge halijafikiriwa kuongeza maisha, yake ni lazima wananchi wajue kwamba; kweli kuna haja ya kuongeza maisha ya bunge. Badala ya wabunge tu kukaa na kufanya uamuzi kama huo.

Juu ya mambo ya local authorities. Mpaka sasa mimi naunga mkono, mayor achaguliwe na madiwani. Na sababu zangu ni kwamba, nchi hii yetu ya Kenya imetawaliwa na ukabila. Sehemu ambapo kabila ni kubwa, linaweza kunyanyasa makabila madogo. Wakatumia wingi wao wakaweka mayor. Lakini ikiwa kila sehemu inayohusika, katika local authority ikichagua diwani, na madiwani waamue juu mayor, hiyo ingefaa. Mahali pengine, labda katika urban areas, tukisema mayor achaguliwe na watu wote labda it applies. Lakini kuna sehemu nyingine, makabila makubwa, yatatumia uwezo wao kuweka mayor. Hiyo ni kusema, makabila madogo, hayatapata nafasi.

Mwishowe, nikimaliza kwa vile naenda safari. Katiba ya sasa itowe uhuru kamili kwa minority groups. Hivi sasa, nitakupa mfano, katika utawala uliokwisha, na utawala ule ambao uko sasa; Pwani ni moja katika sehemu ambayo inakaliwa na minority groups. Ardhi yetu yote imechukuliwa, na wale ambao wanauwezo katika serikali. Sasa utaona kwamba wananchi katika sehemu hii, wenyewe, indigenous; wamekosa ardhi. Na wale ambao wamekuja wakachukua ardhi, wameuza wakapata hela nyingi, wanawaita watu wa pwani maskini, wakati utajiri wao wameunyakua kutoka hapo. Nafikiri, juu ya ugawaji wa ardhi, kila mtu apewe ardhi pahali alipozaliwa; au ni kwao, apewe ardhi hapo, badala ya mtu kwenda kunyakua ardhi ya watu wengine, mahali kwingine.

Basi kwa hayo machache, nachukua nafasi hii, labda nikimalizia kusema, manifesto ya vyama vyote vya siasa katika Kenya inasema itatoa elimu ya bure. Manifesto ya Kanu na vyama vingine. Wanasema watapata watoto wa Kenya elimu ya bure. Lakini yuko mtoto leo anapata elimu ya bure? Nafikiri kuna umuhimu, katiba itungwe, na ndio ikatayotoa uwezo; kuilazimisha serikali, kwa sababu katiba ni mkataba kati ya mtawala, na anaye tawaliwa. Kwa hivyo, Katiba itowe uwezo kwamba kweli, mtoto wa Kenya apate elimu ya bure, akasome bure skuli bila kulipa fees, angaliwe, ajengewe shule na serikali, shule zitiwe taa na maji, na mpaka kiwango cha O-Level. Kusudi, hivi sasa, watoto wale ambao wanatoka katika familia maskini, na hawana uwezo; hawawezi kusoma kwa sababu baba zao hawana hela. Utaona watoto wa matajiri, hata kama halijui, lasukumwa tu; na siku moja litakua naolatawala watu wengine, kwa njia nyingine. Kwa hivyo free education, ni lazima isisitizwe sana, katika Katiba hii; na watoto walindwe vile inavyotakikana. Ingawaje saa hii, tuna act inayolinda mtoto, lakini haijakua very strong. Nafikiri ni muhimu kuongeza hii, katika Katiba. Kwa hayo machache, nasema asante.

**Com. Salome**. Asante sana Mheshimiwa, na asante kwa kutukaribisha kwenye kikao chako cha bunge. Kuna swali kwa mheshimiwa. La toka sakafuni. Okay.

**Question:** Asante Commissioners, nilikua napenda kumuuliza Mheshimiwa afafanue kidogo; kwa sababu amesema kuwe na Rais na waziri mkuu. Hapo labda angetudokezea, angependa uchaguzi wa Rais uwe vipi? Na uchaguzi wa waziri mkuu utakua namna gani.

**Com. Salome**: Asante kwa hilo swali, mheshimiwa tafadhali.

**Hon. Ramadhani.** Mimi, unajua mambo ambayo katika nchi yetu ya Kenya, yamefanya wananchi kwamba hatuaminiani sana. Na haswa tukiwa makabila tofauti hatuaminia. Na hujui nani akwambia kweli, nani akwambia urongo. Kwa hivyo, katika uchaguzi wa Rais, ambaye nimesema atakua ni ceremonial na makamu wake, na Prime Minister. Lazima kuwe na ballot paper. Mwananchi akienda, anamchagua Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu na Deputy Prime Minister wawili. Nasema hivyo kwa sababu, hatutaki mahali siku moja, Rais aseme nimemfuta Prime Minister, au Prime Minister aseme nimemfuta Deputy Prime Minister. Kila mtu awe amechaguliwa directly na wananchi na hakuna mwingine anaweza kumuondoa mwingine.

**Com. Salome**: Asante sana mheshimiwa, tafadhali utajiandikisha kule, na tunakushukuru kwa kuja kutuzugumzia leo asubuhi. Sasa namwita Mwinyi Mita.

**Mwinyi Mita**: Salaam Aleikum. Jina langu, naitwa Mwinyi Mita Ali. Mimi by training ni mhasibu, na nafanya biashara hapa mjini Mombasa. Maoni yangu kuhusu mambo ya Katiba, ningependa kuzungumzia maswala ya ardhi, na mambo ya uenyeji. Ningependa Katiba mpya kwanza iorodheshe kwa uwazi, makabila yote ya Kenya. Hapo nyuma kidogo, sisi kama wazaliwa wa Changamwe, ambao miaka yote sisi twajijua kama ni wa Changamwe, tulikua twapata shida kujiandikisha, kwa mambo ya vitambulisho, ama passport. Ulikua ukisema ni Mchangamwe, unaambiwa Kenya hakuna kabila ya Wachangamwe.

Sasa ingekua jambo la busara, kama makabila yote ya Kenya, kama ni arubaini na sita, au arubaini na nane, yawe yataorodheshwa kwenye katiba uwazi. Kabila za Kenya ni kama zifuatavyo. Kila kabila, na mahali kabila lile ambapo lapatikana: ikiwa wewe ni mkamba, ijulikane unatoka Eastern Province. Ikiwa wewe ni Mkikuyu, inajulikana unatoka, Central Province. Ikiwa wewe ni Mjaluo unatoka Nyanza Province. Hii itawezesha kila Kabila, kua na haki sawa, katika nchi yetu.

Tukija kwenya maswala ya ardhi, sasa custodian wa ardhi nafikiri ni Rais. Ikiwa ardhi yote ni mali ya serikali. Hii imeleta matatizo mengi, kuhusu maswala ya ardhi, watu ambao hawahusiki na sehemu zile zilipo, wameweza kupata allocation za ardhi, na wale watu ambao ni wakaaji ni wenyeji wa sehemu zile, wakati mwingine wamekosa kupewa ardhi, kwenye sehemu ambazo ardhi zile ni za babu zao na ancentors wao. Sasa itakua jambo la busara ikiwa custodianship ya ardhi, itapewa community, badala ya kupewa central government. Iwe kutakua na community leaders, ambao ni trustees wa ile ardhi, na ikiwa imetokea allocation, wao watakua wanajua ni mtu gani ambaye anafaa kupewa ardhi, kwenye sehemu zile. Isiwe ardhi zinagawanywa kama zawadi za kisiasa, ama kikabila, ama kwa njia zingine zozote zisizofaa. Halafu tumeona kuna wananchi wengi ambao kwa

sababu moja ama nyingine wameweza kupata ardhi kubwa sana; kufikia kiwango kuwa ardhi ile hawana matumizi nayo. Pendekezo langu ni kua, ikiwa kutakua na idle farm land, mtu ana land kubwa ya ukulima ambayo haitumii, ikipita miaka miwili, ile extra land, zaidi ya heka hamsini, iwe itaweza kua confisficated, irudishiwe community: na community, will decide, ni nani ambaye anahitaji ardhi ile, aweze kuitumia. Badala ya ardhi iwe inakaa pale kwa muda mrefu hainufaishi mtu yeyote.

Halafu ningependekeza pia, kwa sababu ya makabila, kama alivyosema mheshimiwa, kabila nyingine ni kubwa, nyingine ni ndogo. Lakini kabila zote ni bora ikiwa zitakua zinapata haki sawa, kutoka kwa Katiba ya nchi. Kwa hivyo, ningependekeza, ikiwa Katiba mpya itaweza kuandika kwa uwazi, kua immigrant communities, kwa mfano, badala ya kua Katiba itasema, kabila Fulani, inatoka sehemu fulani. Ikiwa mtu atahama kwenda Kabila nyingine, ikiwa ni kwa mambo ya kazi, mambo ya biashara, iwe yeye atafanya kazi na biashara kwenye ile sehemu aliohamia; lakini asiwe aweza kusimamia mambo yeyote ya uongozi. Hii, itawezesha makabila yote kupata nafasi ya kujiongoza. Kwa mfano ikiwa ni jambo la ubunge, iwe kila kabila, litaweza kua na mbunge bungeni. Kwa sasa nafikiri bunge letu tuna wabunge mia mbili, na makabila tulionayo ni arubaini na nane. Lakini utakuta kuna makabila mengine, hayamo katika wale watu mia mbili. Watu hawa ambao kabila yao haiko represented; ni nani atakaye kua anasimamia mahitaji yao? Itakua jambo nzuri, kama all the Kenyan tribes, zitakua represented in Parliament. Ikiwa ni mambo ya administration, ikiwa ni mambo ya political leadership, iwe immigrant communities haziwezi kuhusika. Wawe wao watapiga kura, lakini wawapigie kura, wale wenyeji wa sehemu ile. Nikisema hivi, namaanisha kua, mimi napendekeza kuwe na serikali ya Majimbo, na ile serikali ya Majimbo iwe itatawaliwa na wale wanati, wale wenyeji wa pale. Halafu iwe serikali itakua na power ikiwa pengine, central government inaona wanahitaji ardhi kwa mahitaji Fulani, ambayo yatanufaisha nchi nzima. Wawe wana-power ya kuweza kuiomba ile ardhi, kutoka kwa community, ambayo wame-hold kama trust; ili waweze kufanya mambo ambayo yatanufaisha nchi nzima. Lakini iwe wata-compensate ile community adequately.

**Com. Salome**: Mr. Mvita do you have a memorandum?

**Mvita:** Sina. Nimeandika in a rough form my thoughts, lakini sina memorandum.

**Com. Salome**: Then you have three minutes.

**Mvita:** Nafikiri nimemaliza.

**Com. Salome**: Kuna swali kwa Bwana Mvita?

**Com. Pastor Ayonga**: Ndugu Mvita, umezungumzia juu ya, mtu akihamia pahali pengine, ile sehemu ambayo amehamia, asipewe uongonzi. Sijui hii itakua namna gani, ikiwa tunasema Mkenya anaweza kuishi kokote katika Kenya; na anaweza kuhusishwa na mambo yeyote ya uchumi, na elimu na kila kitu, kila pahali alipo. Lakini nashindwa kuelewa, kama pia watu ndio wanaomchagua mtu, na wamempenda mtu, na wameona huyu aweza kutusaidia hivi na hivi, wangekataa kuhusishwa mtu

kama huyu? Na hali tunataka kuua ukabila. Mara tunazungumzia ukabila, jinsi ambavyo umeleta mambo, makabila mengine yananyanyasa wengine, makabila madogo hawawezi kupata nafasi zao. Tutauuanje huu ukabila, kama bado tutakua tukiweka visehemu fulani fulani, mifuko Fulani, Fulani, katika maisha yetu ya kusema, oh kama ulitoka pande ile hii uwezi. Na hali tumetaka kua Kenya moja. Unity ya kua Wakenya. Hayo mambo yatakua namna gani? Ungeweza kufafanua kidogo?

**Com. Salome**: Nami nina swali moja kwako, kufuatilia hiyo habari mwana Tume mwenzangu ameuliza. Mimi nataka kuuliza, mtu mwenye amehama ni yupi? Ni yule alihama in this generation, ama hata yule atazaliwa huko na aliehamia hapo; pia atakua mhamiaji maisha yake yote? yeye hajui kule baba yake au nyanyake alikotoka. Katika nchi zingine ukishakaa vizazi Fulani, unakubalika kua wewe mwenyeji.

**Mwinyi:** Asanteni ndugu Makamishena kwa maswali yenu mazuri. Ningependa kufafanua. Kamishena wa kwanza aliuliza ni jinsi gani tutauua ukabila, ikiwa sisi tutapendekeza kua kabila nyingine isiweze kusimamia uongozi, katika sehemu nyingine. Jawabu langu ni kwamba, ukabila peke yake; kama tuseme Mchangamwe, Mkamba, Mjalua, Mkalenjini. Ukabila peke yake si ubaya. Ubaya unaletwa, pindi kabila moja, ama kabila mbili, zitakua zinachukua kila kitu. Ikiwa kabila zingine hazipewi haki zao, ndio shida ya ukabila inatokea. Ndio katika mapendekezo nikasema, itakua bora, ikiwa kila kabila, itapewa haki ya kujitawala. Hii ita-provide checks and balances, kwa sababu wao wataweza kupigania, yale matatizo ya kabila lile, kule kwenye bunge. Itakua kama choir ambapo tuna saprano, tuna bass, kila mtu atakua ana role, katika ile choi. Lakini ikiwa ni sauti moja tu ndio zinasikika, hizo nyimbo zitakua ni boring sana.

Swala la pili, ilikua ni kizazi gani ambacho sisi tutachukulia kua kimehamia ama ambacho kitakua hakiruhusiwi kusimamia ule uongozi? Mimi ningependa kusema, baada ya kuzi-list zile kabila za Kenya, na sehemu ambazo zinapatikana kwa wingi. Itakua hata kama wewe umezaliwa Mombasa, ukasomea Mombasa, lakini utakua huwezi kusimamia Mombasa. Ikiwa ancestors wako hawakutoka Mombasa. Kwa sababu tukisema hivi, nasema through experience, kuna wakati mmoja hapa Changamwe tuli-elect a Member of Parliament.

**Com. Salome**: Could you please just give me dakika moja. Tafadhali ningetaka kuwakubusha kua tunashika haya maneno kwa kanda moja kwa moja. Kwa sababu kama vile mnavyoona tuna wanatume wawili tu. Kwa hivyo wakati tutakua tukizungumzia mambo gani tuliaambiwa Changamwe; itatubidi kucheza hizo kanda tena, ili kila moja aelewe tulipata maneno gani kutoka hapa. Kukiwa kuna kelele zingine, pengine za ndege, naye ndege pia ana haki ya kutoa maoni yake. Lakini za wale wengine, Mwanadamu, ingefaa tafadhali kama tungemsikiza mwenye kutoa maoni ili yaweze kusikika na kunasa katika kanda kwa hali itakayo sikika. Tafadhali kelele zinazotoka nyuma zatutatiza wakati wa kusikiliza maoni. Endelea tafadhali.

**Mwinyi:** Nilikua nasema tuliwahi kupata matatizo siku za nyuma, tulipomchagua mbunge ambaye, alikua anatoka sehemu za Uukambani. Baada ya ku-serve kwa term moja, ile term ya pili, akahamia Ukambani. Kwa miaka mitano, kazi yake anapotaka mbunge, anaenda kwao Ukambani, anarudi bunge. Ikawa mahitaji yetu, hatuna mjumbe. Sasa ili ndilo tatizo tunajaribu

kuli-address kusema, because immigrant hua mara nyingi hawakati attachment za nyumbani. Akifariki, itabidi akazikwe nyumbani, sasa ndio tukasema, itakua ubora, zile indigenous communities zijitawale wenyewe.

**Com. Salome**: Asante sana Bwana Mvita kwa maoni yako. Sasa ningetaka kumpa nafasi Bwana Cleophas Mawasi. Karibu.

**Cleophas Mawasi**: Asante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuongea yale ambayo tunayofikiria sisi wakaaji wa Mikidani hapa. Na nitalemea sana kwa upande wa walemavu. Kwa majina, mimi naitwa Cleophas Mawasi. Tungependekeza kwamba katika Katiba mpya itakayo undwa, wanapo angalia ili swala la walemavu; kuwepo na vifungu ambavyo vitawekwa, kwa misingi ya matatizo ya walemavu. Maanake matatizo ya walemavu si sawa na matatizo ya wale ambao sio walemavu. Katika wale watu ambao ni maskini, nafikiri walemavu ndio maskini zaidi. Pili wao ndio mara nyingi wananyanyaswa ki-elimu. Mzazi anapokua na watoto wake wawili angependa awapeleke shuleni, halafu apungukiwe na fedha, ana prioritize kwanza yule mtoto ambaye, hana ulemavu aende shule, ndio yule mlemavu aende baadaye.

Kwa upande wa ajira pia, hua mlemavu vile vile, ndio wamwisho kufikiriwa katika kuajiriwa, na wakati wa kupunguzwa, ndio wa kwanza kuondolewa. Pamoja na hivyo, mlemavu yeye ako na restricted mobility, ama uwezo wake wakwenda huko na huko, uko na vikwazo vingi sana. Na mara nyingi yeye, kulingana na itikadi zetu za Kiafrika; anaonekana kama mtu ambaye ni nusu. He is viewed as sub-human. Hiyo inazalisha kwamba, baadaye anatengwa. Na anatengwa pia na jamaa zake. Kwa ufupi mlemavu hana sauti yake, katika Katiba yetu hii ilioko sasa.

Natulipendekeza mambo yafuatayo. Kwanza, kuweko na kifungu, katika Katiba hii mpya, ambacho kitahakikisha kuheshimiwa, au kutekeleza kwa haki za watu wenye ulemavu. Pili, tulipendekeza kwamba, serikali ibuni ofisi; ambayo itakua na matawi nchi nzima. Ofisi hii itakua ina-deal entirely, na maswala ambayo, yanawahusu watu wenye ulemavu. Tatu, tulikua tunapendekeza kwamba, hii sign language, ihusishwe katika training curriculum zote, katika nyanja zote nchini; kwa mfano katika teachers training, kuweko pia na sign language, na vile vile katika police training colleges vile vile, na medical training colleges. Wapewe fursa, ya kufundishwa jinsi ya kuongea na mtu ambaye amepoteza uwezo wake wa kusikia, ili waweze kuelewana.

Kwa wakati huu kwa vile kifungu hicho bado hakija kuweko, ama training hiyo haiko katika ma-colleges mengi; tungependekeza hao ma-sign language interpreters, wawekwe katika ofisi zote za public. Tuseme katika hosipitali, kuweko mtu pale wa kusaidia ku-interprete, huyu mtu anasikia vipi ama anamatatizo gani; wawe wanaweza kuelewana. Halafu pia katika ma-police stations, pasikosekane pale sign language interpreter; kwa maana mara nyingi ma-police wamekosa kumwelewa mtu mwenye matatizo ya kusikia, na wakamfikiria labda ni mjeuri, na anakataa kuona vile anavyofanya. Kumbe yeye anamatatizo ya kusikia, kwa sababu hawaelewani basi akakosa kumfahamu na hakamwadhibu labda ki makosa. Na ofisi zingine zote za public; zikiwa na watu kama hao, kutakua kuna uelewano mzuri, na sisi pia tutajisikia hatukutengwa ama hatukutenganishwa na jamii kwa jumla.

Tano tungependekeza vile vile, hawa watu wenye ulemavu, wasinyimwe fursa ya kuweko katika nafasi, ama post za machifu, DO, na PC. Kwa sasa ni vigumu sana kupata mlemavu moja kwa moja, ambaye anaweza kuingia katika line hiyo. Lakini kukiweko na nafasi kama hiyo, matatizo yetu yanaangaliwa kwa udani zaidi. Halafu sita kuna vifaa ambavyo hua vinaagizwa kutoka nje, kwa madhumuni ya kuja kuwasaidia walemavu; kwa mfano kama, hearing aids, kuna braille material, na pia mobility aids. Vitu kama hivi kwa vile hua vinaagizwa nje, vikiingia nchini, kwa sababu ya tax, inabidi tuvinunue kwa bei ghali sana. Kwa hivyo vitu hivi, vikiwekwa tax free, pengine tunaweza tukazipata pia sisi, kwa bei nafuu. Pia tukiangalia lile swala letu la umaskini, ambao umetubana sana, ikiwa tutavipata kwa bei nzuri; basi sisi pia tutafurahia maisha kama wengine.

Saba katika Katiba yetu ya Kenya, mtu mwenye ulemavu haruhusiwe ku-apply for driving licence. Tulikua tunapenda kufungu hicho pia kiweko, ili walemavu nao pia yako magari ambayo walemavu wanaweza kupeleka- kwa hivyo katika nchi yetu hii ya Kenya pia, walemavu tungependa tufurahie kuendesha magari katika mabarabara zetu. Turuhusiwe pia vile vile kua na driving license, tufurahie maisha zaidi.

Nane; watu wenye ulemavu mpaka sasa, hawajaweza kuruhusiwa kuingia katika mabaraza ya municipal ama bunge. Kwa hivyo tungependa Katiba hiyo ijao, walemavu pia waruhusiwe kuweko katika nafasi hizo za mabaraza, na hata bungeni. Either kwa kupigiwa kura, ama katika nomination pia, wawe wanapewa nafasi zao vile vile.

Tisa hawa watu wenye ulemavu; kuna mashirika mengi nchini, ambayo ni service providers, ama wanausika na mambo ya kusaidia kuinua hali ya maisha ya walemavu. Lakini ukichuguza sana utapata katika management, walemavu wenyewe hawako pale. Unapata wale ambao wanaamua, maamuzi kuhusu walemavu, ni watu ambao hawana ulemavu wowote; kwa hivyo unapata mlemavu ambaye yuko pale chini, isipokua ana mtu katika hiyo management ambaye anamjua, yeye haki zake hazipati. Kwa hivyo kukiwekwa mlemavu pale katika management, nafikiri ataweza kuelewa matatizo ya mlemavu mwenzake zaidi, ili wote wawe na usawa; wapewe haki zao.

Kumi, tungependekeza kubuniwe benki, ambayo itakua inatoa mikopo kwa walemavu, kwa minimum interest rates; ambapo mlemavu anaweza akakopa pesa, na akafanyia maendeleo, na akarudisha percentage kidogo, mbali na ambazo ziko sasa katika benki zile zilizoko. Halafu mlemavu, na wale si walemavu, wanarudisha rates sawa sawa.

Kumi na moja: tungependa pia, Katiba itakayoundwa mpya, ituhakikishie usalama wa mali zetu, sisi kama watu wenye ulemavu. Halafu kumi na mbili, katika jela zetu, wanaingia watu wenye ulemavu, na watu ambao sio wenye ulemavu. Lakini ukiangalia hali ya maisha ya kule ndani, kwa mtu ambaye ni mlemavu, yanakua ni magumu zaidi, kwa sababu ya ule ulemavu wake. Kwa hivyo nilifikiri prison department, ama serikali; kwa ule wingi wa watu wenye ulemavu, wakishashikwa, wawe kwenye wing yao. Accommodated, kwa njia ya nafuu zaidi, kuliko ile ilioko; pamoja na wale ambao hawana ulemavu.

**Com. Salome**: Excuse me? Una memorandum ya kutwachia?

**Mawasi:** Ndio.

**Com. Salome**: Basi nitakupa dakika moja ingine ya kumalizia.

**Mawasi:** Nimemaliza ni ya mwisho hii. Kutengwe ardhi ya kuwaweka watu wenye ulemavu pamaoja, ili hata kama ni kusaidiwa; wasaidiwe wakiwa mahali pamoja. Hii itapunguza kujazana kule mijini wakiomba, na kufanya hivi na vile. Halafu mijengo yote ya umma iwe planned kwa namna ambapo mlemavu anaweza akaifikiria vizuri. Kwa mfano, ofisi ya NSSF, ama yeyote ile, ikiwa itakua iko gorafa ya nane, na hakuna lift; imejam. Itabidi mlemavu ajipandishe na gazi, na inakua kwake yeye ni gumu zaidi. Kwa hivyo nyumba zote ambazo zinahusu public service; ziwe zinaweza kufikiwa kwa urahisi, na watu wenye ulemavu.

Mashule yetu vile vile, yaruhusiwe kuwapokea wanafunzi, ama watoto wenye ulemavu pia: wawekwe katika shule zile, maanake wakati mwingine wanarudishwa nyuma, ama wanakataliwa. Na wakiruhusiwa, katika Katiba ijayo, wanatakikana pia wana haki ya kusoma na wale wengine. Wasije wakatengwa, ama wakajisikia wametengwa zaidi. Kwa hivyo mimi nafikiri kwa ufupi, hayo ndio nilikua nayo, kwa niaba ya watu wenye ulemavu hapa Mikindani. Asante sana.

**Com. Salome**: Asante sana kwa maoni yako Bwana Cleophas. Kuna swali kwake.

**Com. Pastor Ayonga**: Bwana Cleophas, umeongea juu ya sign language; na ukasema mtu awekwe katika kila police station, ili mtu ambaye anahitaji huduma hiyo, akipelekwa station, aweze kushughulikiwa vilivyo. Sijui kama ulifikiria kwamba, watu ambao wanahitaji huduma ya namna hiyo, si wengi sana ambao wanaopatikana katika every police station, na ambao watahitaji huduma hiyo. Mtu anaweza kukaa katika police station siku ya leo, kesho, na kesho kutwa, hajaona mtu wa namna hiyo; na mwishowe akachoka. Police wanapochukua training yao, kwamba pia wafundishe sign language, ili kama kutakuja mtu kule katika police station, ambaye anahitaji huduma hiyo; kungekuwemo a police officer ambaye angeweza kumhudumia mtu wa namna hiyo. Kwa maana, yeye kuwe kuna mtu anataka huduma, wala asiyetaka huduma, atapewa nafasi yake ya kawaida ya kuwa police officer.

**Com. Muigai**: Mimi pia nina swali la kufuatia hilo. Saa zingine, haswa ndugu zetu wenye kuhitaji hiyo huduma ya lugha ya ishara, wenyewe hawajajifunza hiyo lugha. Kama tulikua sijui, pahali fulani tumekua, tumeleta mtu mwenye kutafusiri, na wale wenye walikuja hakujua hiyo lugha wenyewe. Hiyo ungeiambatanishaje na ile ya elimu, ili watoto wasiosikia, ama wasioweza kuzungumza, wakapata elimu yao, ili pia wakaweza kutumia hizi huduma hata zinapokuweko.

**Mawasi:** Asante sana kwa maswali yenu, na nafikiri nilikua nishatangulia kusema kwamba; hii sign language, ifundishwe katika

ma-colleges. Lakini kwa vile kwa hakuna hali hiyo katika ma-colleges, tunatatizo la tayari saa hizi. Hilo ni jambo ambalo linatakikana liangaliwe kwa dharura saa hii. Kwa vile hakuna training kama hiyo, katika training colleges. Nikuangalia jinsi ambavyo tuta-address hiyo problem, kwa sasa hivi. Kwa sababu tatizo hilo liko, na visa ni vingi, vya watu wenye matatizo ya kusikia; ambao wameenda police station, na wakawa charged kwa makosa ambao sio yao. Katika mahosipitali; mara nyingi visa viko vya watu wenye matatizo hayo kupewa vidonge ambavyo sivya ule ugonjwa, ambavyo anaugua. Kwa hivyo kwa sasa hivi, hiyo ilikua ni kama suluhisho la dharura. Ili sasa Katiba itakapokuja, itaidhinisha iwekwe katika colleges, baadaye itabidi wale staff wote, wawe wanaujuzi wa hiyo sign language interpreter.

**Com. Salome**: Asante sana Bwana Mawasi kwa maoni yako. Sasa nataka kumpa nafasi Mama Mwanate Mwinyi. Uko hapa nasi? Karibu.

**Mwanate Mwinyi**: Kwa jina naitwa Mwanate Mwinyi. Naishi mtaa wa Mikindani. Maoni yangu ya kwanza ni kuhusu wakubwa. Tukiangalia katika pwani hii, wakubwa wengi, kwanza kabisa nilikua nataka kusema kua, naonelea wakubwa wa Pwani wengi, wawe ni watu wa hapa Pwani, kwa sababu ukiangalia watu wa pwani hao, ndio wanaojua shida za Pwani hino, na wanaelewa wa Pwani wataka nini, na kila kitu wanachohitaji. Kwanza kabisa tukiangalia kwa upande wa kitambulisho. Wakubwa wengi wakiwa ni watu wa Pwani, mtoto yeyote anayemaliza skuli, na amefikisha umri wa miaka kumi na nane; akitaka kwenda kuchukua kitambulisho, kwa mfano tuseme kua mimi ni Mjomvu utaambiwa kua hakuna kabila la Ujomvu. Ambapo ingekua mtu anayetoka Pwani anajua kabila la Ujomvu. Kwa hivyo hapo ningependelea kua, wakubwa wale wanaotoa kitambulisho wengi wawe ni watu wa Pwani.
Pia tukiangalia katika upande wa wakubwa wengine, kama wabunge, na councillor, hata na chief. Wao ndio twapendelea kua wawe ni watu wa Pwani. Maanake pia wao ndio wanaojua. Kwa mfano hata area ya Changamwe, tukichagua mtu wa kutoka Pwani; yeye ndiye anayeelewa shida za Wapwani wote. Kwa mfano hapa Mikindani, tukichagua mtu wa Pwani yeye ndiye ataelewa shida za watu ambao wanaishi pale, area ya Mikindani na ndio wao watakaotatua kila kitu.

Haswa tukiangalia katika mahosipitali. Mahosipitali mengi utapata kua watu wengi wakubwa ni watu wa Bara. Basi ikiwa wewe ni mtu wa Pwani ukienda pale, ukiulizwa, wewe ni mtu gani? Ukisema kua mimi ni Mariam, basi madaktari wengi pale kama ni wakubwa na ni wa Bara, watakupuuza sana; watakuona wewe ni kama ambaye wewe, watashughulika na wale watu wa kwao, kwa sababu pengine wao wana pesa vile, lakini wewe mtu wa Pwani watakupuuza sana. Hata tukiangalia katika maofisi mengine ukienda waomba kazi, na pengine katika ofisi ile aliye mezani ni mtu wa bara; basi vile utakapo kwenda pale utaambiwa, ukiwa wewe utauliza jina useme mimi naitwa Safi. Mkubwa yule atakataa kitu cha kwanza na, ama saa nyingine anaweza kukubali lakini kwa masharti. Kitu cha kwanza atakutongoza. Na kisha atakapo kutongoza, ukikataa hapo hatakupatia kazi. Lakini ikiwa ni mtu mwingine ametoka Bara atamfanyia kazi kwa haraka, na atapata kazi. Kwa hayo machache asante.

**Com. Salome**: Kuna swali kutoka sakafuni kwa bi Mwanate? Bi. Mwanate umesema mambo mazuri hayo. Hukutueleza juu

ya shida za kina mama, shida za vijana, wewe ni mwanamke na pia wewe ni kijana. Tungetaka uendelee zaidi, wakati mwingine, kuhusu kua wewe ni Mwanapwani, wewe ni wakike, na wewe pia ni kijana. Tungetaka sasa maoni yako kuhusu hayo. Pengine si wakati huu huu lakini tungependelea kujua maoni yako juu ya hayo siku nyingine.

**Mwanate**: Kwa upande wa kina mama, sisi wakina mama twanyanyaswa sana. Tukifika kama vile wataka kazi, watu wanakudharau sana, hawakupatii kazi kabisa kama akina mama. Halafu pia ningependelea pia, kina mama wajitolee kua viongozi, ambao wanajua shida za kina mama wengine, ambao wataongoza jinsi ya kuelimisha watu wa Pwani.

**Com. Salome**: Asante sana Bi-Mwanate Mwinyi. Ibrahim Musa. Hayuko. Micheal Mulewa. Omar Mwinyi. Nasur Kibwana. Kuna KiBwana umezungumza katika kikao kingine? Haya nakupa dakika tano kwani, nishakupa zingine katika kikao kingine.

**Nasur Kibwana**: Bwana Commissioners, tunawakaribisha na nawashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Salaam aleikum, ma bibi na maBwana? Kama mlivyo sikia, yakua nilikuwako kule Kibaya, nikapeana maada ya upande Chief Kadhi. Siwe kurudia hayo sababu ninamengine mpya. Jina langu naitwa Nasur Athman Kibwana, mzaliwa wa hapa Changamwe, niko na bibi mmoja watoto wawili. Kabla ya kupoteza wakati, naenda moja kwa moja; maada zangu ni mbili ndogo tu hapa.

Ya kwanza ni haki ya wanawake kina mama na kina dada. Kwa sababu naona wenzangu waliokua hapa, wote karibu kumi, hawakuwakumbuka akina mama. Kama tunavyoelewa mwanamke ni kiumbe ambaye ni dhaifu sana. Na anadhulumiwa kijamii katika sehemu mbali mbali. Kwa sababu ya hiyo nimependekeza haya yafuatayo. Mwanamke atambuliwe kua ni mtu mwenye utu kamili. Ubinadamu wake na utu, uwe sawa na mwanamme. Mwanamke awe na haki ya kupigania uongozi wa viti mbali mbali. Mwanamke awe ana haki, ya kuridhi mali ya wazazi wake. Yakuridhi mali ya mme wake, na mpaka ndugu zake, ikiwa ndugu zake hawana watoto. Hakuna ruhusa ya mwanamke kuridhiwa, kama vile inavyofanyika kivingine. Bwana anafariki, anashuka mtu mwingine, ikiwa na ndugu yake anaridhi. Ikiwa unataka pale ufuate ile njia ya kisawa sawa upose pale, utake kuoa ile inaruhusiwa. Lakini sio kuridhiwa. Na hakuna ruhusa ya msichana kuozwa kwa nguvu, na wazazi wake na vile vile asiozwe akiwa mdogo. Hali hiyo bado, yale masilahi ya kimme na mke bado hajayafahamu. Swala la kunajisi yaani raping. Kama inavyofahamika, miji mingine wanachukulia raping, hata kama ni wewe na mke wako, yule mke ikiwa time ile alikua hayuko kwenye ile mood, unakua-charged. Kwa hivyo hiyo iwe sheria, hapa kwetu hakuna. Wanawake vile vile wawe wakichaguliwa, katika ngazi mbali mbali; kama lile bunge la Afrika Mashariki lililoundwa juzi, hakuna mwanamke hata mmoja wa Kislamu ambaye alitoka Kenya hii yetu. Na kuweko na sheria kali ambayo, wale ambao wanakutwa wanawanyanyasa wanawake, na kuwabagua wapewa adhabu kali ya sheria.

Sasa naenda upande wa watoto. Watoto kama vile tunavyofahamu, nimoja katika jamii yetu, ambayo tuko nayo katika mazingira. Kwa hivyo kuweko na sheria ya kulinda watoto wasiadhibiwe kupita kiasi, na wazazi, au walimu katika masukuli. Kama vile tunavyofahamu watoto huadhibiwa hata ikafika wakati mtoto mwenyewe, anatoroka bila ya kujulikaniwa yuko wapi.

Wazazi wakaingia ku-report kila mahali, na mtoto anatafutwa. Hali hiyo ni ile adhabu ya nyumbani, inayofanya mtoto akimbie. Wazazi na walezi wapewe uwezo wa kuwakemea watoto, kama njia ya kuwatisha. Wazazi na walezi wawe ni jukumu lao kuhakikisha ya kua, watoto wanasomeshwa, elimu ya duniani, na elimu ya dini. Wazazi wasiwape watoto kazi ngumu, wala kuwapeleka watoto mahali kua wajiriwe kazi. Na vile vile kampuni yeyote, isiwajiri watoto wadogo. Na wale watoto ambao wanarandaranda barabarani, iwe ni jukumu la serikali, wapewe makao, na waelimishwe, na vile vile wachungwe. Kwa hivyo Makamishena ninakomea hapo, na nashukuru kwa hiyo time ndogo mlionipa.

**Com. Pastor Ayonga**: Bwana Nasur, sikuelewa, nataka ufafanue, juu ya kuridhi. Kwamba bibi anaweza kuridhi baba yake mali ya babake, na akaridhi mali ya Bwanake. Anaridhi kule na anaridhi hapa, hiyo sasa sielewi inakuaje.

**Com. Salome**: Na mimi nina swali juu ya watoto wanaorandaranda mitaani mwetu. Umesema kua ili liwe jukumu la serikali. Sasa wale wako wangekua jukumu la serikali, lakini miaka nenda, miaka rudi; ama nini maoni yako? Tutafanya nini ili watoto waache kwenda mitaani? Ama tunasema watu waendelee kuwapeleka mitaani na serikali iendelee kuwangoja huko, na kuwapa huduma. Ni mambo gani tungeweza kufanya ili hali ya watoto kua mitaani kupunguka?

**Nasur:** Haya nikija kea swali la kwanza, swala la mke kuridhi mali ya wazazi, na mali ya mme wake. Babake yule mwanamke, alizaliwa na mzazi, sasa mzazi yule ikija ikiwa atafariki, iko share yake yeye, pamoja na ndugu zake, anaipata pale. Mwanamke yule hata kama alizaliwa, atakaa vile vile, ataolewa. Wakati akiolewa, Bwanake bahati mbaya afariki kabla ya yeye, itabidi katika zile assets, mwanamke pia anayo ile share yake ya uradhi. Tukisema ule uradhi, si kua kila kitu chote kitakwenda, la! Kuna-share kulingana na watoto wa kike, watoto wa kiume, na yule widow. Sasa natumaii hapo nimejibu.

Na tukija swali ya hao watoto ambao wanarandaranda tunasema ni jukumu la serikali wangalie makao, wawaelimishe na wachunge. Lakini kinga ambayo iko pale, inakua, ni wale watoto ambao tuko nao sisi, manyumbani, nikuhakikisha yule baba na mama, watoto wale kama vile sheria mpya iko, waende masukulini, wakulie kwenye nidhamu ilio bora. Lakini katika hapo hapo, kuna wale watoto ambao sasa, wanakua saa nyingine, wamekua thrown away, pendekezo nyingine ni kua; welfare ziwekwe katika ma-division, yakienda mpaka katika district, kuhakikisha wana-take care kwa wale watoto, lakini chini ya serikali.

**Com. Salome**: Asante sana Bwana Nasur twashukuru kwa maoni yako. Sasa nataka kumuomba Henry Onunga Owour.

**Henry Owour**: Nashukuru sana Makamishena kunipa hii fursa, pia sisi tutoe maoni yetu kidogo, kuhusu hii marekebisho ya Katiba. Kwa majina naitwaHenry Odunga Owour, mimi nimkaazi wa hapa Mikindani. Yangu ni machache tu, ningependa kutoa maoni kwa hii marekebisho, kwa mambo ya local government. Nikisema local government, sana inahusisha mambo ya councillors; ingekua ni pendekezo langu, ikifika kwa kurekebisha katiba tuwe hatuna institution ama role ya councillor. Nikisema hivi, twaweza kujiuliza sasa katika hizi local authorities, tutakua tukifanya kazi namna gani, bila councillors. Kitu cha

kwanza ningependekeza, Mayors wawe wanachaguliwa directly, na wananchi wenyewe. Kuwe kuna act, katika local government act; ambapo iwe na guidelines, ya qualification ama moral standing ya mtu yule anafaa awe kama Mayor. Na huyu mayor ndiye anaweza kupendekeza wale watu anafikiria, wanaweza kumsaidia kuendesha mambo ya council. Mainly watu professional kwa mambo haya, kama professional kwa mambo ya education, kwa mambo ya engineering, na kadhalika. Pia huyu mayor awe ni mtu yuko answerable directly kwa Parliament ama committee ya Parliament. Isiwe mambo ya Minister, ama politician kuingilia mambo kama hayo. Na huyu mayor awe chief executive officer wa hii council, aliyechaguliwa aiwakilishe. Na mtu kama town clerk huyu awe chief operating officer. Na kama tuna treasurer, yeye ndiye atakua ni mtu anayeshugulika na mambo ya finances ya hiyo council ilioko. Nafikiri ni hiyo maoni kidogo ninayo Commissioners.

**Com. Salome**: kuna mtu mwenye swali kwa mzungumzaji Owour. Mimi ninaswali moja. Umesema kua mayor achaguliwe na wananchi moja kwa moja. Na atakua akifuatiliwa na bunge ama committee ya bunge. Je? nao hao wengine ambao watamsaidia, yeye mwenyewe atawajiri kazi ama watakua wamechaguliwa, ama watakua vipi? Wafanyikazi wa mayor? Kwani hata yeye atakua hana mtu mwingine, isipokua yeye peke yake. Watakua wafanyi kazi wake, ama vipi?

**Henry:** Asante sana kwa swali hilo, maanake itanipa fursa ya kufafanua kidogo; tuseme kama huyu mayor anataka kuchaguliwa, wale office bearers wake, lazima atakua amewatabulisha mapema. Tusema ni kama election ya trade union, utasema mimi nikija nataka fulani ndiye awe ananishugulikia kwa mambo fulani.

**Com. Salome**: Asante sana Bwana Owour jiandikishe, na asante sana kwa maoni yako. Sasa nataka kumpa nafasi hii Thomas Awino.

**Thomas Awino**: Asante sana. My names are Thomas Awino Rundu. Am a resident of Mikindani. I would like to comment on the tenure of office of the President, that is section nine, I forgot to note the chapter of that particular section. It has been said by some of our politicians, that the current President should go back to the office after the end of this term.

**Com. Salome**: Leta chombo cha kupazia sauti karibu na wewe, ndio tukusikie.

**Thomas:** I suspect some individual citizens would like to revert to the old clause, allowing the president to continue holding office until he opts out, or dies in office. The current accepted Constitution, that gives one only two terms should remain in force; as it allows the electorate, to elect competitively, and after a short term of ten years, every right thinking son or daughter of Africa; admires former retired presidents who are leaving in peace in their respective countries. The best example is the ex-president who fought for so long for South African independence only to stay in the office for one term. Other examples are if am not wrong, Leopold Senghor of Senegal, and Julius Nyerere of Tanzania, and our President, who has severally indicated his intention to retire at the end of his two terms, when after introduction of the section replacing our old law, on the presidential election. These are great men and women of Africa, who would like to change the lives of Africans from the colonial boudage,

to freedom for all.

Now on Presidential elections: with the advent of multi-partyism we are currently witnessing, mergers aimed at winnig the presidential election, this is fine: but the presidential candidate should have a running mate, to give the junior partner security of holding responsible positions, otherwise the merger may not work at the end of the day. Section 14, protection of the president while in office. To err is human, the President is a human being, can make human errors or even use the current executive powers to intimidate any individual. It is my considered opinion, that the power of the President should be reduced immensely to make the person of the President liable to prosection in a court of law.

The introduction of two term reigns of power, is timely to our developing country. 10 years is such a short period, that a person ascending to the post of president shall not overstep his duties. The current Constitution protects the President from civil and/or criminal proceedings while in office. This protection should cease, since everyone is exposed to their individual rights. A person holding or exercising the duties of the President should face the law in the event of him breaking the same. He is number one protector of the law and signatory to it; and should be the last to break it. Impeaching a President implies nobody is above the law, and therefore any clause allowing the president to be above the law, should be removed from our Constitution, making him the executor of all functions of the office of the President worried of being above the law. I would like now touch on chapter five of sub-section 78.

**Com. Salome**: I would like to request you not to read word for word, that becomes hard for us to follow. Are you going to give us that memorandum?

**Thomas:** Definitely yes.

**Com. Salome**: So we are going to read it, just highlight the issues. Lakini usitusomee neno kwa neno. Hiyo itakua jukumu yetu sisi wanatume kuisoma. Kwa hivyo pia itatupa nafasi ya kwenda upesi upesi, ili tumpe mtu mwingine nafasi.

**Thomas:** Thank you so much. On chapter five, section 78, these are the fundamental rights. This one touches on the right of an individual to enjoy the freedom of religion, or belief. When you come to this particular section, you find that Kenya started working several years back, on a five day week basis. Today, as we are talking here, some employers, are still stressing on work on Saturday, or Sunday, whatever the case. Now the Sabbath day, according to the bible, starts at sunset on Fridays and ends on Saturday at sunset. If that freedom is really freedom to all, then those who observe the Sabbath, are not given that enjoyment or that freedom, by some employers, or some institutions of learning. It should be very clear that the section gives enjoyment to the members of society, and they should be exposed to it. I think that is subsection 78, that is what I wanted to discuss on Sabbath.

**Com. Salome**: Asante sana, kuna swali kwa Bwana Owino. Kuna swali kutoka sakafuni kwa Bwana Owino. Tafadhali ukiwa na swali, inua mkono halafu tutakuona. Asante sana Bwana Awino. Mimi nina swali moja ndogo. Tuna dini tofauti, unasema Sabbato ya jumamosi na pia siku ya ijumaa iwe siku takatifu. Na pia siku ya Jumapili, kwa hivyo tupunguze siku za kufanya kazi ziwe nne. Ili waumini wa dini hizi kila mtu apate siku moja?

**Thomas:** I think what we are discussing is, we are talking of a five day working week; which starts on Monday and ends on Friday. That is what I said. Every other person has been free, and even Friday they go to the Mosque; they have no problem about this. Saturday has not been left out as stated in the Constitution.

**Com. Salome**: Point taken. Thank you very much. Sasa nataka kumpa nafasi hii, mama Salama Ndadi.

**Salama Hussein**: Kwa jina naitwa Salama Ndadi Hussein, mkaaji wa Mikindani. Maoni yangu kama mkaaji wa Mikindani, na mwanamke wa Pwani, Coast Province; kwanza ningepende kuzngumzia juu ya Mahakama ya Kadhi. Twaona katika mahakama, Kadhi hana uwezo mkubwa kama mahakama zile zingine. Yeye kiwango chake ni kusimamia kitu kama divorce ndoa, na uridhi. Kwa hivyo katika Katiba ningependelea awe akihukumu Waislamu, wawe wakihukumiwa na Kadhi kama vile Koti kuu zilivyo.

Halafu katika uchaguzi wa Kadhi, awe akichaguliwa na Waislamu waumini walio soma; na amechaguliwa awe na elimu zote mbili, za kiwango cha juu. Halafu katika hicho kiti cha Kadhi, kuwe na mwanamke, ambaye atakua na ofisi yake kando na mwanamke huyo awe amesoma na elimu zote mbili za kiwango cha juu. Kuna baadhi za wanawake wanaenda na malalamiko kwa Kadhi, lakini kuna maneno mengine ya ndani, hawawezi kumweleza yule Kadhi. Ama unaweza ukamwelezea, lakini awe anapendelea upande mmoja, ule wa mwenzake. Kwa hivyo, tukipata nafasi, tuwe na mwanamke pale katika ofisi, anayeweza kisikiliza yale maneno; na ukamwelezea kila kitu bila kuogopa na akayapeleka mbele. Kwa sababu upande huo, wanawake wanadhulumiwa.

Tukija katika kesi za upande wa uridhi. Katika uridhi, kama mfano hiyo ya wanawake, kuna sheria zilizoongezwa na Kadhi; utapata kuna wao baadhi yetu Wakristo, ama watu wa Bara hivi, hua wanasema ni vigumu kupata uridhi, kwa upande wa wanawake. Hawapewi uridhi, wanabaguliwa wakibiwa kua wao wataolewa, basi si rahisi kupata uridhi. Aama umeolewa na bwanako, uridhi hupati, pengine umenunua shamba lako, Bwana akwambie, lile shamba haliwezi kua ni lako, linakua ni la Bwana. Ukiondoka, unaondoka, hupati chochote. Kwa hivyo kama umeolewa, kuwe na haki mwanamke kupata uridhi, kutoka kwa Bwanako ama kutoka kwa familia yako.

Na katika divorce. Umeolewa na Bwana, hana chochote; mkachuma mkapata mali vizuri pamoja. After mali imekua nyingi, Bwana yule anapata ndogo ndogo mwingine; anakusahau kabisa, waondoka hupati kitu. Kwa hivyo ningependelea katika Katiba, mali hii ingawanywe nusu kwa nusu. Maanake mlichuma mali pamoja, ulimsaidia kumpikia, na kumfulia. Kwa hivyo ile

mali igawanye nusu, kwa nusu kila mtu apate; sio mtu akiondoka unaondoka, mikono mitupu.

Katika upande wa kazi, sexual harassment. Unaweza kwenda mwanamke umeenda katika makampuni makubwa makubwa kutafuta kazi. Kwa kua wewe ni mwanamke, sio Muislamu wala ni wanawake wote, pengine boss akwambie: mpaka utembee na mimi, ndio ni kwandike kazi. Kitendo hicho mimi mwenyewe kishanipata, ndio maana nikasema kama mwanamke.

Nikuzungumzia katika upande wa bunge. Tukiangalia wanawake Kenya, tuko 52%, wanaume ni 48%, kwa nini sisi tusiwe wengi pale bunge Yote hayo ni wivu. Ukisikia mwanamke ataka kusimama, hakuna atakaye msaidia. Tutasema ha! asimame afanye nini? Kwa hivyo sisi wenyewe wanawake, tuungane tushikane, tupeleke wanawake wengi bungeni. Na sisi ndio tunawapigia wanaume kura mpaka wakapita. Hasa ningependelea katika nomination, viti vya nomination, viwe ni vya wanawake; haswa wale wanawake ambao walijitolea kusimama na wakaanguka. Nakama hakuna aliyejitolea, katika kila district, kuwe na wanawake wawili wanarepresent. Na katika hao wanawake, kusikosekane mlemavu. Maanake atazitetea haki za walemavu katika bunge.

Halafu katika upande wa uchaguzi. Ningependelea wakati watu wakipiga kura, zile ballot boxes ziwe transparent; ndio kila mtu aone vile hesabu zinavyoingia pale. Na wakati wa kuhesabiwa, sizipelekwe masafa marefu kwenda kuhesabiwa; maanake utasikia baadhi ya ballot Fulani, zimepotea hazijulikani. Kwa hivyo kama hapa Changamwe, zikihesabiwa, pengine zihesabiwa pale kwa police station zi siwe zimeenda mbali, na hizo ballot boxes ni transparent. Kila mtu atahakikisha ameona ni kitu gani kimeingia katika ballot box fulani.

Katika watoto wa mitaani. Katika kupunguza hao watoto wa mitaani, patakapo patikana mtoto chokora anazunguka, mtoto yule achukuliwe, aulize kama ana wazazi wake. Maanake kuna baadhi ya sisi mama, twawatuma watoto wetu kwenda kuomba omba nje: na ilihali si maskini, ni mtu anaweza kutafuta kazi na akapata. Wala si kiwete wala si chochote. Ni ule tu uvivu, na ile kutaka kupata cha bwerere. Na kama waweza patikana watoto wa mitaani, hawana wazazi ama nini serikali iwaangalie watoto hao kea upande wa elimu, mavazi na kadhalika.

Upande wa ardhi na mali. Hii ndio tatizo kubwa mwanzo hapa kwetu Pwani. Utapata mtu, for example hapa Mikindani, haswa upande wa kwashee, ambayo ni ardhi mababu zao, walizaliwa pale; lakini kwa sasa twaona watu wanyanyaswa, mali zinachukuliwa. Mwabiwa zile ploti mlipie na ilihali ni zenu title deed hampatiwi, au utapata mtu, kwa kua yeye ana mbavu kubwa, ana plot nyingi; kwa kua mwenyewe hajiwezi, wanamnyanyasa wanaichukua ile plot, inakua ni yake. Kwa kua mwenyewe hana mbavu za kwenda kupigana kule mbele kuzungumza: sasa hiyo plot anaichukua ni yake. Sasa ningependelea, kila mwananchi, awe anapewa title deed yake, kujua ile ardhi ni yake. Na ardhi ikiwa ni yake juu peke yake; kuna pahali kama Malindi, unasikia kuna chumvi, mtu ni haki yake, anaambiwa aondoke, wanataka kuchimba chumvi. Ardhi yake iwe juu, chini si yake. Ama hapa Mikindani kuje kupatikane dhahabu au vitu kama hivyo utaambiwa ardhi ni zenu juu, chini yachukuliwa na serikali. Kwa hivyo ningependelea Katiba, ardhi ikiwa ni ya mtu, iwe ni juu na chini: isiwe ni juu peke yake, pia

kilicho chini iwe ni mali yake. Sio haki mtu kuchukuliwa mali yake hivi akiona, na ile mali ni yake, sote tunahaki kupata mali.

Upande mwingine ni katika upande wa Eda; nazungumzia kama mwanamke wa Kislamu. Tuko na Makadhi ambao ni Waislamu wenzetu. Kwa nini mtu akiwa katika Eda hapewi leave? Unapewa siku kadhaa uketi nyumbani, halafu unarudi kazini ukiwa umejifunika hivi waenda kufanya kazi. Na ilihali mtu akiwa amefungua anapewa maternity leave. Na ambapo ile eda mtu hakupendelea, ni kitu kimetokea naturaly imekuja tu, mtu hakutaka. Kwa hivyo ningependelea mtu anapewa eda leave, na analipwa kama vile anavyolipwa katika maternity leave. Na anapotaka kuomba leave tena, ya kawaida apatiwe. Na pia katika maternity leave, mtu apewe maternity leave yaka na alipwe sio kama katika kampuni zingine, ushaachukua maternity leave, kazi umekosa. Kwa hivyo mtu akichukua maternity leave, kazi inaendelea, na anapotaka tena kudai mambo za leave, apatiwe.

Katika kunajisiwa wanawake. Kuna kesi za watu wananajisiwa, pengine mzazi mwenyewe amenajisiwa; lakini anaogopa kwenda kusema kule mbele: kwa sababu ya nini? Ukienda police kusema, waona haya, yaani waona ni kitendo cha aibu. Kwa hivyo pale police, kuwekwe mwanamke, kuwe na officer mwanamke, ambaye atazungumza na yule mwanamke, akienda pale na problem zake hataogopa kumzungumzia. Na mtu anapopatikana ananajisi mwanamke, ahukumiwe kifungo kikali. Ama Bwana anapompiga bibi yake, msiogope: wengine wanaogopa kua Bwanangu amenipiga, mtu anaku-harrass nyumbani, anakufanya vyovyote; unaogopa kwenda kupeleka yale mashtaka police kwa kua police atakwambia: “wewe ulikataa kumfungulia bwanako mlango, ama humfanyii Bwanako hivi”. Kwa hivyo kuwe na mwanamke, ambaye atatusikiliza sisi wanawake pale, kila tutakacho sema, awe anatusikiliza, na kukipeleka mbele.

Upande mwingine ni mambo ya usawa. Kwa nini tukiwa makazini, utapata mtu mwanamme, analipwa zaidi, kuliko mwanamke? Kwa kua yeye ni mwanamke hafai kupewa mshahara sawa na yule mwanamme. Kwa hivyo ningependelea katika Katiba, sote tuwe sawa, kama vile Katiba inavyotaka wanawake na wanaume wawe sawa. Katika kuandika Katiba, na pia katika kupewa kazi, na hata katika kupewa post Fulani: tuchukuliwe sawa na wanaume.

Halafu katika muudo wa serikali tunayoitaka. Kivyangu mimi ninavyosema, serikali iwe ya Majimbo. Nikisema Majimbo, simaanishi Mbara aende kwao. Kenya ni yetu, na sisi ni wana Kenya. Unaweza keti mahali popote. Nikisema Majimbo namaanisha tuna viwanda vikubwa hapa Pwani. Tukiangalia, oil refinery iko kwetu, hiyo bandari iko hapa kwetu. Kwa nini zile tax ambazo zinatolewa hazitusaidie sisi Wanapwani? Zinapelekwa juu, hatuijui zinawasaidia nani. Zinawasaidia wao wenyewe hali hapa kwetu tunaumia. Makazi hatuandikwi sisi, na kunao waliosoma sio ati watu wa Pwani hawajasoma, kunao waliosoma lakini nafasi hawapati; zote zinapatikana kwa juu. Kwa hivyo ningependelea hizo tax, kuundwe tume fulani yakuzisimamia zile pesa za kuendeleza hapa Pwani. Kwa hayo machache asanteni; kuna mengine pia sisemi, nitapeana kwenye memorandum.

**Com. Salome**: Subiri maswali. Wa kwanza tafadhali. Njooni wote hapa mbele, ndio mtumie microphone yangu.

**Joel Musango**: Asante sana. Mimi naitwa Joel Musango, na ningependa kuuliza mambo ya uridhi. Umesema ya kwamba wewe ukiwa kama mtoto wa boma, ikiwa wewe umezaliwa hapa na unafaa upate uridhi kutoka kwa babako. Na kule utakapoolewe pia upate uridhi. Sasa mimi ningependa kuuliza, ikiwa utapata uridhi kwa babako hapa; uende uolewe kule kwa Masai, Bwana afariki upate uridhi. Uende kule Turkana uolewe, Bwana afe upate uridhi hapo. Uone hapo hapafai; kesho utaruka uende Ethiopia, uolewa kule bahati mzuri, pengine kule ndio umezaa. Umekufa huko huko; watoto wako huko ule uridhi wako uliouwacha Umasaini hawajui. Je hayo yote yatakusaidia kivipi?

**Com. Salome**: Asante sana ningepende kutilia mkazo kua maswali yawe mafupi na very focused. Sitaki habari ya kuanzisha majadiliano kati ya mzungumzaji na mwenye kuuliza maswali. Kulikua na mikono mingine miwili; Andika hayo maswali, utayajibu yote kwa pamoja.

**Question:** Asante sana, niko na maswali kama matano hivi. La kwanza yeye amesema wanawake wanabaguliwa katika bunge; na wanawake wako 52% na wanaume 48%. Wakati walikua wanachagua wanawake kwenda kwa East Africa Assembly, mbunge wa Msambweni ni mama; lakini alipiga kura upande wa ku-support mwanaume aende, badala ya mwanamke kwa nafasi ya tatu. Sasa atasema je kwamba, wanaume wanabagua wanawake, na wanawake wenyewe wana jibagua wenyewe?

**Com. Salome**: Karibu, ulikua pia wewe una swali? Nilikua nimeona mikono mitatu, lakini sasa imekua mingi, lakini wewe mzee uliza swali lako.

**Question:** Swali tu kidogo tafadhali. Jana ilikua ni mtu atoe maoni yake, sasa leo imekua ni kujibizana, hiyo kweli itakua ni maoni?

**Question:** Kulingana na bibilia, Mungu hakuumba mwanamke kutoka kwa kichwa awe kiongozi, au atoke kwa mguu ili anyanyaswe: alimtoa ubaruni. Sasa wanawake wanafaa waunge wanaume mkono kwa yale wanayoyafanya. Hata hao wanawake ambao wako juu, utapata wanatoa mawazo kutoka kwa wanaume. Mwanamke anafaa aunge mwanaume mkono kwa kile anachokifanya. Utapata hao wanawake ambao ni viongozi; nyumbani kwao kuna wasichana, au wa mama wamewekwa hapo nyumbani,, wanafanya kazi. Hao wamama sio?

**Com. Salome**: Tafadhali mtu akishazungumza, kuna nafasi ya kumuuliza swali la ufafanuzi, la kukuwezesha kuelewa vile alivyosema. Ikiwa wewe una maoni tofauti na yake utamgonjea yeye amalize yake, wewe umeshajiandikisha, nitakapo kupa nafasi utaeleza maoni yako. Lakini hauwezi kuja hapa kuanza mjadala kati yako na. Tunaelewana hapo? Kwa hivyo ukiwa na swali, ni swali tu la kukuwezesha kuelewa, vile huyu alivyosema. Lakini huwezi kuja. Utatueleza maoni yako wakati utakapo pata nafasi yako ya kuongea. Asante. Kwa hivyo jibu maswali unayotaka kujibu. Usiyotaka kujibu, usijibu: nimekusimamia kama mwenyekiti.

**Salama:** Asante mwenyekiti. Nitamjibu kwanza huyu wa uridhi. Nadhani hakunielewa vizuri, Mimi nimezungumzia kuhusu uridhi. Watu wa Bara, ambao hivi ni maoni ambayo nishapata kwa watu tunayozungumza nao tulipofanya hizi mikutano. Wakasema kua, watu kwao, hawaruhusiwi mtu anaponunua shamba, hua si lake mwanamke shamba ni la mwanamme. Wanapoachana na Bwana, lile shamba analiacha pale pale, ambapo ile mali ni ya Bwana. Kwa nini mwanamke asiwe na haki ya kua na lile shamba, na ilihali anauwezo? Na katika uridhi nimesema mwanamke aambiwa hataki uridhi wa wazazi wake, wanapewa wanaume, kwa kua yeye ataolewa. Kwani yeye si mtoto? Ni mtoto amemzaa, kwa hivyo anahaki ya kupata uridhi. Sisi kislamu yetu imewekwa una thuluthi yako utapata. Na kwa hivyo pia wengine, wana haki wote wamezaliwa, pia wapate uridhi. Yeye kama hakuolewa atapata nini. Kuolewa ni majaliwa, sio kitu ya lazima kuolewa.

Halafu umesema mtu anatoka, anaacha hapo, anaenda mahali kwengine anaolewa, anaachwa anapata uridhi: hiyo ni majaliwa ya mtu yake mwenyewe. Lakini ile haki ya uridhi ni apate.

Nanikija kusema upande wa wanawake bungeni, sikusema kua wananwake wabaguliwa, nimesema sisi wenyewe wanawake, tuna wivu; na ambapo sisi tuko wengi twaweza kusimamishana, tukawa wengi katika bunge. Lakini sisi ni wivu ndio tumeweka mbele. Kwa hivyo nilikua nataka wanawake waache wivu; mwanamke mwenzako akitaka kusimama ,wamsimamisha kisawa, apite awe kule mbele. Nominated seats ziwe ni za wanawake bungeni. Haswa na wakichanganyikana na wanawake viwete.

**Com. Salome**: Asante sana bi Salama, wakati huu wakutengeneza Katiba. Ni wakati wa sisi wana Kenya kuzungumza pamoja. Nimesikia kutoka jana na juzi wakati nimekua nikisikiza matakwa ya wana Pwani, wakisema sisi wana Pwani tumebaguliwa hatuko hapa, hatuko pale. Basi ikiwa wana Pwani wanajisikia wamebaguliwa, lazima pia wawakubalie wanawake waseme yao, wakisikia wamebaguliwa. Uzuri wa Katiba ni kua ikipitia kwangu yafanya mazuri, ikipitia kwako inafanya mazuri hayo hayo. Kwa hivyo wakati mnaposema mnabaguliwa kwa ili na lile, hatuna DC Muislamu, hatuna nini, halafu mwanamke akisimama kusema hatuko bungeni, mnamkemea, basi hiyo sio Katiba. Katiba is about justice. Usawa, ukweli, haki; na haki hiyo ni kwa mzuri na pia kwa mbaya, ni haki kama ya mvua. Kwa hivyo mtu akianza kutoa maoni yake, aheshimiwe kwani hivyo ndivyo anavyoona; na ndio tumesikia kila mtu atoe maoni yake mwenyewe. Kwa hivyo mwanamke akisikia ana tashwishi ya kutoa, mpeni nafasi atoe. Wewe nawe ukipata nafasi yako, yapinge aliyosema; lakini apewe nafasi yake atoe, na tusianze mjadala wa kupinga mtu, akiwa bado yuko sakafuni. Tunaelewana hapo? Heshima zetu lazima tusitulize kwa kila mtu. Wanaozungumza wakubaliwe. Akimaliza na sisi tukija, basi nasi tupatiwe hizo heshima zile zile, za kusikizwa na maoni yetu,na sasa ningetaka Silas Angore.

**Silas Angore**: Kwa jina naitwa Silas Angore, mimi nina mambo mawili matatu, ambayo ningetaka.

**Com. Salome**: Ningeomba zile kelele za kule nyuma zifupishwe tafadhali. Mkizungumza kule nyuma tunanasa hayo maneno katika kanda wetu wa tape. Tafadhali naomba, sitaki kusema ni akina mama, lakini ukweli wa mambo, ni nyinyi wenye

kuzungumza. Tafadhali tusizungumze wakati wakutoa maoni, ndio maneno haya yasitatize ukanda wetu. Subiri nafasi yako ifike. Endelea Bwana Angore.

**Silas**: La kwanza ni juu ya Katiba, kwanza Katiba yenyewe kama leo Bi. mwenyekiti tulipoanza; ulisema tunaweza kutumia Kiswaili, Kizungu, lakini tukiangalia Katiba yetu imeandikwa kwa kizungu, ambacho hata wale waliosoma, pia kinawatatiza. Ukiangalia sana, kuna sehemu hata wengine wamesema, hata lawyers wenyewe, inakua vigumu kuielewa. Kama wale wanasheria ni vigumu kuielewa, sisi ambao hatukusoma hivyo, tutaielewa vipi ile Katiba, ili tuweze kuijua udani wake, na tofasiri yake? Kwa hivyo ningependekeza Katiba, na si Katiba peke yake, na sheria zetu za Kenya, ziandikwe hata kwa Kiswaili; ili tuweze kuzielewa zaidi. It is said kua ignorance of the law, is no defence. Kwa hivyo ikiwa hujui ile sheria; huwezi kujitetea kotini useme mimi nilikua sijui: lakini ungejulia wapi? Serikali inachukulia kila mmoja wetu anajua sheria, lakini ni wachache sana wanaojua zile sheria zetu. Kwa hivyo ni vizuri, hata sheria, Katiba iandikwe kwa Kiswaili, na sheria zote ziandikwe pia kwa Kiswaili. Sikusema Kiswaili peke yake nimesema pia kwa Kiswaili. Hakuna neno moja ambalo liko katika Katiba ambalo haliwezi kutotafasirika kwa Kiswaili, kama maneno ya juzi tu television, inaitwa runinga, hayo mambo ya 63 yalitungwa huko yanaweza kukosa neon la Kiswaili. Kweli?

Lingine ni kwamba, baada ya kua imeandikwa hivyo, Kiswaili, iwe rahisi pia kufikika. Iwe rahisi, kila mwananchi, aweze kuifikia. Kuwe distinction ya hizi Katiba iwe mtu anaweza kuinunua popote. Sio kua sasa mpaka niende Nairobi kwa Government Printers, ndio ninunue Katiba, ama hata ukifika huko unaambiwa zimeisha. Inatakikana hata kwa kila bookshop, nikiingia dukani, niweze kupata, na pia sheria zetu zote. Kwa mfano kama criminal law ni gumu, lazima tuijue, vitu vingine tunavifanya bila kujua, lakini sheria ile kama tungekua tunaweza kununua hizi sheria zote, act zote, ingekua rahisi sana. Kwa mfano, wewe mwenyewe mwenyekiti unakuta watu wengine wanakuja hapa, wanazugumzia kitu ambacho kiko katika sheria. Kiko vile vile kabisa wanavyozungumza katika sheria. Kiko vile vile kabisa anavyozungumza kabisa katika sheria, lakini hajaiona, hajui hata ataipata wapi; sasa kama ingekua inaweza kupatikana ki rahisi ingekua vizuri zaidi, ingetusaidia.

Jambo lingine ni zile nguvu za president. Nguvu za president ni nzuri na wakati mwingine zinatumika vibaya. Nikisema hivyo namaanisha kua, nchi yetu unaona imekua kidogo stable kwa muda mrefu, kwa sababu ya zile powers za president. Yeye ndiye ana-appoint Ambassadors, Permanent Secretaries, Ministers, wale wanaongoza katika jeshi, yeye ndiye ana-appoint yeye ndiye mkuu wa majeshi. Inakua ni rahisi sasa, wale watu kumheshimu yule president. Hiyo inasaidia, lakini wakati mwingine pia, inakua ngumu wakati mtu anachaguliwa bunge, anaangukua: president anatumia zile powers ku-nominate yule yule ambaye amekataliwa na wananchi, katika Changamwe kwa mfano, halafu anakua nominated kwenda Parliament,anaenda anapewa ministry. Je? wale watu waliomkataa, President huyu amewaweka wapi? Amewachukua kama kina nani? Kwa hivyo zile nguvu za president, sisemi ziondolewe, lakini nasema, kuwe na kamati ya ku-nominate, kama ni Changamwe, au tuseme kama ni Coast Province watu sita wapendekezwe; halafu atakayechaguliwa awe katika wale watu ambao wamependekezwa. Sio Rais mwenyewe achague tu vile anavyotaka. Kwa hivyo zile powers, ziwe kidogo zimepunguzwa, kiasi ambacho kwamba itaweza kutusaidia na sisi, lakini sio kutumia mambo ya urafiki.

Jambo la tatu, wenzangu wamezungumzia mambo ya Majimbo. Majimbo ni mambo mazuri sana, ni serikali nzuri sana; hata sisi wenyewe tunalilia misaada wakati mwingi. Tunaomba misaada labda Amerika. Sasa sisi wenyewe tunakataa Majimbo, na tunaomba misaada katika serikali ambayo ni ya Majimbo, Ujerumani ni Majimbo, hata England, ni Majimbo kila Jimbo linajaribu kabisa kujitetea, kufanya bidii, sio kua sisi tuwe tunategemea kahawa au chai. Sisi pia tuna chumvi hapa, kwa hivyo nguvu ile ile ambayo tunapata kutoka kwa chai na kahawa, na sisi wale nao wanahitaji chumvi; kwa hivyo tunahitajiana sote. Kwa hivyo Majimbo ni serikali nzuri ambayo inaweza kutusaidia kuendeleza provinces zetu. Sisi tunashindwa na kuendesha Majimbo manane, na wenzetu America wana Majimbo 52.

La mwisho ni mambo ya street children. Mambo ya street children ni jambo ngumu sana, kama mwenzangu alivyosema ni kwamba, watoto wengi hua wanatumwa kutoka nyumbani. Kwa hivyo ikiwa tunataka kumaliza mambo ya street children, lazima tuangalie kule nyumbani. Lazima tutumie machifu, tutumie wale wafanyi kazi, ambao wanaangalia mambo ya watoto kule mtaani. Maanake sisi kama Mikindani hapa, tunajua mtoto wa Fulani, nyumba Fulani, ni kimwona town nitajua yule ni mtoto wa fulani. Ikiwa tutaanzia huku mashinani, tutaweza kumaliza mambo ya street children. Lakini kama itakua vigumu, basi itakua vigumu hivyo hivyo, hatuwezi kuanzia kule juu, ndio tuje chini. Mfano kama Cuba, Cuba hauwezi kupata street child. Kwa nini? Wale watu wanachukuliwa, kama ni kusaidiwa na serikali, wanachukuliwa wanapelekwa katika jeshi, wanasomeshwa na wanalishwa huko huko. Wakimaliza shule wanakua wanajeshi. ndio unasikia Cuba, askari wake ni wa kali kwa sababu hawana kitu kingine wameacha nyuma. Kwa hivyo hata hapa, kama tunaweza kuchukua mfano kama huo, wakuangalia mambo ya street children; utaona watoto wale watatolewa town, maanake ni watoto wa watu ambao wako hapa hapa. Kwa hivyo kwa hayo machache, nafikiri nimesema sana, hata dakika zangu karibu kuzimaliza, asanteni sana.

**Com. Salome**: Asante sana Mr. Angore. Swali? Hamna.

**Question**: Nataka kumuuliza juu ya Majimbo. Amesema Amerika Majimbo, pia Kenya tuwe na Majimbo. Lakini Kenya huwezi kuilinganisha na Amerika kwa ajili ya maendeleo yao. Isitoshe mtu atakubaliwa kuishi katika Jimbo lolote analotaka?

**Com. Salome**: Nafikiri swali ni hilo moja tu kama mtu atakaa kwa Jimbo lolote analotaka.

**Silas**: Asante sana, nafikiri hata nilikua nimesahau kulifafanua hapo mwanzo. Ni kwamba katika serikali ya Majimbo mtu anapewa uhuru, kama vile Katiba inavyosema, kua anaweza kuishi katika Jimbo lolote. Ni kwamba tu ukijiandikisha katika Jimbo hili hauwezi kujiandikisha katika Jimbo lingine. Ujue maslahi yote yatakua ni ya hapa hapa Pwani. Kwa hivyo, kile kitakachopata mtu wa hapa Pwani; kitakupata hata wewe ambaye wewe ni wa Bara, lakini umekuja hapa Pwani, umejiandikisha kama mtu wa Pwani. Kwa hivyo wewe ni wa Pwani. Kwa mfano hii Coast Province sasa ikididimia baharini, ni watu wangapi wa Bara watadidimia? Sini wengi, na mtaabiwa ni watu wa Pwani wamedidimia. Kwa hivyo wewe pia ni mmoja. Nikiongezea ni kwamba, katika kugawanya kazi, au kugawanya maslahi, au economy ya nchi, utaangalia kama sehemu

sitini kwa mia, itabaki hapa hapa. Ile arubaini iliobakia, labda kuna sehemu kidogo ambayo itachangia katika serikali kuu, kuna sehemu kidogo ambayo itachangia katika watu ambao wanatoka nje: labda kwa kazi fulani ambazo kwamba hatuzijui, au wale ambao wanakuja kutufundisha kazi. Wale ndio tunawapa ile sehemu nyingine iliobakia. Lakini sehemu kubwa zaidi, kama sitini kwa mia, ama sabini kwa mia, ibakie hapa hapa Pwani. Kwa hivyo wewe, kama mtoto wako umejiandikisha hapa, bila shaka akienda kuomba kazi, kitambulisho chake kinaonyesha huyu ni wa Pwani; kwa hivyo atapewa kazi, kwa kua yeye ni Mpwani. Lakini ukija naye ukisema umeandika Central Province, sasa tukufanye nini? Ijapokua una ruhusa ya kuishi mahali popote, lakini lakini lazima ujiandikishe pale unapoishi. Sio kua unaweza kuishi tu na hujiandikishi.

**Com. Salome**: Asante sana Mr. Angore, sasa nampa nafasi Bwana Pilip Oluoch.

**Philip Aluoch**: Kwa jina naitwa Pilip Aluoch. Mimi maoni yangu kuhusu Katiba ya Kenya.

**Com. Pastor Ayonga**: Leta kinywa chako karibu na chombo cha kupazia sauti ili tukusikie.

**Philip Aluoch**: Katiba ya kwanza ya Kenya kutokea 1963, ilikua kuna mchezo ndani sana, ambapo, wale wakubwa walichezea Katiba sana. Hiyo Katiba ilikua imezungumzia mambo mengi. Sisi wa Kenya, tulisema ya kwamba tabadilisha Katiba. Kuna sheria zingine ambazo ziko kwa ile Katiba tutatoa, na zingine tuongeze nguvu. Kwanza wadhifa wa Rais. Tulisema ya kwamba sisi wa Kenya tunataka nguvu za Rais zipunguzwe.

Ya pili, tulisema ya kwamba sisi kama wa Kenya kwamba wadhifa wa Chief upunguzwe. Tulisema ya kwamba polisi wasikue na uwezo mkubwa sana, pia huo upunguzwe. Na ya nne sisi tunataka wanawake wavae mavazi yenye heshima kwa sababu kuna mavazi ambayo yanachangia ukimwi zaidi. Mama aki vaa suruali inayomkaza, nafikiri wewe kama mwanamme utafikiria mambo mengi. Katiba iseme Wakenya wavae mavazi yanayofaa. Mavazi ya heshima, kama ya wenzetu hapa Mombasa, mkoa wa Pwani. Usione bui bui ni mbaya, kwa sababu wa navaa kulingana na sheria, na utaratibu wa dini. Kama tungekua tunavaa mavanzi kama hayo, na kwambia Kenya ingekua mzuri. Haya maneno ya ukimwi ingekua hakuna. Na mimi natoa pendekezo hilo kwa Tume ya Katiba, tafadhali tuangalie hilo neno.

Ya tano: Mwenzetu mwingine alisema mambo ya Jimbo. Sijui mambo ya Majimbo yataleta manufaa gani Kenya: tuangalie mambo ya serikali ya mseto. Majimbo, ni wewe unapotaka kuja mkoa wa Pwani, utakua una-passport. Kama wewe unaenda Mkoa wa Nyanza, utakua na passport ya kukaa huko; kwa sababu utakua unapewa muda. Tuangalie serikali ya mseto au serikali ya Majimbo, ni gani itakayofaa. Hayo ndio niliyokua nayo.

**Com. Salome**. Asante sana Bwana Aluoch kuna swali kwa Oluoch?

**Com. Pastor Ayonga**: Bwana Oluoch, umeongea kuhusu mavazi ya akina na habari ya ukimwi. Mimi nafikiri ukimwi

unaenezwa na watu wote.  Kuna wanaume wanaoeneza ukimwi, kuna mama wanaoeneza ukimwi.  Mbona iwe tu mama wanaovalia vibaya?  Ungesema watu wote wavae mavazi mazuri.  Na mienendo pia iwe mizuri.

**Com. Salome**.  Bwana Oluoch, na mimi nina swali moja kwako pia, ningeuliza juu ya mavazi ya kina mama.  Lakini mwezangu ameuliza.  Lakini habari ya ukimwi ni ya wanaume na wanawake.  Swali lingine ningetaka kuuliza ni, maoni yako juu ya serikali ni gani?  Unatueleza tufikirie mseto, tufikirie Majimbo; watu wametwambia kinaganaga wanataka Majimbo wewe mwenyewe unataka mfumo gani?

**Philip Oluoch:**  Asante sana mimi maoni yangu nilikua sitaki serikali ya mseto.  Ambao itahusisha kabila yote ya nchi ya Kenya wakawa pamoja kwa bunge moja.

**Com. Pastor Ayonga**:  Na pia nilikusikia vizuri ulivyosema nguvu za polisi zipunguzwe. Hukutuwambia ni nguvu zipi za polisi, ambazo ungependa zipunguzwe.  Crime zimezidi, nyingi, mauaji, wizi, na nini na nini, na wewe unasema tupunguze nguvu zao. Sasa mambo yatakua namna gani? Ungeweza kutuambia ni sehemu zipi ambazo ungependa nguvu zao zipunguzwe.  Na pengine utuambie sehemu zingine ambazo ungependa nguvu zao ziongezwe.

**Philip:**  Kulingana na vile umezungumza nitakujibu kwa sababu tuko kwa maoni.  Polisi wa Kenya wananguvu zaidi ya kupata habari, ya kwenda kushika mtu ovyo.  Tunataka anapoenda kushika mtu akue na search warrant, tujue ya kwamba mambo itaendelea namna gani.  Tukipata kama anaweza kua na search warrant itakua ni vizuri.  Kwa sababu kwingine, wanajidai mapolisi, na si mapolisi.  Wanakuja kwetu kuwashika watu, na waenda kupigwa kule, halafu unyang'anywe pesa, halafu urudi; wanasema ni polisi ya Kenya.  Sasa tulikua twataka, maoni yangu, Kenya polisi ikuwe na search warrant, ikikuja idhibitishwe ni polisi.  Hii ndio maanake nilikua nasema hivi.  Ya pili nilikua nimeulizwa swali lingine kuhusu serikali ya mseto, na serikali ya Majimbo mimi nataka serikali ya mseto, kwa sababu itahusisha Wakenya wote, watakua katika bunge moja.  Wala haitachaguliwa kutoka wapi, wala wapi itakua serikali ya watu wote.  Kuna wadhifa nyingine kama ya urais ilikua ipunguzwe kidogo, hapa pia tumechangia kidogo, kwa sababu nataka ipunguzwe.  Isikue tumepata kama Rais amefanya jambo lingine, ama amekosea Wakenya tumpeleke kotini.

Na ya nne ambapo naweza kusema ni ya mwisho kabisa,  Nilikua nataka Wakenya wakue na mavazi rasmi huyu waume na wanawake.  Maanake watu wengine walizaliwa kivingine, waonapo nguo imebana mwili; na wajua mwanamme ni mtu hivi hivi; mpaka atamtamani.  Ndio sababu hapo ninasema ya kwamba tuwe na mavazi rasmi, isionyeshe sehemu muhimu za mwili. For example kina mama wa Kislamu wakivaa bui bui yao, hiyo sawa. Hata magonjwa yakiweko, lakini huoni, yamefunikwa na bui bui.  Nakilichoko ndani huoni.  Na hivi sasa, hivi sasa wanavaa hata hapo barabarani, upate mama amejaza 'long' ndi.  Sasa wewe akijaza long, we mwanaume wewe huwezi kujifikiri, kwa sababu utasema lugha, na lugha ni pesa, ndio sasa unanunua ukimwi unapeleka nyumbani.

**Com. Salome**: Na je, kuna baba wengine wataka kuomba mfano wa kina baba waislamu wakuvaa kanzu, ukaficha ulicho nacho. Hii ni wakati wa kuzungumza haki za kila mtu, usizilimie zako tu, ukirudisha upande mmoja. Ikiwa ni za pande moja itatubidi kugeuza Katiba tena baada ya miaka kumi. Kina mama wakisema haki zao hazikulindwa wakati huu. Kwa hivyo tunataka kulinda zote. Pengine ni sisi kina baba na kina mama sote wenye tutaomba nguo ya Kislamu Kanzu na buibui sote tufiche tuliyonayo.

Sasa nampa nafasi Bwana Hamisi na ningetaka kusema kua, saa sita unusu tutakihairisha hiki kikao, mpaka saa nane. Ningetaka tena kuwaomba kina mama, sisikii sauti zenu, siwezi kua mama mmoja mwenye kulinda haki zenu. Leo mimi sina maoni, kazi yangu ni kusikiza. Kina mama nataka kuona majina yenu kwenye orodha ya majina; na kila nikiletewa kijikaratasi; naangalia kutoka juu mpaka nchini, sioni majina ya kina mama. Kina mama mnataka kikao cha kipekee, mbali na kina baba? Mnataka vipi? Mnataka cha kipekee, au mnataka kukaa na akina baba, mzungumzie mambo yenu pamoja. Mnataka kuzungumza pamoja? Sioni majina yenu mtazungumza wapi pamoja, na hamko kwenye list ya majina.

Basi Bwana Hamisi K. hayuko? Bwana Washington Opondo. Karibu. Kina mama tafadhali mngetaka kuzugumza pale nje kwa dakika tano hivi mkubaliane kama mnataka kikao chenu pekee, chenye tutawapa, ama mngetaka kikao cha pamoja. Lakini mama hamwezi kuzungumzia kwenye mkutano wangu, kwani si elewei tena vile kunaendelea. Excuse me. If there are any discussions, can they be done at the side, so that we can continue; and come back with a decision. If you want a special seating, we are ready to give it to you. If you want to discuss along with the men, we are very ready to give it to you. However, we do need to continue with this talks uninterrupted. Please, thankyou very much. Endelea Bwana Washington Opondo.

**Washington Opondo**: Nachukua nafasi hii kutoa maoni yangu. Kwa majina ni Washington Opondo. Niko napendekezo moja. Kidogo liko unique, lakini ni maoni yangu. Kwamba wakati wa general elections. Twataka tuwe na political camps. Hizi political camps zitakuja hivi. Napendekeza kwamba, mkutano au mikutano ya mwisho, rallies; kwa wale ambao wanagombea viti ya Parliament, na vile vya civic, wafanye mikutano yao siku saba kabla ya election. Kwa mfano, iwe kwamba ni Jumapili, ndio mkutano wao wa mwisho. Wapewe siku tatu kupumzika, yaani jumatatu, jumanne na jumatano. Siku ya nne, hiyo ni Thursday, wawe katika camps: yaani Thursday, Friday na Saturday, siku tatu. Siku ya nne Sunday, wa-report back katika places zao.

Madhumuni ya kusema hivi ni hivi. Wakati huo ambao watakua wako katika camps, itawasaidia wawe wamepumzika vizuri, baada ya kufanya campaign zao. Na pili litawasaidia wawe hawatapoteza pesa nyingi kukimbia huku na huku. Na kwa upande wa wale voters, pia itawapa nafasi ya kukaa chini, wakingojea election. Waende katika uchaguzi wakiwa na sober minds. Mara nyingi tunaona wakati wa campaign candidates wanakua na shida, kufanya campaign mpaka asubuhi ya election day; kukibizana huku, na huku ku-confuse voters. Hatutaki. Watupe muda na sisi tuwe na la kufikiria tumchague nani. Mara nyingi hua unaona tunachagua the wrong candidate, kufuatana na confusion, wengine wameleta mia moja, na siku ya mwisho yule

wrong candidate, analeta mia mbili mbili, halafu wana-confuse voters: next day wanampigia kura natunakuja kujuta. Kwa hivyo mimi naonelea kwamba twataka tupewe nafasi, hawa watu wawe katika holidays zao siku hizo ili, watupe nafasi kabisa. Tukienda ku-vote Monday next day, tuwe tuko na sober minds. Hayo ndio maoni yangu.

**Com. Salome**: Asante sana Bwana Opondo. Kuna swali kwa Bwana Opondo? Nami pia sina swali kwako. Asante sana kwa maoni yako. Faki Haji. Kama hayuko Bwana Joseph Onyango.

**Joshua Kirui**: Okay thank you very much, I would like to introduce my self: my name is Pastor Joshua Kirui, the one who registered is my fellow worker, am the leader of the 7th day Adventist Church. I would like to begin by reading a verse in the bible. The book of Daniel Chapter 4, verse 17, says: "The sentence is by the degree of the watchers, the decision by the word of the Holy One, to the end. That the living may know that the Most High rules the kingdom of men, and gives it to whom he wills and sets over it the lowliest of men. What I wanted to begin with is that, in this Constitution making, we should realize that God is a ruler, who is ruling in the kingdom of men: and therefore my first recommendation is that Constitution we are going to make should be sub-ordinated to the laws of God, as given to Moses on mount Sinai, the ten commandment.

No. two, I would like to talk about the freedom of worship. Our current Constitution, guarantees freedom of worship to everyone. However the 7th day Adventists have suffered, regardless of the Constitution granting freedom to everybody. Seventh day Adventist members, worship on Saturday. But unfortunately, this day is not recognized as a day of worship. By the way, the commandment no. 4, among the ten commandments, talks about the Sabbath and the seventh day of week, which we recognize as Saturday. But the Seventh Day Adventist members have suffered a lot, especially the students have been expelled from school, for keeping Saturday as Sabbath. We have a lot of our young people, who have denied education, because of keeping the Sabbath. Others have been forced to write examinations on Saturdays instead of being in church. Or taking part in games, taking part in parents days or being denied jobs by the government or by the parastatals because of Saturday.

We would like to recommend that the Constitution recognizes Saturday as a day of worship, so that Seventh Day Adventists may no longer be harassed; or be prevented from worshiping their God. I would like to recommend that, all registered religious organizations be allocated public land equally, favouritism and sectorianism should not be allowed. There is no where in our laws, where churches are classified as minority or majority. What am trying to say is that we find that, in some areas our churches are denied land, to put up churches, just because some people say it is a small church; or it is a minority church. No. 3 I would like to recommend that, religious organizations should be allowed to import tax free vehicles, public address systems, and religious literature; so long as they are used for spreading the gospel. No. four I would like to recommend that, in the current Constitution it says if somebody is aggrieved on the question of religious liberty; he can go to the high court. But many of our people do not have money to go to the high court. I would like to recommend, that the lower courts be allowed, to handle the question of religious liberty; and the government should pay for it.

On the question of family, I would like to recommend, that there should be a section in the constition to address family issues. This will give strength to enacted laws. Parents education should not be left only to churches. The government should give these responsibility to a ministry. Another recommendation is that the Constitution, should guarantee and protect the right the of spouse, child or dependant, to inherit the estate of the deceased; where there was no specific will, on distribution. The Constitution should encourage citizens to make wills. Another recommendation is on health; and I will recommend that more funds should be allocated to the ministry of health. With adequate funds, it will be possible to have sufficient drugs, and equipment in hospitals. The authorities should act first on health institution workers, who steal drug and other equipment meant for patients. Those caught stealing should be sentenced instantly, or made to pay for what they have stolen. What am saying is that, right now in Kenya, you can not get proper medical attention in government hospitals, because there is a lot of stealing of drugs, a lot corruption so am saying those who are doing so should be prosecuted.

**Com. Salome**: Do you have a memorandum for us Pastor?

**Joseph**: Yes.

**Com. Salome**: Then you have one minute because we have five minutes for those with a memorandum.

**Joseph**: Okay I will go very fast. Another one is on the question of abortion. What we are saying is that, abortion be outlawed. It should not be allowed; instead, those engaging in prostitution, should be dealt with, by the law, instead of allowing for abortion. On the question of education, I would like to recommend that the government should provide free education, at least primary education to all. Nowdays we talk of free education, but actually there is a lot of money being paid by parents. So the government should tackle that issue. And lastly on HIV/Aids, I would like to recommend, that activities contributing to HIV/Aids, such as homosexuality and prostitution, needs to be outlawed. Behaviour change approach, should be used, in fighting HIV/AIDS. Thank you very much for giving me that chance.

**Com. Pastor Ayonga**: Thank you very much pastor. Any question for pasto?

**Com. Pastor Ayonga**: Pastor Kirui, you talked citizens to be allowed to make wills, what kind of will is this you are talking about, because one would think that there has not been any problem at any time about will making. Would you please elaborate on this?

**Com. Salome**: I also have a question for you pastor. Infact two related questions. My questions are on abortion. So which part of the abortion do you want to be made illegal, the mans part of the abortion or the woman's: because it takes two to make a child. But the money has been allowed to abort his half. In the present Constitution you can make a baby and say, I do not

want it. I see that as the first level towards abortion. Or is it the physical abortion of going to the doctor, that you want to do away with? I have the same question about prostitution. Again in our present situation, half or 50% of prostitution is allowed,because the man is allowed to prostitute, it is the woman's part that is illegal. So do you want us to re-look at those rules, how do you want us to deal with this? Keep it the way it is; dealing with 50% of the situation, and do you think 50% of the situation, is going to solve the problem?

**Joseph:** Thank you very much, let me response to the first question on wills. What I was saying is that, while the Constitution allows for people to make wills, many people are very ignorant on how to make wills. So people should be educated, and if possible assisted on how to make wills. So that when they die, they do not leave chaos behind. No. two; is the question of abortion. I did not mean to address only one side of the question, what I was saying is, the source of the problem should be addressed. If it is prostitution,then it should be addressed on both sides for men and ladies. The seventh commadment prohibits prostitution; so I was saying that, that should be part of the Constitution, to make it criminal, for either men or women, to engage in prostitution.

**Com. Salome**: Thank you very much. I would like to call Jane Adeya; na huyu atakua mzungumzaji wetu wa mwisho, kikao hiki Saa sita unusu ningetaka kuahirisha kikao hiki, ili watu waende kwa swala, halafu tutakutana saa nane.

**Jane Adaye**: Asante sana Bi. Mwenyekiti, kwa majina naitwa Jane Adeya. Mimi nina maoni yangu, kama manne, ama matano hivi. Oni la kwanza, ni kuhusu uchaguzi wa wabunge. Mimi ni mfanyi kazi, na ni mtetezi wa wafanyi kazi pia.

Ningeonelea katika hii Katiba mnayounda, wafanyi kazi wapewe nafasi sita, wale Trade Unionist wapewe nafasi sita katika bunge; wasiwe kwenye chama chochote. Iwe free itangazwe kua kuna nafasi sita, ambazo zitakua zinapiganiwa ubunge, na watetezi wa wafanyi kazi. Ili tukienda kule bunge tuweze kutetea maslahi ya wafanyi kazi; kwa sababu ya nini kusema hivyo, ni kuwashauri wabunge hao tunawachagua ndugu zetu. Wakienda kule bunge, hawangalii maslahi yetu wanaangalia maslahi yao na familia zao, na watoto wao. Na wakiwazia kua leo tunaongeza mshahara wa wabunge kutoka, may be 50,000 to nusu million, haichukui even five minutes, for them kupitisha huo mswada, wana sign mbio mbio. Lakini wale wanaofanya kazi, walioko mashinani kwenye makampuni, ambao ndio tax payers; ambao wanafanya wao wabunge wapate mshahara kulingana na vile sisi tunavyokatwa pesa kutoka kazini, hatupewi mshahara. Unaweza kuona kama hivi jana ilikuako ni siku ya Labour Day. Ni aibu sana kwa Minister of Labour, kusema anaongeza wafanyi kazi 7%, surely kwa nchi kama hii, ambayo tunakatwa tax pesa nyingi: Waziri kusimama mbele ya umma ya wananchi kusema anatuongeza 7%, ni jambo mbaya sana. Kwa hivyo ningependelea Katiba iwekwe, tukipewa hizo nafasi sita, Minister for labour, lazima awe ni trade unionist; ambaye atatetea masilahi ya wafanyi kazi.

Swala la pili nilikua nikuhusu polisi wetu tulionao. Ndio, wengine ni ndugu zetu, ni jamaa zetu, lakini kazi wanayofanya, ni kinyume ya ile training wanayokwenda kule Nyeri. Unapata siku hizi hakuna kazi, watu wetu wamekua retrenched, watu

hawana kazi, mtu anaamuka asubuhi hajui aende wapi, unatembea unapata mwanamme, anaogopa hata kwenda nyumbani mapema, maanake mtoto ataamuliza, “baba hata biscuit ya silingi leo hukuninulia?” So the man has to stay outside, afike nyumbani may be saa tatu, kama mtoto amelala. Polisi wetu wa Mombasa, maanake mimi ni mzaliwa wa hapa, na nimejaribu kutetea wafanyikazi wangu waloshikwa, kila siku niko kotini. Anakushika usiku, unatembea unaenda nyumbani, may be saa mbili, ama saa moja unusu. Shtaka unalo andikiwa hata ni la aibu. Ati ulipatikana ukirandaranda, na kukojoa barabarani, hatuna hata vyoo vya serikali. Wewe mwananchi utakojoa wapi ukishikwa na mkojo? Hao polisi, vile mwenzangu alivyotangulia kusema, waregeshwe training, they should go back for re-training. Na kusisitiza upande wa polisi, unapata mama siku hizi, mtu akishikwa, akifikishwa police station, for example hii yetu ya Changamwe police station. Hii Changamwe Police Station, ndio imekua koti, at the same time it is a police station, mama ameshikwa na mnazi, ama mtu ameshikwa jioni msako, unaambiwa Bwana ukitaka utoke hapa, toa silingi mia tano; and that thing known everywhere. Sasa police ndio pamekua pahali pa kukatia mtu hukumu ya kulipa mia tano; ambako tuko na makoti, ambaye mtu atakikana apelekwe kule, to plead guilty or not guilty: so that judgement could be done fairly. Kwa hivyo police wetu waabiwe, taratibu za kazi zao, nguvu zipunguzwe.

Jambo lingine lasimamia upande wa Traffic. Sisi wafanyi kazi twapata shida sana, kwanza sisi wa kuishi upande wa Changamwe. Unatoka nyumbani, unatakikana kazini saa mbili. Unapata traffic police, amesimama roundabout saa kumi na mbili na nusu asubuhi: matatu ikipita ashanyosha mkono katikati, they cause a lot of road accidents. Maanake wewe unaenda katikati ya barabara, whereby huna ruhusa ya kusimamisha gari. Mtu anasimamisha gari, na inabidi hiyo matatu ifunge emergency break, maanake traffic ameisimamisha. Na ukisimamishwa hakuna swala la mtu atakuuliza, ni conductor atoke mlangoni, aende apeane mia tano, gari inaenda. Sasa wame-make habit, of getting money through the matatu drivers, ambapo ikiwa huna, labda ndio umeanza kazi; wafanyi kazi wachelewa kwenda kazini. Naiyo kitu imezungumzwa na ikazungumzwa, hatuoni sheria inayochukuliwa kuhusu traffic. Kwa hivyo tunaomba katiba, ma-traffic police, wanaopelekwa mahali, wasikae zaidi ya mwaka mmoja, let them be transferred, so that they feel the pinch. Wafanyie wananchi kazi kulingana na sheria.

Jambo lingine nazungumzia kuhusiana hizi election zetu sisi, kama trade unionist. Trade unionist, tunapata, kulingana na sheria ile ya ILO, inatakikana iwe free and fair election, Serikali ya Kenya kupitia kwa Rais, yeye mwenyewe ali-sign hiyo sheria; kua hawaitangilia any uchaguzi wa watu wa trade union. Lakini inaenda kinyume cha sheria ile ali-sign, kulingana namkataba wa dunia. Unapata tukienda kuchagua mwenyekiti ama general secretary wetu, wakututetea katika maswala yetu ya kikazi; unapata wanasiasa wanaingilia. Kwa mfano uliona ile ya Dock Workers Union here ni Mombasa. Sharif, aliingilia openly, kwenya public, kwenye nini, na yule ni mwanasiasa; he is a Minister. Hiyo sheria ina-govern trade unions, mtu akichagulia, kama ni mbaya ni mzuri, ni sisi wafanyi kazi tumemchagua; tunataka ile sheria inasema kua, serikali isiingilie maswala ya wafanyi kazi, ikae hivyo hivyo. Ukishachaguliwa, ukienda Nairobi, usajiliwe, na uwe wewe unasimamia wafanyi kazi wale waliokuchagua.

Jambo lingine, ni hizi nguvu za president. Wenzangu wamesema, mimi pia naomba zipunguzwe. Na pia hiyo two terms, iwe

hivyo hivyo. Maanake Kenya, hatuko better than any other country. Ukiangalia Tanzania, Rais akisha-serve for only two terms, hababaiki hata kwenda tena ku-campaign. Anajua wakati wangu umeisha, mwengine naye ajaribu, aingia naye achaguliwe, aone atafanyia wananchi nini. Unapata hapa Rais anataka akae toka achaguliwe, mpaka atakapokufa. Hiyo ni sheria mbaya, maanake kama ni mtu anatunyanyasa, atatunyanyasa mpaka siku ile atakufa, ndio unyanyasaji utaisha. Na sisi Wakenya sasa tumepiga hatua, si kwa Waislamu si kwa wakristo. Tumeenda masule tunashukuri ndugu zetu waislam siku hizi pia wanawaruhusu watoto wao kusoma; zamani ilikua wasichana hawasomi. We are very happy we have doctors also who are Muslims, wamesoma wameelewa sheria inaenda wapi. Tunataka Rais apunguziwe, zile nguvu alizokua nazo. Akifanya makosa wananchi sisi ndio tuliomchagua, na sisi tupewe sheria, kama ni two third of Kenya ambao watamvote out, tumpeleke kotini, na yeye ashitakiwe kwa mashikata kama nchi nyingine. Uliona Clinton, alipelekwa kotini, kwa kua alimtongoza mwanamke wa wenyewe, na kesi iliendelea. Pia Rais akifanya kosa, apelekwe kotini, like any other president.

Jambo lingine, sisi tunaomba, iwe kama wakati wa marehemu hayati Mzee Jomo Kenyatta. Waswaili wasema majuto hua ni mjukuu, wajua, you remember mtu akiwa mzuri, wakati anapokufa. Hata leo mmeketi hapa, tutasema ma-commissioner wazuri, lakini wengine watasema ni wabaya. Lakini saa ile utaondoka hapa, tutasema, yule mama alikua mzuri, ama yule mzee commissioner alikua mzuri. Unaangalia wakati wa marehemu Kenyatta, ndio nilikua mdogo, lakini nilikua at least I had the knowledge. Kenyatta alikuwa hawezi kumpa mgeni yeyote Kenya licence, ya kufungua kampuni, mpaka upitie kwa Mkenya, yule Mkenya ndiye atakuwa yuko licenced. Kampuni wewe mgeni, utakua share holder, lakini not to be given a license. Sasa iko opposite, na huyu mtukufu Rais wetu, twampenda tumempigia sisi kura. Saa hizi unapata makazi, na makapuni yote Kenya, ni ya Wahindi. Mhindi anakwambia, hakuna mahali utanipeleka, serikali yako iko kwa mfuko wangu, which is true. You can take them nowhere. Kwa nini mtu anatoka India anakuja hapa anafungua kampuni yake? Akija anakuja na chambari, within two three days anaendesha Mercedez benz. Wewe mkenya unazidi kua mtumwa mpaka siku ile utakufa. Those are the people making this country poorer and poorer. Please Katiba ibadilishwe, Mkenya apewe ruhusa ya kua na license not a foreigner.

Jambo lingine nitasimamia kuzungumzia ni kuhusu hino ministry of lands. Ministry of land iko na watu wako very much corrupt from the province, to the national level,in Nairobi. Unapata councilor, for example yeye ni councillor wa Mikindani, lakini ana ma-title deeds ya Changamwe constituency nzima. Anaenda kila mahali akiona plot ya mtu, anajua mzee alikufa, baba alikufa, watoto wamebaki, hawajui chochote; anaenda Nairobi he turns the title deed, anakuja anasema hii land is mine. And it has happened, na niko na ushahidi, and I have taken some papers to anti-corruption. It has happened here mostly in Mikindani, tunachagua wabunge, mbunge anakua na plot kumi, mtoto wake ana tano, mjukuu ana sita, wewe mwananchi huna hata robo ya kiwanja, na you are the owner of that land, and you are the Kenyan who voted for that MP. Hapa ma-councillor wetu, Bwana mwenyekiti, wapunguzie mambo ya kuuza hizi plot za serikali. Hizi plot zimewekwa na serikali kutoka wakati wa ukoloni zisaidie kwa maswala ya serikali. Hapa Mombasa hakuna hata choo. Tulikua na choo kimoja, Coast Bus, kikauzwa kumejengwa guest house. Tukawa na choo kingine opposite central police, kimeuzwa kumejengwa hall. Sasa, for example wewe mfanyi kazi unatafuta kubarua, umekaa pale nyuma GPO, umepiga mguu kwa mhindi, umetafuta kibarua, umekosa. Umekwenda kula mhogo moja, silingi tano, na maji umekunywa, wasikia mkojo. Hakuna mahali utajisaidia, na hakuna mtu

atakubali uende nyumbani kwake ukakojoe. Maanake hakujui, hajui watoka wapi. We have that problem, na twajiita wanakenya, Kenya tuko free, na Kenya tuko nini, lakini bado twadanganyana. Lazima address wananchi na Wanakenya wajue kua wao ni wana Kenya, na wana haki katika nchi ya Kenya, kama zile nchi zingine.

Jambo lingine na la mwisho; mambo ya kizungumzwa na Mtukufu Rais, ama akisema kua tupunguze bei ya kitu fulani, yatekelezwe. Kama wakati wa Kenyatta nakumbuka akisema, punguza unga iwe silingi tano, ni lazima itakua tano, na kulikua na watu wanazunguka wakiangalia zile bei. Kama umepandisha, unashikwa, unachukuliwa hatua. Lakini saa hivi hakuna, mtu anauza Brookside ni maziwa hayo hayo, ukienda kila duka ni brookside mwenye kutengeza ni mtu mmoja. Unapata mwingine anauza ishirini na nane, mwingine ishirini na tano, duka lingine ishiri na sita. Sasa, huyu mwananchi wa kawaida, ni lini ataweza kujihimudu aweze kula yeye na family yake. Hata kama ni one meal a day, maisha yamekua magumu, Lakini sisi hapa hatuwezi, makampuni yalioko, ni ya Wahindi. Mhindi kukuandika, kama hapa kampuni nyingi, Changamwe Constituency, nyingi zaidi ni za kushona nguo: ambao kina mama na kina baba wanaenda kuomba kazi. It is very sad unapata kua ile kampuni, Muhindi akishakuingiza ndani, kuna shift mbili ya mkusu kutoka asubuhi mpaka jioni. Kuna mwingine anaingia saa kumi na bili na nusu, mpaka kesho asubuhi. Wewe mwananchi wa Kenya, unajiita mimi ni Mkenya, nilitetea uhuru, ama wazazi wangu walitetea uhuru; ukishaingia pale saa kumi na mbili jioni, Mhindi anakufungia ndani, na vifuli kumi, anabeba ufunguo anaenda nao nyumbani kwake kulala. Zile machini zinatumia electricity, you work there under very tight circumstances, ambapo moto bahati mbaya ikipiga shot, tunaenda kupoteza wafanyi kazi wote, wale wanafanya kazi pale, maanake hawatatoka nje. Ukuta unashinda hata hii hall. Serikali inajua, PC anajua, tulimpelekea maswada, ministry of labour wanajua, lakini because hajui yeye, alichukuliwa from nowhere to become a minister, he can not feel the pinch ile mimi nasikia kile kiatu ninacho kivaa. Kwa hivyo, twaomba ikiekwa sheria, isiwe sheria ya mwananchi wa kawaida mdogo, tajiri anakua na uhuru, hapana. Mwananchi ana right, na wananchi na wafanyikazi, ndio wanaweka serikali. Kwa hivyo tuchukuliwe sisi wafanyikazi kama watu muhimu; mimi hata nyinyi pia, ni wafanyi kazi, tupewe maslahi na mshtari wa mbele, katika nchi hii.

**Com. Salome:** Asante sana bi. Adeya. Kuna swali kwa Bi. Adeya.

**Com. Pastor Ayonga**: Mama Adeya, ningalipenda ufafanue vizuri, sikuelewa uliposema, trade union ipewe nafasi katika bunge. Pili, wale trade unionists wanaweza kupigania maslahi ya wafanyikazi. Je? ulifikiria pia, tukianza mtindo wa namna hiyo, kila kikundi kitakuja kusema, tunataka watu na sisi kiasi hiki, katika bunge. Kama ni wakulima waseme, hakuna anayeelewa habari ya ukulima, tunataka watu sita katika bunge; kama ni watu wanaofanya vitu fulani fulani wahubiri pia wa makanisa wa misikiti, wanasema hakuna mtu anaweza kuelewa mambo yetu, isipokua sisi wenyewe. Hii ingeweza kuleta shida. Kwa maana tunapochagua watu, ingeonekana kwamba wafanyikazi ndio huchagua watu wanaoenda bunge, na wanapochagua mtu wamemfikiria uwezo alionao, kwamba ataenda kufikiria maslahi ya kila mtu. Na kwamba angeweza kufanya kazi yake, akichukua mzigo wa kila mtu. Mbona trade union ipewe watu sita katika mbunge, na watu wengine wasipewe pia kiasi wanachotaka. Ikiwa hivyo basi, mambo ya kua na bunge la watu waliochaguliwa haitakua na maana tena.

**Com. Salome:** Kuna maswali kadhaa, nitampa kila mtu nusu dakika, kwa hivyo una saa ya kuuliza swali moja; kwani tayari kumefika saa ya wenzetu Waislamu kwenda kuswali. Kwa hivyo ningepeana nusu dakika hapa. Can you come over please? Tafadhali njoo hapa mbele, na ufupishe sana swali lako.

**Question**: Asanteni sana kwa kunipatia nafasi hii tena. Si swali hasa namuuliza, lakini nikuongezea. Sasa kuongeza trade unions, viti katika bunge. Itawezekanaje na kuna wale wabunge ambao wamechaguliwa kuwakilisha maslahi ya watu wote? Lakini pia Waziri wa Labour akiongeza mishahara ya wafanyi kazi asifanye peke yake tu, lakini ashauriane.

**Com. Salome**: Tafadhali, wakati wa kuenda kuswali umefika, kwa hivyo nitampa Jane nafasi ajibu. Swali lako utatuuliza utakapo pata nafasi ya kuzungumza.

**Jane**: Asante sana Bwana mwenyekiti, mimi nitakujibu kulingana na vile ulivyosema tukipewa nafasi sita. Kumbuka Kenya, idadi ya wafanyi kazi ndio wengi. Ambapo kulingana na tax payers, ndio inafanya nchi iweze nawiri. Kuna miaka mingi hatujapewa misaada kutoka IMF ama World Bank. Na tumejimudu kulingana na zile kazi tunazofanya, kutokana na makampuni yetu. Ndio sababu nikasema, tupewe nafasi sita za wafanyi kazi. Mkulima unayetaja ni mfanyi kazi, maanake tuko na chama cha Wakulima, ambacho wao pia, they are under the umbrella of COTU, ni wafanyi kazi. Mkulima hawezi kua si mfanyi kazi. Nimfanyi kazi anapoamka kwenda shambani, anafanya kazi na yeye pia anachama, kinachomtawala, ambacho kinamsimamia yeye mkulima.

Hao wabunge unaosema sisi tunawachagua kama wafanyi kazi, tulikua tuna-make mistake, tunachagua watu wenyekwenda kuangalia matumbo yao. Niambie wewe toka uwe mwenyekiti, ni lini umesikia bungeni, mswaada wa mbunge yeyote, kutoka pahali popote, ambaye amesimama akazungumza kuhusu maswala ya wafanyi kazi? Either wananyanyaswa, ama mshahara mdogo, ama nini. Wao wanazungumzia matumbo yao, na hata majuzi wamezungumza kua, mtu akiwa mbunge zaidi ya miaka kumi, alipwe pension. Sasa kama mtu akifanya miaka kumi, alipwe pension nusu million, mwingine aingie tena miaka kumi, alipwe tena, hii nchi tutaipeleka wapi? Wao wanajiangalia matumbo yao. Tunataka trade unionist, ambaye watakua wakitetea masilahi ya mfanyi kazi, kutoka mashinani. Example like Zambia, Zambia Chiluba alikua mfanyikazi. A trade unionist like Atwoli of COTU, be made a president, that is why akiongeza kitu, hata silingi moja, wafanyikazi wanaingia kwa barabara. Anajua uchungu wa kua mfanyikazi, ama mtetezi wa mfanyi kazi sababu nchi inaongozwa na wafanyikazi. Kwa hivyo sisi bado, hatutaki kua chama chochote. Kenya is a multi-party country. Tukisema tutakua Kanu, mtatufanya vile mmefanya Mwahima maanake sasa amesema ameenda Ford People anapelekwa kotini. We just want a trade unionist, asimame kama ni Changamwe, tutampigia kura as a trade unionist, akienda bungeni, asichukuliwe kama bunge wa kawaida awe ni mbunge anatetea maslahi ya wafanyikazi; si maslahi ya kua ataangalia tumbo lake. Na tuwe na sheria, we have a right, to vote him out, kama hatatufanyia maswala yetu. Maanake hata bungeni, hakuna maswala ya kua, wafanyikazi wanahaki ya ku-strike. Juzi mliona wenzetu, wa Kenya Airways, wamestrike kulingana na maswala yao na haki zao, kua wananyanyaswa na ile kazi kweli ni ngumu.

**Com. Salome**: Jane, tafadhali fupisha ili wenzetu waende wakaswali.

**Jane**: Sawa, hiyo ndio tunasema tuwe na wale wafanyikazi, wangekua bungeni, wabunge wafanyikazi wangewatetea, hawangeambiwa tena, wajisajili tena waombe, waende wapigie mtu magoti, waregeshwe kazini. Ingeandikwa wewe, ile ni haki yako. Ndio maana tunataka wafanyikazi, wawe na watu wao bungeni, wakutetea haki zao, na maslahi ya pale wanapofanya kazi.

**Com. Salome**: Asante sana. Ningetaka sasa wakati huu, kukihairisha kikao hiki, mpaka saa nane, asanteni sana.

**Com. Pastor Ayonga**: Kuna Washington Opondo? Faki Haji, sasa mbona majina haya yako hapa, na wameongea. Ebrahim Omar, Mwangi Wa Ngereka. Kijana wewe ndiye Mwangi? Nitakupa dakika tano, utoe maoni yako, na toa yale makubwa makubwa. Tafadhali tuwe kimia, ili Mwangi atoe maoni yake.

**Mwangi Wa Ngereka**: Katiba hiyo mpya, ijaribu haswa kuangalia vijana. Ukiangalia nchi yetu hii, vijana ni wengi sana, na wengi wetu hatuna kazi; na tunaishi maisha hivi hivi. Si kwa sababu nchi yetu haina raslimali ya kutosha, mali iko, lakini katika ule uongozi mbaya, ndio imefanya vijana wengi, tusiwe watu ambao tunajiweza vizuri. Kwa hivvyo ningependekeza, Katiba mpya ambayo itatengenezwa, kama ni upande wa mawaziri, ama kuchaguliwe ofisi moja ambayo itakua na waziri, ambaye atakua akihusika na mambo ya vijana, humu nchini.

Halafu vile vile ningependa kupendekeza, Civic Education. Unajua kwa kweli ni muhimu kupata hii elimu ya haki ya binadamu; ni nzuri sana. Kwanzia miaka kumi hivi iliopita, tungekua tukifundishwa haki zetu; nafikiri watu wangekua wengi sana, kuja kutoa maoni; kwa vile ambavyo wanajua haki zao. Lakini kwa vile wengi, hata pengine ile Katiba iko sasa hivi, wengine wetu hatujaiona, tunasikia tu Katiba, Katiba. Kwa hivyo ingekua vizuri kama watu wangekua wakifundishwa, tusiwe tu ni wakati kuna mambo ya Katiba. Iwe ni sheria, watu wawe wakifundishwa juu ya Katiba ya Katiba yao.

Halafu vile vile kuhusu kazi. Kwa kweli nchi yetu nafikiri ina mambo mengi ambayo watu wanaweza kupata kazi, haswa upande wa ukulima. Tuna rotuba nzuri sana, na nafikiri viongozi wetu ambao wanatuongoza, kama wangekua na muelekeo mzuri wa kuangalia, hasa raslimali za upande wa ukulima, nafikiri kazi tungezipata.

Halafu juu ya ID. Unapata pengine mtu akitaka kuchukua kitambulisho, kama pengine nimekaa hapa Mombasa Pwani, au pengine mtu wa Pwani ametoka hapa ameanda Nairobi amekaa. Ukienda kuchukua ile kitambulisho na wewe ni Mkenya, unaanza kuambiwa, sijui enda uchukue kitambulisho ya nani, enda ukuje na sijui nini, nini, hiyo si halali. Ningependa kitambulisho, mtu kama ni Mkenya, na tumeambiwa katika hii Katiba ya sasa Kenya ni yetu, unaweza enda mahali popote ukae, ufanye kitu chochote. Ningependa kama nikuchukua kitambulisho kama una zile sitakabadhi ambazo wanataka, wakubali

uchukue kitambulisho bila ya kukuambia mambo mengi.

Halafu tena nguvu za Rais. Ningependa Rais, nguvu zake zingine zipunguzwe. Ama pengine naona wakati mwingine, pesa nyingi zatumika tu hivi hivi. Sababu pengine kama Rais amekaa amependekeza pengine kuteuwa kamati fulani, ishughulikie mambo fulani; utapata katika zile pesa ambazo zinatumika, zitakua ni zetu wananchi, na kukiwa na kamati nyingi kama hizo, pesa zetu zitatumika hivi hivi, na pengine hizo kamati hazina mafanikio yeyote. Kwa hivyo ningependa kamati kama hizo kwanza kabla Rais mwenyewe hajazichagua, zichaguliwe na bunge kwanza.

Halafu kuna hii freedom of assembly; pengine kuungana kwa watu. Nafikiri kuungana kwa watu ni vizuri sana, kama pengine kuna mtu anataka kutoa maoni, watu wakikusanyika pamoja, ni vizuri sana watu waungane pamoja, kama mtu anatoa maoni; mradi tu isiwe ni maoni ya uchochevu, ama maoni mabaya. Lakini kama ni maoni ambayo yatasaidia ni mazuri sana.

Halafu elimu, although elimu imekua ni ya bure sasa, lakini naona si ya bure. Kwa sababu watoto bado wakienda shule, wanaitishwa fee, natunasikia ni ya bure. Kwa hivyo pengine kama hiyo section ambayo ilipitishwa, elimu ikue ni ya bure, pengine itiliwe maanani zaidi. Ndio hata sisi tunatoa maoni hapa, tujue hata sisi tukiyatoa yatakua na umuhimu kwetu. Si kuja hapa kusema mambo, ambao baadaye hayatatekelezwa. Halafu kuhusu elimu ya watu ambao wanahitajika kuchaguliwa kama wabunge ama kama councillor. Wengine wamesema elimu pengine iwe ya university.

**Com. Pastor Ayonga**: We sema yako wacha ya wengine. Maoni tunataka ni ya Mwangi Wa Ngereka, si ya wengine.

**Ngereka:** Okay thank you very much. Elimu ambayo inatakiwa kua nayo, kama unataka kua mbunge, ama councilor; mimi maoni yangu ningependekeza hivi, kama mradi tu umefikisha elimu ya form four, ama pengine una elimu ya darasa la nane. Unajua uongozi si elimu. Kuna mtu ambaye utapata amesoma sana, lakini kwa kusema ukweli, hawezi ongoza watu. Na kuna mtu ambaye hajasoma, lakini anaweza ongoza watu vizuri sana.

Halafu katika makabila, Kenya tuna kabila nyingi sana, na tumekubaliwa tukiwa makabila mengi, kuishi popote; kwa hivyo mtu akitoka hapa akitembea mahali fulani, na ukae hapo zaidi, pengine ukue unataka kununua kitu fulani hapo; hivyo naona ni haki uweze kununua hicho kitu.

Halafu kumalizia, ningependa kuongea juu ya birth certificate. Birth certificate ni kitu muhimu sana, na hizi vitu zingine vinaitwa passport. Kwa hivyo ningependa katika Katiba mpya, vitu kama hizo, ziwe zikitolewa bila mtu kuulizwa mambo mengi; iwe ni kama vyenye mtu anachukua ID, juu ni haki ya mtu kupata vitu kama hizo. Asanteni.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante sana, hayo yalikua ni maoni ya Mwangi wa Ngereka. Kuna yeyote aliye na swali? Mwangi unaweza kuja upande huu ujiandikishe. Next ninataka Peter Owino. Situlikua na Peter Owino ni the morning? Ni wewe ndiye

uliongea asubuhi? Unaweza kuchukua kiti Peter Owino.

**Peter Owino**: Asante sana Bwana mwenyekiti wa tume hii.

**Omari Hasan Shaban:** Salaam Aleikum, jina langu naitwa Omar Hassan Shaaban. Kwanza maoni yangu ni juu ya aina ya serikali. Ningependelea kua serikali iwe ya ubunge, ambapo waziri mkuu, anachaguliwa na chama chenye uwezo zaidi. Na rais abaki kama ishara ya Taifa. Pili ni juu ya uraia. Ningependa, mtoto aliyezaliwa na mzazi ambaye si mwananchi wa Kenya, na ameolewa, au ameoa Mkenya, apewe uraia automatic, bila kuulizwa maswali. La tatu, ningependelea kua wabunge wateuliwe wale wazaliwa wa pale mahali. Sio mtu kutoka mbali aje asimamie hapa, ambaye hatajua hali ya watu wa pale. Yule mzaliwa yeyote hata kama ni wa kabila gani; lakini amezaliwa pale mahali, asimamie ubunge au udiwani ili aweze kuongoza watu wa pale.

Tatu ningependelea tuwe na wabunge wa kuteuliwa maalum, au madiwani maalum: lakini hawa wakiteuliwa, wachaguliwe kutoka makabila madogo, ambayo hayana representatives katika bunge au katika council. Wachaguliwe nao waweze ku-represent watu wao, ambao ni wa makabila madogo.

Lingine, ningependa vyama vya kisiasa vichunguzwe. Badala ya kuweka open, ya vyama vyovyote, tuweke vyama vitano visimamie nyadhifa ya nchi. Zingine ambayo nilokua nalo; bunge liwe na jukumu ya kusimama peke yake, bila kuingiliwa na Rais, au na serikali. Lenyewe lisimame peke yake bunge liwe na uwezo. Ningependa pia kuchaguwa kwa mawaziri, wachaguliwa na Rais, lakini wapelekwe majina yao katika bunge, ili lidhinishe, kua watu hao wanafaa kufanya kazi ya uwaziri au la. Ofisa yeyote, ambaye atachaguliwa kuongoza, katika nyadhifa zozote, pia apelekwe katika bunge; badala ya Rais ku-appoint apeleke katika bunge; wabunge wapitishe kua mtu huyu anafaa hau la.

Na vile vile katika uraia; identity card, iwe ni ushahidi maalum ya kua Raia. Kwa hivyo nashukuru sana Bwana Kamishena kwa kunipa nafasi hii; na mengine yamo, lakini nitayapeleka pale kidogo yatachukuliwa.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante Bwana Omar Hassan. Kuna yeyote ana swali? Mzee unaweza kuja hapa ukatuachia maandishi, na ukajiandikisha. Juma Yusuf.

**Juma Yusuf**: Bwana Kamishena, wananchi waliokuja kusikiliza au kutoa maoni, kuhusiana na mambo ya Katiba. Mimi naitwa Juma Yusufu, na toka hapa katika kijiji cha Kwashee, katika hii tarafa ya Mikindani. Mimi maoni yangu ni kuhusu muundo wa uchaguzi. Bwana Kamishena, kama tunavyojua, uchaguzi ni mojapo ya misingi ya kidemokrasia. Katika misingi tofauti tofauti, uchaguzi una-play part kubwa sana, katika kuiendeleza hii demokrasia. Mimi maoni yangu, Bwana Kamishena, ni kwamba, uchaguzi uwe umewekewa tarehe maalum na bunge. Kama vile nchi nyingine zinavyofanya. Isiwe kwamba huu uchaguzi itakua Rais ana mamlaka.

Jambo la pili, ni mamlaka ya Rais: katika Katiba hii ya sasa, inampa Rais uwezo mkubwa sana wa kuchagua na kufuta. Rais anaweza asubuhi akamchagua waziri, jioni akamfuta. Kwa hivyo mimi napendekeza kwamba, uwezo wa Rais upunguzwe kiasi cha kwamba, huyu Rais kwa mfano, akiwa anakasoro yeyote; aweze kufikishwa kwenye kamati ya bunge na kushitakiwa. Vile vile uteuzi wowote wa Rais anaoufanya, ikiwa ni kwa makahamu wa Rais, ikiwa ni mawaziri, ikiwa ni vyeo vikubwa vya serikali, kuwe na kamati maalum ya bunge; ambayo itachunguza ability ya hao watu aliowachagua.

Jambo lingine ni kuhusiana na vyama vya kisiasa. Hii leo, tumeona kwamba katika miaka thelathini na sita iliopita, tulikua tumezoe kuwa na chama kimoja cha kisiasa, mpaka wakati 1992 wakati ile section 2A ilipoondolewa. Tuliona kwamba, kulikua na utaratibu wa chama kimoja, kua na uwezo wa kila kitu. Maanake uwezo wa kutumia fedha, uwezo wa kutumia vyombo vya habari, kwa manufaa ya chama kile. Kwa hivyo tunaomba kamati hii, Bwana Kamishena, ifikirie kwa hivi sasa, kuna vyama vingi vya kisiasa, na vyama hivi vyote vipewe uwezo sawasawa. Vipewe nafasi sawasawa. Kama ni fedha za kushughulikia mambo ya uchaguzi, kama ni vyombo vya habari vile vile, maanake kupewa air time; kwa sababu itakua ni makosa sana, iwapo kwa mfano, chama kile kinachotawala kiweze kupewa uwezo mwingi kuliko zile vyama vingine. Itakua lile lengo, ambalo sisi tunalifikiria la kidemokrasia, itakua hatujalitimiza.

Kuhusiana na haki za mwananchi, Bwana Kamishena ikiwezekana hii kamati ya kutengeneza katiba, ifikirie sana mambo ya elimu na afya. Hii leo katika Kenya, unakuta kuna familia nyingi sana, za watu ambao hawawezi kusomesha watoto wao, kwa sababu hali zao za kifedha ni mbaya. Kwa hivyo matokeo yake ni kwamba, watoto wengi sana wanazunguka; sio kwamba hawataki kusoma, lakini ni kwamba wazazi hawana uwezo wa kuwasomesha. Kwa hivyo tunataka kuwe na utaratibu, wa hii serikali , ya chama chochote; ; kuwe na specia budget, ambayo itawekwa, ya kuweza kuhudumia mipango ya elimu, na vile vile ya afya. Nakumbuka wakati wa nyuma, ilikua ukienda hosipitali za serikali, zilikua ni bure. Lakini labda kwa sababu ya uchumi kuharibika, ilibidi kufanywa cost sharing. Kwa hivyo mimi napendekeza, twajua uchumi wetu ni mbaya, twajua serikali haina pesa, lakini izingatie kuweza kupunguza ile idadi ya pesa ambazo inalipisha watu, ili hatimaye watu waweze kupata matibabu yanayostaili.

Jambo la mwisho, ni kuhusu mahakama, na haswa kuhusiana na ofisi ya kadhi. Sisi kama waislamu hapa Kenya, sisi kuna sheria zingine, kwa mfano za umilikaji, ambazo sisi hutumia kitabu cha Mwenyezi Mungu. Kwa mfano, wewe ni Bwana, uko na bibi, ukifariki, katika kitabau chetu cha Koran, kinaelezea kwamba, bibi anakiwango fulani cha pesa atapata, kwa ile mali ya Bwanake, watoto wanakiasi fulani cha pesa: lakini utakuta kwengineko huenda kukatokea ubishi. Yule mzee ameshaondoka ikawa mama, kile kiasi ambacho amepewa kulingana na ile sheria ya Koran, yeye akapinga kwa hivyo yeye akaenda katika mahakama kuu. Kwa hivyo mimi nafikiria, hii tume iweze kuifanya hii ofisi ya Chief Kadhi, iwe independent iwe maoni yake, yaani maamuzi yake, yasiweze kupelekwa katika high court. Kwa hivyo nikimalizia hapo, Bwana mwenyekiti, naomba kwamba hayo maoni tulioyatoa, nyinyi mtayazingatia na vile vile mtayatimiza kwa vile tunavyotarajia.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante sana Bwana Juma Yusuf. Hayo maandishi utatupa?

**Juma**: Hapana, sina maandishi.

**Com. Pastor Ayonga**: Huna maandishi na nimeyaona?

**Juma**: Ni points.

**Com. Pastor Ayonga**: Basi Kanda imenasa maneno yako yote. Njoo hapa ujiandikishe. Joseph Ngutu.

**Peter Owino**: Tutakua na mambo ya price control hata wewe ukiwa umelima mahindi yako, utajua itaenda kwa bei Fulani, serikali imetangaza. Lakini sasa, ikiwa leo serikali inakwambia, uza mali yako vile unavyotaka. Itakua ni vipi yule mtu ambaye anapata mapato ya juu, na mapato ya chini, zote tunanunua hiyo bidhaa bila kuangalia huyu anapata mshahara silingi elfu mbili, huyu anapata million moja.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante kama unaweza kutoa maandishi yako, ujiandikishe hapa. Huyo alikua Peter Owino. Micheal Magak. Unamaandishi Micheal. Nitakupa dakika tano za kumulika maandishi yako. Sema majina yako.

**Michael Magak**: Kwa jina naitwa Michael Magak. Nawakilisha muungano wa mashirika yasio ya serikali inaitwa, Elimu yetu Coalition. Elimu Yetu Coalition ni muungano wa makundi mbali mbali ya mashirika yasio ya serikali, yaani Civil Society Organisation; na makundi ya wataalamu, yaani professional groupings. Pia tuko na education and research institutions, na pia tuko na washiriki wengine katika sector ya elimu yaani education sector. Maoni haya ni maoni ya Elimu Yetu Coalition, sio maoni yangu tofauti. Mimi nilipewa jukumu la kuleta maoni haya hapa.

Kwanza tutatoa maoni kuhusu elimu. Nasema hivi, the Constitution of Kenya must entrench education as a fundamental right and be part of the first generation line. And make universal free primary education constitute the spirit for the framework of a new Constitution. Nikumaanisha, elimu itambuliwe katika Katiba mpya, kama haki ya kimsingi. Na maoni yetu ni tagi zote za kimsingi zisiwe zinaweza kubadilisha na bunge, lakini ziwe zinaweza kubadilishwa na kura ya maoni ya wananchi wote, ambao wamesajiliwa kupiga kura. Wabunge wasipewe uwezo wa ku-amend provision for fundamental rights. Of which we want education to be considered, part of that.

Pia kuna maadili Fulani, yaani principles, ambayo tumeyafikiri tukayaweka chini, katika mswada huu. Kwanza tunataka elimu iwe ina ambatana na mahitaji ya wananchi. Education should be responsive to the needs of the people. Tena tunataka access to education. Uwezo wa wananchi kupata elimu. Enrolment, retention, completion and transmission: that every person, child,

youth, adult shall be able to benefit from educational opportunities designed to meet their basic learning needs. Kila mwananchi awe mtoto, awe kijana, awe mtu mzima, awe na uwezo wa kupata elimu bila ubaguzi wowote. That everyone has a right to education and it shall be free and compulsory in all elementary stages. Nataka elimu iwe ya bure na ya lazima kwa watu wote. That the focus of basic education, must be actual learning rather than organized rote learning. Elimu iwe practical sio mambo ya cram vitu, halafu ukitoka huko huwezi kuwa productive.

Tunataka katika Katiba itabue kwamba, that the state will afford subsidy towards payment of school fees, to assist parents, should the burden of education, be beyond their means. Hiyo ni kumaanisha tunataka serikali ianzishe fund fulani ya kushughulikia watoto wa Kenya, ama watu wazima ambao watahitaji elimu ya juu. Kama higher education loans board, lakini iwe ya watu wote, sio, wa higher education peke yake.

Halafu pia tunaongea mambo ya management, decision making, and supervision and quality assurance, katika sector ya elimu. Katiba iwe na an independent Constitutional authority, that is answerable to Parliament, si wizara ya elimu. To regulate sector ya elimu na hii iwe composed of eminent persons representing all stakeholders. Na tukisema wahusika, stakeholders tunamaanisha wazazi, teachers, sponsors , kama kuna mashirika yana-sponsor mashule, wanafunzi na kadhalika. Tunasema pia ili walimu wajisikie huru, Teachers Service Commission iwe a Constitutional institution. Iwe entrenched in the Constitution, na Commissioners wawe na security of tenure of office. Ili wakitoa mwongoza Fulani, wanatoa bila uoga wa kufutwa kazi. Hivyo, we will ensure that independence of the teaching profession. Na pia, uongozi wa mashule, kama tuna board of governors, parents teachers associations: tunaonelea tuwe na management board, sio BOG wala PTA. Tuwe na management board ya kuongoza mashule.

Pia kuna mambo fulani ambayo yanachibuka katika sector ya elimu, yaani contemporary challenges affecting our education. Moja yao ni HIV/Aids, ingine ni usalama, poverty, ingine ni gender issues, na teenage pregnancies na child labour. Kwa hivyo tunasema hivi, the new Constitution must ensure, that there is sufficient response in our basic law to emerging contemporary charges in our education. The state should provide education opportunities to all children, especially those with special needs, and difficult circumstances. Kama wale walemavu, wafikiriwe sana; na wale wengine wanamahitaji maalum.

Affirmative action: kule kuwafikiria watoto wasichana, lazima tukubali, kwa sababu za ki historia, sababu za kimila, na maadili Fulani; watoto wasichana hawawezi shidana na wavulana wenzao. Lazima kuwe na affirmative action, ndio wakifika kiwango wanachoweza shidana na wavulana sasa tutawawacha washindane. Lakini kwa hivi sasa, kwa sababu za kihistoria, na sababu zingine, hatuwezi kuwawacha hivyo. Kwa hivyo kuwe na affirmative action, katika education. Requirement for enrolment ya wasichana, iwe kidogo chini.

kuna education financing, yaani matumizi ya pesa za serikali, katika elimu. Serikali inatumia shilling kumi na mbili kwa mwaka, katika mtoto moja, katika primary school. Kulingana na utafiti wetu. Wale wanauchumi hodari, are telling us, serikali inahitaji,

only four hundred shillings per child; tupate elimu ya bure, kwa watoto wote wa Kenya, katika primary school. Silingi kumi na mbili ni aibu; kama serikali inatumia silingi kuma na mbili kwa kila mtoto kwa mwaka mzima, kwa hivyo haina nia ya kuwapatia watoto elimu ya bure. Na sisi tunataka elimu ya bure, ya lazima, na kwa watoto wote. Halafu nitamalizia na mambo ya curriculum.

Curriculum iwe inafikiria mahitaji ya watu wa sehemu fulani. Kama physics haina maana na mtoto ambayo yuko Ganze, asifundishwe physics. Lakini kea wale wanaunda curriculum. The curriculum will not be subjected to frequent and uncoordinated changes to ensure stable resource base in terms of materials, and text books. That panels of teachers should be constituted to develop the curriculum at zonal levels, to ensure relevance and head teachers should not be involved.

Head teachers. The new Constitution must ensure that over specialization should be removed from our curriculum, so that education provided produces an all round person. Na mwisho sisi katika Elimu Yetu Coalition Bwana Kamishena, tuko na imani na Commission yenu, kwa hivyo tunawaomba muendelea na kazi yenu, isipokua mambo mengi yanatoka huko na kule. Nyinyi ni kama wakunga, na wakunga wakizalisha mama, hawasikii kilio cha mama, wanamwangalia yule mtoto yuko karibu kuzaliwa. You are like midwivies, soon you will deliver to us a bouncing healthy baby, called a New Constitution: so, mzibe masikio yenu kwa loud mouthed politicians ambao wanataka kuharibu mambo ya katiba. Kwa sababu when a mother is about to give birth to child, lazima asikie uchungu na maumivi. Go ahead do not listen to anybody. We have confidence in you, and produce a good Constitution, that will stand the test of times.

**Com. Pastor Ayango**: Thank you Bwana Magak. Na kabla sijakuwacha utoke, I need some clarification. You just said that the government is spending Ksh. 12 per child, per year. Does this include primary, secondary and university, or what level does these Ksh. 12 pay for? And also how much money would have been adequate per child, per year, in your estimation, or as per your research?

**Magak:** Bwana Commissioner, tumefanya utafiti Kenya mzima, kwa sababu tuko na branches katika mikoa yote ya Kenya. Na tumepata serikali inatumia Ksh. 12 peke yake, kwa kila mtoto, katika primary education, kwa mwaka. It is horrible it is shameful. Na kulingana na swali lako la pili: kulingana na utafiti wetu, tunahitaji Ksh. 400 kwa mtoto mmoja, kila mwaka, ili watoto wote wa Kenya, wapate elimu ya msingi, bure. Utafiti wetu unaonyesha kuna watoto million tatu Kenya mzima, ambao hawako shuleni, hawana elimu hata kidogo. Na pia utafiti wetu uanonyesha kuna watu wazima 4.2m, hawajui kusoma wala kuandika kabisa kabisa, na hao wanapasa kujumuishwa katika elimu. Thank you.

**Com. Pastor Ayonga**: Thank you Bwana Magak. Unaweza kutuachia copy ya memorandum yako? Asante, unaweza kuja hapa ukajiandikisha. Sasa namtaka Mzee M. Mwidadi. Huyu ndiye Mzee Mwidadi? Mzee sema majina yako, yaingie kwa kanda, na halafu nitakupa dakika tano utumulikie memorandum yako.

**Mzee Mwidadi**: Mwenyekiti wa mkao huu, wa Tume ya kurekebisha Katiba, na wananchi ambao wamehudhuria. Jina langu ni Mzee Mwenyeuzi Mwidadi, kutoka kijiji cha Jomvukuu, lakini hapa nawakilisha Wamiji Foundation. Mwenyekiti sina memorandum ya kutoa, kwa hivyo nafikiri, nastaili kupata dakika kumi. Kwanza nazungumzia Katiba yenyewe vile ilivyo, ni kitabu wengine hawajakiona. Moja ya sababu, ambayo sisi twajaribu kurekebisha hii Katiba, ni kua hii Katiba inaupungufu. Upungufu wa kwanza katika Katiba hii, haina utangulizi. Preamble, tukiangalia Katiba za nchi zingine ulimwenguni, mfano Katiba ya Canada, katika utangulizi au preamble imesema: Katiba ya Cananda itafuata mfumo wa serikali ya Uingereza. Kwa hivyo wewe ukishika hiyo Katiba kuisoma, utajua kile ambacho kitafuata, kile ambacho wakitarajia, katika Katiba ile.

Vile vile Katiba hii, mwenyekiti wa mkao huu, haielezi hii Katiba yamuhusu nani. Sisi leo tumeona tukija pale, tumeulizwa ujitambulishe kama Mkenya. Kwa hivyo twataka katiba mpya, ieleze wazi wazi, kua Katiba hii yamuhusu nani, na matarajio ya mwananchi wa kawaida, katika Katiba hii. Msingi wa Katiba yeyote ni wananchi wenyewe, wamehusika vipi kuitengeneza katiba ile. Kwa hivyo sisi twaishukuru serikali ya Kenya; imewapa wananchi nafasi, kushiriki kurekebisha Katiba hii, kwani jambo lolote ukishiriki, hua na nguvu.

Kitu kingine ambacho kimepungua katika katiba hii, ni kua hakuna kifungu chochote katika katiba hii, ambacho kimeeleza sisi wananchi wa Kenya tutailinda vipi, Katiba hii. Ukichukua mfano wa Katiba ya Uganda, kuna kifungu kimeeleza, watu wa Uganda watailinda vipi Katiba yao. Hata imesema ikiwa ni lazima, waweza kuilinda katiba kwa kumwaga damu. Kwa hivyo tumeona, kwanza haina haiina utangulizi, ambao ni muhimu sana, ni kama dibaji, kitabu ukikisoma hujui haswa madhumuni ya kitabu kile ni nini.

Vile vile Katiba hii, haikueleza matarajio na malengo ya Mkenya wa kawaida. Kwa hivyo katika ile preamble, au utangulizi, twataka Katiba ieleze wazi, matarajio na lengo, la mwananchi, katika Katiba ile. Na vile vile iongeze tungelinda vipi katiba hii yetu. Katiba vifungu ambavyo nataka kuzungumza virekebishwe, kwanza ni kifungu cha arubaini na saba, katika Katiba hii; ambacho kimeeleza utaratibu wa kubadilisha Katiba. Tumeona katiba yetu ya Kenya, umri ni miaka thelathini na sita, lakini imebadilisha mara thelathini na mbili, na ukichukua Katiba ya wenzetu ya wa Amerika; imeudwa mwaka wa elfu moja mia saba na themanini na saba, one thousand seven, hundred, eight seven lakini imebadilishwa mara ishirini na sita peke yake. Umri wake ni miaka mia mbili na kumi na tano. Kwa hivyo tujiulize, kwa nini Katiba yetu, ambayo ni changa sana, imebadilishwa mara nyingi, kuliko katiba ya Amerika. Kwa hivyo tulikua twaiomba Tume, kwanza iangalie misingi ambayo ni muhimu kutiwa katika Katiba mpya. Mfano, katiba ya Uingereza, msingi wake muhimu ni mila. Vile vile ni common law. Tatu ni bill of rights, na nne ni conventions ambazo ni traditional agreements. Kwa hivyo, vitu kama hivi, ndio inafanya katiba kua na nguvu, kwa sababu katiba ya pata msingi. Katiba yetu ya Kenya, haina msingi wa ki Katiba. Kwa hivyo twaiomba Tume, wakati hii Katiba ikiundwa, iwe na misingi, kwa sababu misingi ndio inaifanya Katiba kua na nguvu; na hua si rahisi kubadilishwa.

Kifungo kingine ni kufungo cha hamsini na sita, ambacho kimempa Rais wa nchi hii sasa, kuamka asubuhi, hata kabla hajanawa uso kutangaza kua bunge limevunjwa na uchaguzi ufuate. Tumeona Katiba nyingine za ulimwengu, zina calendar kuonyesha

bunge laweza vunjwa vipi, laweza kuahirishwa vipi; na tulikua twaona vile vile, itakua ni muhimu kuwa nguvu za kuendesha bunge lisiwachiwe ofisi ya Rais peke yake.

Jambo lingine ambalo nimeliona limepungua, ni katika mambo ya ardhi. Land matters and rights. Katika Katiba hii ya sasa, mambo ya ardhi ambayo yamezungumzwa katika kifungu mia moja na kumi na nne, mia moja na kumi na tano, mpaka mia moja na kumi na nane; ni habari ya trust land peke yake. Ardhi ya mdhamana. Lakini ardhi nyingine, hata ardhi ya government, ambayo government land ilitokana na crown land ordinance, ambayo ilifanywe elfu moja, mia tisa na kumi na tano. Tukiangalia sasa, mkuu wa nchi, afaa kua custodian peke yake, sio aweza kugawanya ardhi vile anavyotaka. Kufuatana na sheria za ardhi sasa, ni makosa sana. Jambo lingine ambalo nimeona linakasoro katika mambo ya ardhi, ni kua badala ya kuweka trust land peke yake, vile tungefanya katika Katiba tuangalie, how are we going to administer government land? Government land act, ambayo ni chapter mia mbili na thamanini, ya sheria za Kenya, haikutoa muongozo kamili, kufuatana na nguvu za kikatiba. Ardhi ya serikali yafaa kumilikiwa namna gani? Kwa hivyo twaiomba Tume, in addition kuzungumzia habari ya trust lands.

Nitazunguza kidogo habari ya governance. Tumeona sasa kuna matatizo makubwa, tuaanze kiwango cha chini local government. Wakati ambapo tuna councillor wa area, na tuna chief wa area. Utaona kama kuna project au kunajambo lolote, chief atakuja aseme, "mimi ndio nawakilisha serikali kwa hivyo ili nataka lifanywe kufuatana na mwendo wangu". Na vile vile atakuja Councillor aseme, "mimi nimechaguliwa na watu, kwa hivyo mimi ndio nina nguvu za watu, kwa sababu mine is an elective post". Kwa hivyo tumeona, hii parallel governance, imetuletea matatizo makubwa sana. Sisi twaiomba Tume iangalie, ikiwezekana katika hizi serikali mbili, serikali ya local authority, na vile vile serikali kuu kupitia kwa provincial administration, ziwe harmonized. Iangaliwe njia ambao, hizi pande mbili zinafanya kazi namna gani.

Jambo lingine mwenyekiti ambalo natakakuzungumzia hapa, ni habari ya haki za kibinadamu. Katika Katiba hii ya sasa, sura ya tano, Katika kifungu kifungu sabini mpaka kifungu thamanini na sita, kimeeleza haki za kibinadamu. Lakini tumeona katika hizi haki za kibinadamu, nyingi za vunjwa; na hua yule ambaye si mueza, hawezi kuchukua kesi yake, kwa Constitutional court. Lakini tumeona nchi zingine za ulimwengu, hizi Constitutional courts au courts za Katiba ziko, kuna haja yakuiunda. Kwa hivyo ukiwa na kesi yako, ikiwa haki zako za msingi zimevunjwa, waenda moja kwa moja, kwa koti ile ya Katiba. Na nchi zingine kama tujuavyo, wasaidiwa ki fedha wapewa legal advice, legal assistance; kwa hivyo tungeomba, kwani msingi wa Katiba yeyote ni haki za binadamu. Ikiwa haki za binadamu hazijalindwa, Katiba ile itakua haina maana yeyote. Kwa hivyo twaiomba Tume hii, ibunishe koti ya Katiba, iwe ni koti kama hizi koti zingine ambazo tunazo; na mtu yeyote aweza kupeleka kesi yake, akifikiria katiba au serikali imedhulumu, imevunja haki zake za binadamu. Sasa ziko sura ya tano, kifungu cha sabini, mpaka themanini na sita.

Kitu kingine cha mwisho, ambacho nataka kuzungumzia, ni habari ya pension. Ama haki zile za wale ambao wame-retire. Tumeona katika Katiba ya sasa, Principle Pension Officer, au yule sasa ni Director wa Pensions; amepewa uwezo na Katiba, na vile vile kufuatana na sheria ya pension act, kua aweza kumsimamisha mtu ambaye apata pension, asiendelee kupata pension

yake. Nilikua nafikiria, hizo itakua ni nguvu amepewa mtu, na hakuna uchunguzi wa kutosha kuhakikisha kua makosa ambayo yule mtu ambaye apokea pension, amefanya, hastaili pension yake kusimamishwa. Kwa hivyo nilikua na fikiria mimi, kabla wale ambao wanapokea pension, kutoka kwa serikali au mashirika mengine, kue na tribunal ambaye itampatia nafasi yule mtu, kupeleka defence yake, kabla pension yake haijasimamishwa. Kwa hivyo nilikua nafikiria kifungu cha mwisho, ni kifungu ambacho, kieleze mwananchi wa kenya ataweza vipi kuilinda hii Katiba. Ikiwa hii Katiba hakuna kifungu cha kuilinda, itakua maanake shughuli zote hizi tulizozifanya, zitakua hazina maana yeyote. Kuulinda katiba, ni kitu muhimu sana.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante sana mzee Mwidadi kwa maoni yako. utatuachia copy? Kuna yeyote aliye na swali kwa Mzee Mwidadi? Ndio.

**Question**: Mzee Mwidadi umeongea kuhusu uvunjaji wa bunge. Kwa maoni yako haifai jukumu, ama uwezo wa kuvunja bunge, iwe ni ya Rais. Wewe ulikua unaonelea uwezo wa kuvunja bunge, uwe ni wa nani? Na ufanywe kivipi?

**Mwidadi**: Kufuatana na kifungu hamsini na tisa, cha Katiba ya sasa. Rais amepewa uwezo wa wa kuvunja bunge, na watu kwenda kea uchaguzi. Nimesema tena nguvu hizi kuachiwa mtu mmoja ni hatari. Mimi maoni yangu ni kua, wabunge wenyewe, ikiwa kutakua na motion-kama vile wakati wataka kuahirisha bunge-leader of the government business, hutoa pendekezo, kua bunge laweza liairishwe. Kwa hivyo mimi nilikua nafikiria hata kama ile process hivi sasa ni ndogo, lakini kuwe na process ambayo ianze kwa lile bunge. Wenyewe waweze ku-recommend, au kupendekeza kwa rais, lakini haya yaanze kwa lile bunge lenyewe. Maanake kitu ambacho kinatendeka sasa, ni kua sisi twawapa wabunge, nguvu hizi kwenda bungeni, lakini mkono huu wawapa nguvu, na mkono huu nguvu zile sisi twazichukua. Kwa hivyo tulikua twafikiria mambo haya ya kuahirisha bunge, mambo haya ya kuvunja bunge, liwachiwe bunge lenyewe: na ikiwa kutakua na time table, itakua hakuna matatizo, kwa sababu wabunge wenyewe wajua tarehe fulani bunge lahairishwa, tarehe fulani bunge la vunjwa. Kwa hivyo they can initiate, the recommendation or a motion can be raised in Parliament, and then they can even discuss it like any other motion. Then their recommendation will go to the president for his action. Thank you.

**Com. Pastor Ayonga**: Ni kusema Mzee Mwidadi kwamba, bunge liwe na programme. Time table ambaye inajulikana hapo mbele. Kwa maana tukianza kuwachia bunge kwamba watakuja kuona ni lini, katika programme hiyo itaharibu mambo. Mtu anaweza kua amesahau, ameendelea na mambo mengine. Programme ya bunge itengenezwe na iwekwe dhahiri, wazi kwa kila mtu. Asante. Sasa mzee unaweza kuja hapa ujiandikishe. Anayekufuata ni Joel Musango Ochieng. Ochieng unamaandishi, kwa hivyo anza kutoa maneno yako.

**Joel Misango Ochieng**: Asante sana. Kwa jina naitwa Joel Msango, mimi nimkaaji wa hapa Mombasa, Mikindani. Maoni yangu ni kuhusu Katiba iliotengezwa kuhusu koti ya hapa Kenya; Katiba iliotengenezwa kuhusu koti ya hapa Kenya; ni Katiba ambayo inaumiza Wakenya, na imewaumiza kwa mda mrefu sana. Sababu ya kusema hivyo; koti ya Kenya imepewa uwezo mkubwa ambao haiustaili. Ikiwa polisi anaweza kushika mtu leo kama saa mbili asubuhi, ikifika saa nane huyu mtu amefikishwa

kotini. Na mtu kufikishwa kotini, judge atakuuliza wewe umepatikana ukiwa unakojoa ovyo ovyo, na ukiwa utasema la, utapelekwa rumande kwa siku kumi na nne. Hiyo ni dhuluma kwa mwananchi yeyote, awe mkubwa awe mdogo. Kwa hivyo mimi ningeonelea ya kwamba koti za hapa Kenya zipunguziwe uwezo kama huo, ambao mtu akiwa ameshikwa aadamane na yule aliyemshika; waende wafanye kesi, akitoka hapo ajue yeye ni mfungwa ama sio mfungwa. Kwa hivyo sina mengi, ni hayo tu.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante Bwana Ochieng. Kuna yeyote aliye na swali kwa Ochieng? Ochieng unaweza kuja hapa ujiandikishe. Mwingine ni Alex Oluoch. William Onyango. He is in? Okay. Huyo ni William Onyango.

**William Onyango:** Asante sana. Mimi nitazungumzia kuhusu mambo ya ulemavu. Kwa sababu mimi mwenyewe ni mlemavu, na nimeona ni jaribu kuwakilisha wenzangu, ili yale maoni pia yatiliwe maanani. Sasa tukija kwa upande wa walemavu, nilikua na onelea kuwe na elimu ya bure kwa upande wa walemavu. Kwa sababu wengi wa walemavu, na wale wazazi walemavu; watoto wao hua wako manyumbani, na hawawezi kuwapeleka shuleni. Wakati ukijaribu kumfuata umuulize, anakuelezea kua, hana uwezo wowote. Kwa hivyo huyu mtoto atakaa nyumbani, mwisho akimaliza kua mkubwa, anamalizia barabarani kuomba pesa. Kama elimu ingekuwa ya bure kwa upande wake, sidhani kama ingekua ni rahisi yeye kwenda barabarani. Walemavu wale ambao wamepata elimu kidogo, hua ni vigumu kuwapata wameingia barabarani kuomba pesa. Lakini kwa wale ambao wameonja shule kidogo, hua mambo ni mazuri kwao. Kwa hivyo tulikua tunaomba, ikiwezekana hasa kwa upande wa walemavu Katiba ijaribu wapate elimu ya bure.

Jambo lingine, utakuta kua, kwa mfano kama hapa Mikindani, utakuta mitaro hua imewachwa wazi wazi, na hao ndugu zetu ambao hua hawawezi kuona, wanatumia zile fimbo za kutembea; kutembea kwao inakua ni ngumu. Ikiwa wanajaribu kutumia zile dectetor watatembea mara muda kidogo washaatumbikia mitaroni. Lakini mitaro kama ingekua imetengenezwa katika hali ambayo imezibwa, basi na wao wangeweza kufurahia kama wananchi wengine lakini kwa sasa hii imekua ni vigumu sana.

Jambo lingine; kuna ndugu zetu ambao hawana uwezo wa kusikia, sasa wakati wakiangalia television, hua ni vigumu sana, wao kufuatilizia ni kitu gani kinaendelea; lakini katika nchi zingine, unakuta pale kwa television hua kuna mtu fulani ambaye anainterpret angalau pia nao wafurahia. Lakini hizi TV zetu wakati mnaangalia mnafurahia, huyu mwingine anabakia anahuzinika. Kwa hivyo kama ingefunguliwa pia wao waweze kufurahia kama watu wengine, ingekua vizuri sana.

Wengi wa walemavu, hua wanaitwa majina, utakuta kiguru, kiwete sijui nani. Wale ambao wameonja elimu kidogo, yale matusi hua sio kitu kwao, kwa sababu wanasaidiwa na elimu. Lakini kwa mlemavu ambaye hajaenda shule, wakati ukimwita kiguru, kiwete, yeye kujitokeza pale ndani ya nyumba, itakua ni vigumu, kwa sababu anaogopa hilo jina. Na wengi wao, wakienda katika shule za watu wakawaida kusoma pia wakati wale wanafunzi wanawaita viguru na viwete pia hutokomea kabisa, wakawacha kusoma. Kwa hivyo kama wangepata kufungu cha kuwa-protect, ingekua ni jambo la maana sana.

Kuna hii hazima ya walemavu, ambapo walemavu hua wanajifaidi nayo. Kwa mapendekezo yangu, ingekua ni vizuri mlemavu mwenyewe, awe aki-control hiyo hazina. Badala ya kuchukuliwa mtu wa kawaida. Kwa sababu ikiwa mlemavu mwenyewe atakua pale; yeye yale machungu hua anayasikia. Kwa hivyo itakua ni rahisi yeye, kama ni ile kusaidia, itakua ni rahisi. Lakini kwa sasa imekua wengi walioko katika hiyo hazina wanaingiza kwa matumizi yao wenyewe.

Tukienda kwa hizi public schools, walemavu imekua ni vigumu; kwanza walemavu inatakikana wasome kama hao watu wa kawaida. Shule zichanganywe. Kuna shule zingine ukipeleka mwanafunzi mlemavu, wanasema mlemavu hakubaliwi kabisa, tafuta shule zingine. Hata kuna shule nyingine hapa hapa Mikindani, kuna mwanafunzi ashasoma mpaka darasa la nane, alipofika atakina afanye exam, akaambiwa wewe tafuta mahali, uende ukasome kwa sababu utaharibu ile mini – score. Ikabidi sasa sisi kama chama, tuende kwa ministry of education, ndio akasaidiwa. Kwa hivyo, wote wanatakikana wakubaliwe waingie katika shule za kawaida, na pia wasome kama wanafunzi wa kawaida. Kusiwe na ubaguzi kwa vile ni mlemavu ama si mlemavu.

Tukienda kwa upande wa mahosipitali, ulemavu na umaskini, ni kitu vinaandamana. Ukiambia mlemavu yeye aende kwa hosipitali alipe pesa pale, hua nikama ambao umemmaliza. Wengi wao hua utakuta akishidwa kwenda hosipitalini, anazidiwa, anakufa. Wengine wao wakiambiwa waende hosipitali na hawana pesa, wanachukua hiyo advantage wanaenda barabarani wanaanza. Wakati wakipata hiyo pesa pia wanazitumia kwa njia zao wenyewe. Sasa pendekezo langu, hosipitali kwa upande wa walemavu iwe bure, bila wao kutozwa chochote; kwa sababu ikiwa utamwambia atakikana naye atoe kitu kidogo, itakua ni ngumu.

Jambo lingine ni kwamba, walemavu pia ni watu ambao watakakufurahia kama nyinyi. Kwa hivyo kama unafanya kazi, pia mimi nataka nifanye kazi. Kama ni biashara, mimi pia nataka nifanye biashara. Kwa hivyo ningefurahia sana, kama mlemavu pia angepewa uhuru wa kufanya biashara, kama mtu wa kawaida. Ama kama ni kazi, inatakikana atengewe nafasi fulani ya kazi, serikali itenge, kwa mfano, kama inachukua watu kazi, even one percent sio mbaya kwa upande wa mlemavu, ili kuwatia moyo. Lakini ikiwa utasema kua hata mlemavu naye aanze kujitafutia, vile mtu wa kawaida anavyojitafutia, wengi wetu tukienda kwa hizi ma-interview hua hatuchukuliwe. Tunaabiwa kwa vile wewe ni mlemavu hutaweza, sasa unatupiliwa kando. Lakini ikiwa kuna kifungu fulani pale, kina lazimisha basi sisi tutafurahia kama hao wenzetu wengine.

Biashara-mimi mwenyewe hapa mimi ni mfanyi biashara, hivi majuzi, kulikua na ubomoaji wa vibanda mimi ni mmoja wa walio adhiriwa na mimi niko na bidii, na nina penda kufurahia kazi kama vile nyinyi mnavyo furahia. Hao walikua wakibomoa, ningefurahi sana wangenifuata wakaniambia, "wewe toka mahali fulani hapa, nenda hapa, "nikatae ndio wabomoe. Lakini kuja kuivunja vunja, bila kufikiria mimi kama mlemavu nitafanya nini. Hicho ni kitendo kimoja kibaya sana, tena cha imla. Nafikiri ingekua ni vizuri ningefatwa waniambie wewe Bwana, toka tumekupatia mahali fulani, singekataa. Sasa nina hakika wengi wa walemavu, na marafiki ambao nawajua, wamemalizikia barabarani saa hii. Wanaomba pesa, kwa sababu biashara yao

iliharibiwa; huku serikali inasema kua, inaondoa umaskini, badala yake inaongezea umaskini. Kwa hivyo sisi walemavu pia tuangaliwe kama watu wengine, tusiaciliwe hivi hivi.

Bwana Kamishena kwa upande wa walemavu, tuitengewe kiti kimoja kwa sababu sisi kuchaguliwa kwetu hua ni ngumu. lakini tukipata mwakilishi mmoja mlemavu, katika wale nominated councillors ama MP, basi tutafurahi; angalau naye atakua kama mwakilishi wetu pale mbele. Kwa hivyo nafikiri Bwana Kamishena anataka kuni-cut short, nina mambo mengi ya kuzungumza, kwa sababu nilikua nimejitayarisha vyakutosha.

**Com. Pastor Ayonga**: Ni kweli, lakini tuna watu wengi tungalipenda na wao wapate nafasi. Unaona tulianza jua likiwa kule, sasa mnaliona liko wapi? Upande huu, na sitaki yeyote atoke hapa bila yakupata nafasi.

**Joel:** Nashukuru sana Bwana Kamishena kwa kunipatia nafasi hii; nafikiri kwa mengi zaidi nitawasilisha memorandum yangu pale, na isije tukawa tunazungumza, halafu mwisho mchukue mwende mkatupilie kando. Sisi walemavu hatutaki tuongee juu ya kazi za serikali, muende mukazungumze, mukishamaliza kuzungumza, inatupiliwa kando. Nafikiri mmeona walemavu wachache sana, kwa sababu wamejua hutendeka hivyo. Kwa hivyo, wale wachache ambao tumekuja tukazungumza, jaribuni mambo yetu isije ikawa ni story tumekuja kupiga, na kupoteza wakati.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante, hebu ni kwambie maneno yote umesema yamenaswa na kanda; na yatachukuliwa kama maoni ya Mkenya yeyote. Na tena nataka ujue kwamba tutachukua maoni Kenya nzima, tumemaliza Central Province, wiki ijayo tutamaliza Coast Province, na kila pahali kuna walemavu. Tena nataka ujue, mimi kama Pastor nataka nikwambie hivi, kila mtu ni kiumbe cha Mwenyezi Mungu na Mungu anatupenda sisi sote; na lazima tutendeane, sisi kwa sisi, ule wema ambao ningependa nitendewe mimi mwenyewe. Bila ya madharau yeyote, bila ya unyama wowote, juu ya binadamu mwenzangu. Kwa hivyo haki lazima ionekane ikitendwa, maneno yako hayatatupwa hata kidogo; mimi naweza kusahau ulioyasema yote, kwa maana watu ni wengi, lakini kanda haisahau. Na Mungu akubariki. Unaweza kuja hapa ukajiandikisha.

Next, list yangu bado ni ndefu, kwa hivyo ningependa wale mnao kuja, mje ukiwa umeweka mawazo yako straight, mambo yako yote yawe tayari. Sasa ni Gideon Mutemi. Hayuko? George Odongo? Mbaraki Ali, basi baada ya huyu mzee, kaa hapa karibu. George Odongo unamaandishi ambayo utatupa? Kwa hivyo tafadhali sema point zako, na zile zingine ambazo wengine wameshasema tayari, wewe tumlikie maneno mapya ambayo unatakakuongeza, kwa Katiba.

**George Odongo**: To introduce my self, my names are George Odongo. I am giving my views in the capacity of a student leader, I am the secretay-general of the Mombasa Polytechinic Students Union; and these are the problems of the students. The demand for higher education in Kenya is high, and not all students who pass O-level exams; get university admission. I would recommend that all national colleges, and polytechnics should be awarded education loans, the same way university students get loans, through the higher education loans board.

Mombasa Polytechnic is offering certificate and diploma courses, in medical laboratory technology, and phamarcy, whose students are being examined by the Kenya National Examination Council, and yet the students cannot get industrial attachment in the government hospitals. So my main worry is this, the government has authorized the Mombasa Polytechnic to train students in medical lab. Technology and pharmacy, and the students are supposed to go for industrial attachment in government hospitals; yet they can not be allowed, simply because there are a click of people sitting in Nairobi headquarters, calling themselves board members. They have given the administrators of these hospital an authorities, instructions that any student of Mombasa Polytechnic, should not be given a chance for industrial attachment. I recommend that the Polytechnic students should be given equal opportunities, the same way their counte part in Kenya Medical Training colleges get these chances.

I recommend that a provision should be made in the new Constitution that makes it easy for a student, who has undertaken a certificate course, and wishes to get a degree to do so. In the current situation it is very difficult for someone who has a certificate course to go for a degree course, and I would recommend that a student who passes with a credit should be allowed to go in third year for a degree course, which takes four years.

My last point. The government should equip all the institutions of higher learning, with modern learning facilities e.g. you find that in Mombasa Polytechnic, the engineering students are taught using machines which are obsolete thereby it becomes difficult for these students to get employment. You find that when you go for attachment, or when you get employment, you are told that you have not been taught the required thing. I recommend that the government should equip all this institutions. And this point has been said over and over again, but I have to insist on it again.

Primary education should be made free and compulsory. I suggest that you commissioners, should at least find time, to come to these learning institutions so that you can collect views of the youth. Simply because, you can not find a child, who can come here infront of adults to speak their mind. So it would be adviseable that you go to the areas, other so that every view of Kenyans is collected.

**Com. Pastor Ayonga**: Thank you George Odongo. Let me ask you this George before you leave, did I here you say that the students at Mombasa Polytechnic, who take courses in Phamarcy and Medical Laboratory technology, are denied opportunity to work in government hospitals? What would be the reason?

**George:** What we are being told is that the Polytechnic has no facilities to offer these kind training; but I believe that it is the government which has authorized the polytechnic to train students on these courses. So it would be better, if the Polytechnic has no facilities, then it should not be allowed to train students in these courses in the first place. Otherwise we think that we should get equal opportunities.

**Com. Pastor Ayonga**: Yes, that is something one would worry about. The polytechnic is allowed to train, and then the trainees after they complete their course are told you do not have the facilities. Why should you have wasted your three years. Then what happens to your students, where do they go?

**George**: If you are lucky enough you can get employment in private sector, or in the vibandas which are operating here within.

**Com. Pastor Ayonga**: Thank you George. Now you can come here and register your name. Huyo ni mzee Mbarak Ali. Endelea.

**Mbarak Ali:** Mimi kwa jina, ni Mbarak Ali, kutoka kijini cha Jomvu. Na nimefurahi sana kufika katika Tume hii ya marekebisho ya katiba. Kwanza nitaaanza na mahakama. Mahakama ninayoanzia ni mahakama za Kadhi. Mimi nilikua naomba, au nafikiria kua, huyu chief Kadhi awe anauwezo kama Judge mkuu, kwa waislamu. Na pili masharti awe ana shaada za sheria za Kislamu. Tatu; katika maimamu, wawe na uwezo kuchagua chifu kadhi, na makadhi, waende kwa mtihani.

Jambo lingine ni katika kuchagua wabunge au madiwani. Katika kugombea uchaguzi wa ubunge au udiwani, kwanza awe ni mwanati wa pale. Na mgombea uchaguzi huyu, akiwa ni mwanati wa pale; amesimama akashidwa mara mbili, basi asiwe na haja kupewa nafasi yakupigania tena. Mgombea urais, mbunge au udiwani akigombea awami mbili, bila kufaulu asiruhusiwe tena kusimama. Tatu; tumekubali kiwango cha pesa kiongezwe na Tume ya uchaguzi. Hapo nitafafanua bila shaka, yaani kuna kitu ambacho kinafanyisha kutoa kama ushawishi watu kupigania uchaguzi, lakini kiwango kilichoko chaweza kua ni kidogo; kipandishwe, na usimamizi wakuangalia kiwango hichi, tume ya uchaguzi iwe ikiangalia.

Na tatu; katika Makamishena wale ambao watachaguliwa, either awe ni Kamishena wa marekebisho ya Katiba, awe ni Kamishena wakuangalia mishahara, awe ni Kamishena wa kuangalia ardhi, au awe atatumika kwa mda wa miaka mitano tu. Akimaliza hapo, kamishena achaguliwe mwingine kushika hizo nafasi.

Kuhusu ardhi; jamii ya mahali pale, iruhusiwe kumiliki ardhi mahali pale. Kumiliki ardhi kiwe na kiwango maalumu, kama eka mia moja. Kuna baadhi ya watu, katika Kenya hii, wana eka elfu ishirini. Kuwe na kanuni; ikiwa si raia apewe plot ikiwa atastawishwa kiwanja. Kwa mfano, amekuja Baniani, lakini amekuja asema hapa mimi nataka kujenga kiwanja cha kutengeneza nguo. Si raia lakini ataka kustawisha na tutapata mahali tuandike watu wetu hapo. Iangaliwe, apatiwe hiyo plot, ajenge hicho kiwanda ili kuendeleza wananchi wa pale.

La mwisho kwangu kwa Bwana Kamishena. Uwakilishi bunge au udiwani, ugombaniwe na mwananchi peke yake. Uajiri wa kazi, uwe wa asilimia sabini na tano, wa pale. Ufisasdi: yeyote ashikwaye na ufisadi afilisiwe. Twataka serikali ya Majimbo na 75% ya pato litumikie Jimbo lile, na 25% iende serikali kuu. Ni hayo tu Bwana Kamishena kwa sasa.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante sana mzee Ali. Utatupatia maandishi?

**Ali:** Nitaangalia.

**Com. Pastor Ayonga**: Utaangalia tena lini mzee? Ulikua unaswali kwake? Mzee unataka kuulizwa swali?

**Question**: Bwana, umesema wale wenye kusimamia uchaguzi, waangalie kiwango cha kufanya mambo ya kura kisifichwe. Unafikiri kitaweza kusimamiwa namna gani, na hicho kiwango ki mfukoni mwa mtu?

**Ali:** Na fikiri ili si jambo geni. Ni Jambo ambalo ukiangalia sheria za kura zitakwambia, mbunge au councillor asitumie kiasi ya zaidi ya pesa hizi. Twataka kuuliza wewe, unahakika kwamba kiwango anachotumia hakifiki pale?

**Com. Pastor Ayonga**: Asante. Atakaye fuata ni Omar Hassan, na Nyundo Joto awe karibu. Omar Hassani. Umaandishi? Unayo, kwa hivyo utumlikie yale makubwa makubwa, na nimekupa dakika tano.

**Com. Salome**: Fatuma Yusuf kama yuko hapa na ako tayari. Hayuko. Na Fatuma Salimu Adhumani, Zubeda Suba, Zubeda ulituzungumzia jana wataka kutuanzia leo.

**Zubeda:** Ndio.

**Com. Salome**: Lakini umejiandikisha kua ungetaka kuzungumza? Margaret Mbaya. Judy. Okay, Binti Mariam Tawe. Hajafika? Tamauya, haijaandikwa vizuri. Siwewe Tamauya. Wewe ni nani. Watakakuzungumza hapa, ama kule. Basi nenda kule. Haraka Muhidari. Mary Kenia. Ndende Rekia. Sidi Chake. Katura Hamed. Rehema Munyasya. Ni wewe basi tuanzie nawe. Waandishi wa habari wakiume wakija mtaona shida.

**Interjection**: Hawana neno.

**Com. Salome**: Basi njoo, na ukae nyuma.

**Afusa Kibwana**: Jina langu kamili Afusa Shamaua KiBwana. Kuchangia hii Katiba, tunajiuliza kama sisi ni wazaliwa wa hapa Pwani? Tumekaa mababu wa mababu wa babu tukitia fahamu, twajiona tuko hapa hapa, baadaye tunaitwa ma-squatter. Ma-squatter sisi hatuna kibali, twaweza kwambiwa wakati wowote kuja kwambiwa, ondoka hapa si pako, na mtu kama wewe umezaliwe pale. Sasa utakwenda wapi? Kama sisi waislamu. Waislamu sisi, sheria zetu zinatokamana na Chief Kadhi. Chief Kadhi yule huzileta kutokamana na chief Kadhi uradhi wetu unatokomana na Chief Kadhi, mambo yetu yote, yatokomana na

Chief Kadhi. Lakini Chief Kadhi yule hana uwezo. Yakua wewe utakua na sheria zako, waenda kusema ka Chief Kadhi, hua sitasikizwa ki sawa sawa; na pengine upate uhaki, pengine upate bafriji. Tunaomba, uradhi wetu urudi kama vile zamani. Maanake zamani, uradhi wako ulikua ukitokomana na Chief Kadhi, ukapawa kile kilichochako. Ambacho unatakikana upate. Lakini sasa vilivyo, hivyo utambiwa uende kwa Kabila liwasii, ukifika kwa Kabila liwasii, sheria iliyeko hino, ya kikwetu na kikwao ni tofauti kubwa sana.

**Fatuma Ahamed**: Jina langu ni Fatuma Ahamed, nilikua mimi nafikiri ni maswali. nilikua nauliza, katika hiyo kiti ya udiwani, ikiwa pengine mtu anataka kuchaguliwa; nilisikia kwenye Katiba hii, kizungumziwa, mpaka mtu awe amefika form four. Sasa je ikiwa mtu hakufika form four, na wale wa pale mtaani wampenda yeye sana, je? yawezekana huyu kupigania u-councillor ama ni vipi? Ama mpaka awe amefika hiyo form four.

**Com. Salome**: Hii Katiba tutakayoiandika sasa, mpaka mtu awe ametoa maoni yake. Wewe maoni yako ni nini? Bi Ahamed.

**Bi. Ahamed**: Mimi maoni yangu, nilikua nataka mtu awe bora wale wa kijiji chake wampenda; awe atachaguliwa, hata kama hajui kusoma. Awe amesoma kidogo, lakini pia achaguliwe. Hata kama hakufika pale form four.

**Com. Salome**: Kuna mtu mwingine mwenye jambo angetaka kuchangia?

**Beatrice Mbithi**: Ningependa kujua, kama katika Katiba, kuna chochote kilikua kimepitishwa juu ya retrenchment?

**Salome**: Hakuna.

**Beatrice:** Kwa hivyo maoni yangu nilikua naonelea, wakati wa retrenchment, serikali ingeangalia wenye watakua retrenched; badala ya kutoa wale walioandikwa nyuma wakawacha wazee, wakaangalia kazi ya mtu vile anavyo fanya, ndio retrenchment ikafanywa. Kuliko kuondoa vijana, halafu wanawacha wazee ambao wamekaa kazi ni muda mrefu; washasomesha watoto wao wakamaliza, wakatafuata mali, sasa kijana ambaye ndie ameanza, anakua hawezi kujisaidia.

**Com. Salome**: Sasa umeamuaje wazee waende vijana wabaki?

**Beatrice:** Wazee waende kwa sababu yeye ametafutia jamaa zake, na wameenda mpaka kiwango Fulani, ambacho wanaweza kujitegemea.

**Com. Salome**: Unataka je? Unaweza kupata mtu ni kijana na hana bidii, na mtu ni mzee lakini ona bidii, sasa unasema wazee waende, tutumie umri?

**Beatrice:** Wazee waende vijana wabaki. Hapo ndio bidii sasa itaangaliwa.

**Com. Salome**: Mtu mwingine yeyote?

**Mary Kamene**: Kwa jina naitwa Mary Kamene, na nachangia upande wa kina mama. Akina mama saa zingine wanashida ndani ya nyumba; unaweza kosewa na Bwana, ama ukapigwa. Ukifika kwa Chief ama ukienda Changamwe badala aende akajue ni kitu gani kimefanya ufike pale, anakwambia nenda urudi; ama nenda mkaelewane na Bwanako, na pengine pale umewacha umesimamiwa na kisu. Ukienda Changamwe anakwambia, "wewe akina mama mnasubua, nendeni mkaelewane, "saa zingine anakwambia, "umemnyima", sasa hiyo hua haitupatii raha moyoni mwetu. Nikumia tunaumia, unarudi lakini roho iko hawa. Hakuna usaidizi mwingine sababu ushaasukumwa unaambiwa, "ulimnyima", hiyo inakua si vizuri, inatakikana serikali ituangalie sana. Waume wanatunyanyasa.

**Com. Salome**: Ungetaka kuangaliwa vipi? hebu jaribu kufikiria ni jambo gani linaweza kuwekwa katika Katiba, likajaribu kusaidia.

**Mary:** Ningependa hata kama ni kwenye serikali, kama pale Changamwe sasa, panawekwa mama, ambaye atatusikiza maoni yetu. Kwa sababu mama atasaidia maoni yake, sababu yeye pia ana mume ndani ya nyumba, atatuelewa. Huyu pengine amefukuzwa kama mimi. Atajua vile atakavyoyapeleka, na vile atakavyorejesha. Pia kwa Chief, Chief pia hata kama yuko mme pawe mke; wawe wawili wawili pale, mme na mke Nikienda pale namwambia mwenzagu, "wajua kulikua hivi na hivi," ananielewa urahisi kwa sababu yeye ana nyumba yake pia, anajua vile atanifunza, pengine mimi ndiye nina makosa, ama Bwana ndiye mwenye makosa; atajua vile atakavyo ni direct. Lakini akiwa ni waume, kwa waume wafukuzwa, ningetaka wachanganwywe. Kama ni Mikindani, mme na mke, Changamwe mme na mke, polisi na machief wazee wote wachanganywe. Tuwe mama yuko ndani, kwa sababu sisi wakina mama ndio tunapata shida sana. Asante.

**Com. Salome**: Hakuna mtu mwingine ana jambo lingine la kuchangia?

**Nini Kibwana**: Jina naitwa Nini Kibwana, sijui kama yangu ni maoni, lakini kwa upande wa elimu; utakuta mwalimu ambaye anabidii ambapo ile skuli inapita kweli kweli. Mwalimu kama yule aambiwa aondelewe katika ile skuli, apelekwa mahali pengine. Katika kule mahali anapokwenda, ni ugenini, na pia ile kazi ambayo alikua akifanya huko mwanzo hua nikama ambaye amevunjika moyo. Sasa kule kutakua hakuna chochote kinachoendelea, na huku alikotoka pia utakuta, skuli kama haiendelea tena. Sasa pale ni masikitiko, kwani yule akiwachwa pale angeendeleza vizuri. Huu ujinga ni kwa hatusomi tukawa juu; kwa sababu ya wale waalimu kubadilishwa, yule mwenye bidii anaondolewa, tunaletewa mwingine, pengine amepelekwa nchi isio ya kwao, anasema ahachana. Napendekeza wale waalimu ambao wanabidii, wangaliwe wawachwe, maanake kwa mfano, mwembe unazaa maembe mengi; sasa huwezi kuuambia ule mwembe ukiukata yale maembe nadhani yataacha kua mengi. Kwa hivyo yule mwalimu angeachwa, ndio tungeinuka pia tukawa juu.

Fatuma Ahmed: Nikiongezea vile huyu mama alivyosema, ni kweli. Huko polisi hua wanawake twanyanyaswa sana pengine umekwenda umesema kua, you have been raped, "eh ukweli lakini? Umekuwa raped kweli? Wewe malaya wewe, wee sijui nini". Kwa hivyo, hiyo ni sana hiyo mambo yako hasa hapa polisi. Kwa hivyo, ingekua kama vile ambapo twasema Rais awe mwanamme, na mdogo wake awe mwanake na pale polisi iwe hivyo hivyo. OCS akiwa mwanamme chini yake awe mwanamke. Hiyo iwekwe awe mawanamke, maanake aweze kututea pale. Hua watunyanyasa sana pale upande wa polisi. Hiyo ni kweli kabisa.

**Com. Salome**: Kuna mtu mwingine amebaki?

**Margaret Mbaya**: Nanishaongea kule Chandaria, lakini haya, ni maoni yangu mengine, ambayo marafiki na majirani pia wamenituma. Sisi wanawake tuwe na umri mdogo wa kufanya kazi, kama 35 years hivi, ili tuwapishe hawa wasichana wetu, wapate kazi, kuliko sisi sasa kuendelea. Halafu vile ambavyo tutalipwa, tulipwe mpaka ile 55 years. Hilo ni pendekezo la wana mama pale mtaani. Halafu na maBwana nao, wapate 45 years, ili wa wapishe vijana wao, nao wapate kazi. Maanake wanapiga mlami sana hapa, na wazee nao washakula vyakutosha. Maoni yangu ni hayo. Asante.

**Com. Salome**: Nina swali mama wa 35 years, ikiwa alisoma mpaka akapata shahada ya masters, kitambo aanze familia yake, atakuwa amesoma ana umri wa miaka 28. Sasa awache kazi akiwa na miaka 35?. Ndio unasikia tunataka maoni ya wazee, tunataka ya vijana, tunataka ya kila mtu. Kwa hivyo saa zingine unaweza kutoa maoni mengine ukifikiria yatasaidia, lakini waiona tu kutoka kwa upande wako. Kumbe kwa upande yule mwingine, inaweza kumuweka mwingine mashakani. Sisemi hiyo sitaichukua nimeshaichukua lakini wakati wa Katiba, ni wakati wa kufikiria pamoja na kuangalia mambo Fulani yakifanywa yatakua na madhara gani kwa yule mwingine?

Basi kama hamna mwingine ningetaka kuwashukuru sana kwa hii habari ya kufikiria tukawa na hiki kikao; kwani tumeshasikia kina mama wengi, mimi mwenyewe kwanza nimekua na hofu kubwa ya kusikia hatusikii matakwa ya kina mama. Kama hayo mambo ambayo mmeleta; mambo ya watoto kutungwa mimba, mambo ya kubakwa, mambo ya kupigwa nyumbani. Haya mambo hayazungumzwi wakati tumekutana mkutano wa dharura. Yana kosa kuja, lakini kina mama wasipopata nafasi ya kuyalete kwenye katiba ya wakati huu, tutangoja miaka ingine hamsini, ama mia moja ndio ifanywe. Kwa hivyo nashukuru sana, kua mlikua na ushujaa wa kuja pamoja ili tuweze kuwasiliana akina mama tukiwa pamoja. Tukayaleta hayo ambayo kwetu ni makubwa, na hayaeleweki na watu wote walioko pale. Shukrani.

**Interjection:** Napendekeza wamama wakienda nyumbani, wakawaambie wenzao waje saa nane kesho, waje kwa wingi. Na ikiwezekana sijui wanataka saa gani nzuri, wapeane maoni yao. Saa nane sawa akina mama?

**Salome:** Wakitaka kuja, wakitaka kikao cha pekee, basi niko hapa na muwaambie wa mama wenye ulemavu waje pia, kuna

mama mwenzao mlemamavu, na yuko tayari kuwasikiza. Kwa hivyo ninataka kuwashukuru sana, na kuwaambia tafadhali fikishenikina mama wengine wengi tusikie maoni. Kwani wakati wa Katiba hauji tena kwa muda mrefu kweli. Naningetaka kuwashukuru wafanyi kazi wa Tume ya mageuzi ya Katiba wenye wamekuja haraka haraka kwenye kikao hiki, ndio tuweze kusikika na kusikizana; asanteni sana kwa kazi nzuri. Na sasa ningetaka kukiitangaza kikao cha Tume ya marekebisho ya Katiba, kikao maalum cha kusikia maoni ya akina mama, kutoka kikao cha ubunge cha Changamwe, kua kimeisha; asanteni na Mungu awabariki. Kama kuna mtu angetufungia na maombi, kina mama ni watu wa kupenda kuomba.

**Zubeda:** Kwa jina la Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema mwenye kurehemu tunakushukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwatia moyo wanawake hawa wakaja hapa, wakatoa maoni yao, na twakuomba Mwenyezi Mungu uwajalie uwatie hima, kesho wafike kule, watoe maoni yao, kwa roho zao takatifu. The rest in Arabic.

**Fatuma Ahmed:** Msichana akipata mimba, twataka huyu msichana amuoe. Na akiwa hatamuoa, basi amtumikie huyu mtoto amuhudumie mpaka awe mtoto mkubwa wakupata kazi.

Na naomba kama ikiwezekana hii Ijumaa iwe kama vile ambavyo ni Jumapili. Yaani watu wapewe ruhusa ya kwenda msikitini, watoto wapewe ruhusa waende misikitini. Hii siku ikishafika saa sita, watu wapewa ruhusa waende msikitini wakaswali, na pia katika maradio, iwe kama vile Jumapili, kwa vile kuna hii mambo ya Pwani iwe yazungumzia mambo ya dini siku ile yote. Tukianzia pale wakati wa kuswali tu, basi iwe yazungumzia mambo ya dini siku hiyo yote, maanake ni siku njema.

Jambo lingine pia naomba, Katiba hii iangalie mambo ya sikukuu. Katika sikukuu hii ya Kislamu kweli hua watu wapewa ruhusa, lakini wapewa kimakosa. Maanake ile siku ya sikukuu haswa hampewi ruhusa. Mwangoja mpaka siku ya pili ndio public holiday. Sasa sikukuu ishakwisha, ndio yaja yapewa public tena ambapo sikukuu ishakwisha. Sasa twataka, siku ile ile ambayo mwezi inaandama, nayeye Chief Kadhi naye aseme kweli mwezi waandama, iwe hiyo hiyo sikukuu isiwe watu wataka kwenda swali halafu kisha warudi makazini. Iwe ni sikukuu na itiwe maanani ni sikukuu tu; isiwekwe ati ni public holiday, siku nyingine ile ya sikukuu iwe ni sikukuu.

Na katika viongozi: sisi tumepewa viongozi wanawake, waambiwa ni viongozi wa kina mama, wewe wajulikana kila pahali, wewe ni kiongozi. Lakini serikalini hujulikani, maanake hupewi chochote. Hujulikani, wa enda tu, ikiwa ni wakati wa kura watumiwa huna malipo yeyote. Kwa hivyo twataka, kama ni kiongozi amechaguliwa ni kiongozi wa kinamama, kiongozi yeyote uwe una malipo Fulani, ya kuingia moyo angaa. Lakini wewe wenda tu, miaka mitano, watumika hivi na hivi, ukija nyumbani, watoto walala na njaa. Huna namna ya kufanya, wewe waitwa ni kiongozi waalikwa harambee wewe, wambiwa ndio mgeni wa heshima, utakwenda toa nini, wewe mwenyewe huna chochote. Kwa hivyo kiongozi lazima naye angaliwe katika serikali, ajulikane huyu ni kiongozi, apate malipo yeyote nayeye. Naona nimemaliza.

**Maki Mwandeshi**: Mimi naitwa Maki Mwandeshi, swali langu ilikua ni ufanuzi zaidi kuhusu, mwanamme anapomweka

msichana mimba, alee mtoto mpaka umri gani?

**Speaker**: Kufikia miaka kumi na minane.

**Maki Mwandeshi**: Na hii pension ambayo umeizungumzia hapa nyuma, tunajua kwamba ni ya miaka mitano, lakini umependekeza iwe mpaka miaka kumi na minane. Je? Mme atafariki wakati watoto wote wamevuka miaka kumi na minane.

**Fatuma Ahmed:** Asaidiwa yule mama mpaka kufa kwake nayeye.

**Maki Mwandeshi**: Ndio hapo nilikua nataka ufafanuzi zaidi.

**Com. Salome**: Ninaswali moja kwako mama mvulana akipata mtoto na msichana, amulee mpaka miaka kumi na nane. Siku hizi watoto wetu wa miaka ishirini na sita bado wako nyumbani, wanatafuta kazi. Bado unampa chakula, bado unampa pahali ya kulala, sasa wewe bado umemwachia mpaka miaka kumi na nane, halafu ikiwa huyu mtoto wake hajapata kazi, itakua mzigo wanani akisha fika miaka kumi na nane.

**Fatuma Ahmed**: Atajishughulikia hivyo tu. Kama ni wakuolewa ataolewa. Kama ni kusoma amemaliza kabisa, amepata kazi, ajue sasa ajitengemea mwenyewe.

**Com. Salome**: Asante sana mama, kwa maoni yako. Wewe ni mama Fatuma Ahamed. Okay asante kwa maoni yako. Nani mwingine yuko tayari kutoa maoni yake? Unaitwa nani? Nini KiBwana. Basi endelea mama Nini.

**Nini Kibwana**: Jina langu naitwa Nini KiBwana. Maombi yangu ni kuhusu kwa upande wa kazi. Utaona mtu ambaye yuko juu yako, yuwafanya kazi kwa bidii, kwa kua yeye ana masomo ya juu. Na wewe ambaye wafanya kazi kwa bidii zote kulingana na elimu yako, ni haki na pengine uko na hamu na ujuzi wa ile kazi. Kwa vile masomo yako ni ya chini, hua hufahia kwani watu wale hawaendelezwi wakawa kama vile wengine walivyo. Swali langu la kwanza lishakwisha.

La pili, ni kuhusu habari ya watoto ambao wafanya kazi majumbani. Huona shida nyingi, maana ikiwa mtoto yule ni wa kike hua na shida mle nyumbani, yule baba ambaye ni tajiri wake humlazimisha kua wafanye mapenzi,

kama vile wanavyofanya na bibi yake. Na kisha hapo hapo katika ile nyumba, pengine kuna mtoto wa kiume, ni mkubwa ambaye aweza pia kupata bibi. Sasa mtoto yule mfanya kazi, utamkuta baba yu wa mwendesha, na yule mtoto yu wa mwendesha. Hapo hapo yule mtoto apata mimba akisha pata mimba, mwishowe yule tajiri humwambia nenda zako; hua hakuchukuliwi hatua yeyote kuhusu ile mimba. Akifika kule kwao, je? mama mbona hii mimba umeipata, umeipata wapi? Akiletwa pale yule tajiri humwambia aa sisi mimi, na akisema ni wewe baba, na huyu mtoto wako, hua hachukuliwe chochote. Huambiwa aha, wewe nenda zako. Kwa maoni yangu hata kama ile mimba ametiwa na baba, ameitiwa

na yule mtoto, mimi ningeona yule mtoto na babake wakamwangalia yule mtoto, mpaka atakapo zaliwa na kisha kama ingekua yawezekana, akatafutiwa njia ya masomo akasoma. Na pia wale wanaowandika watoto wakike, ni maoni yangu, kwa nini kama wako yuwasoma, na yule wa mwenzio hasomi, huwezi kuona vibaya kama hivi vimetolewa skuli za adults zile. Yule mtoto yule badala akufanyie kazi, pengine shida ya mzazi wake alikua hana pesa za kumsomesha, ningeomba akufanyie kazi, lakini umpeleke shule umchukue kama mtoto wako, na kisha wale wanaofanya vitendo hivi, hatua zichukulie kali juu yao. Yangu ni hayo.

**Com. Salome**: Kuna swali kwa mama Nini?

**Question:** Katika ufanyaji kazi, utaona mtu ambaye yuko juu, ningeomba Katiba iangalie wanyonge, ambao walisoma wakashindwa hadi vidato vya juu; watengewe skuli wao waende wakasome. Katika kazi utaona mtu ambaye yuko juu yako, hafanyi kazi kwa bidii, wewe una ujuzi wa kazi, lakini kulingana na masomo yako ni ya chini, hua wafanya kazi kwa bidii, lakini hutambulikani kama wewe waifanya ile kazi. Kwa maoni yangu, ingekua ile kazi nikafundishwe, na mimi yale masomo ni yapate yafanane kama vile yule mwingine. Kwa hivyo kama kuoneana. Pengine mimi nafanya kazi kwa bidii zote, lakini masoma yangu hayaniruhusu ni ya chini, ndio sasa mimi ndiokilio ninacholilia wale wenye masomo ya chini. Watengewe mahali wasomeshwe, nao wafike kama ni Certificate za form four, nawao wapate. Hicho ndicho kilio changu kwa wafanyaji kazi.

**Com. Salome**: Asante. Mwingine.

**Mwanabibi Mwikaa**: Mimi natetea umaskini. Unyonge huu ni wa hapa tuishiko. Na wenzangu wa serikali, na mji ule na mababu na mababu. Lakini sasa ambazo ni wa serikali twaambiwa tuondoke. Tutaondoka pale twende wapi? Na watoto ndio hao wa kisoma kazi hawapati. Tukienda kwa hao tulioweka mbele, wakwambia bado, bado, kama twataka kwenda tafuta mji, tuteme mwitu. Basi matatizo hayo pia twataka mtutee na nyinyi. Hii ndio Katiba.

**Com. Salome**: Kwa mapendekezo yako, ungependa mfanyiwe jambo lipi? Kwa kuona kwako unaona Katiba ingemtetea vipi?

**Mwanabibi**: Katiba mimi nataka kazi. Kazi watoto hawana, watoto waharibika. Kisha wambiwa watoto wafanya maasia mabaya, kazi hawana. Je watoto wale hawana kazi, si wataiba? Maanake ikiwa mtoto hana kazi, hana cha kufanya. Je itakua ni vizuri vile? Twalilia kazi.

Nyingine twatetea maisha yetu pale mjini. Twataka Katiba itutetea mtufanyie ule mji wetu tuketi. Kwa sababu tuko taabuni, twambiwa tulipe, kulipa malipo hatuna kitu, watoto hawana kazi, tutalipa nini? Tulipe ardhi na nyumba. Tumpeleka mapeni kidogo, twadikwa magazetini kua tumeiba. Basi serikali inabidi itizame kile kijiji chetu. Na watoto wapate kazi na, sisi mamazao agao tutuemeno. Yangu mimi si mengi.

**Question:** Mimi nataka kuuliza saa zile wanaambiwa walipe magazeti?

**Mwanabibi:** Ndio magazeti tulipe.

**Com. Salome**: Hiyo ndio kusema nini mama?

**Mwanabibi:** Na tulipe na ikiwa hujalipa unatolewa kwa magazeti, eti wewe maskini.

**Com. Salome**: Majina hayo yameandikwa kwa magazeti watu walipe au vipi?

**Mwanabidi**: Sasa ndio hapo hatuelewi, tulisoma tu.

**Fatuma Mwinyi**: Jina langu Fatuma Mwinyi, mimi maoni yangu nikuhusu upande wa biashara. Kama wafanyi biashara wadogo ambaoa hawana uwezo, lakini mtu hawezi kukaa bure; maanake hajui unga atautoa wapi. Hana kazi, hana Bwana, kama sisi kina mama saa zingine, Bwana amefariki, amekuachia watoto, hujapata Bwana mwingine, na haukuajiriwa kazi. Sasa uwezo pia wa biashara kubwa hauna; uwezo wako ni kibiashara kidogo umefungua tu, kama mlangoni kwako hivi, ama umetoka nje, unaona mlangoni kwako hupati wateja, unaenda kama baraza fulani hivi, ukae ile biashara yako uze uze angalau mpaka njioni, wapata chakula; wewe na wale watoto. Hakikutoshelezi, lakini ni kule kuhangaika. Sasa tunaomba serikali kama biashara ndogo ndogo kama hizo, utaona mara unakimbizwa mbio na municipal, mara unakimbizwa mbio, sasa mtu kama huyu akikimbizwa mbio, asipo fanya hicho kibiashara, wale watoto atawalisha na nini?

Watoto pia wataka kusoma, sasa kwa hivyo twaomba serikali, kama ni license ingalie zile biashara kubwa, na wale ambao ni watu wamejipanua ki biashara au ni sawa watoe licence. Lakini kama watu wadogo wadogo, ambao huwezo hawana, mtu anajaribu tu ile kutafuta ile riziki, mtu kama huyu aachwe free, ajitafutie; maanake ile biashara yenyewe pia inaonekana. Kama umetoa silingi mia tatu, unanunua kile kitu,1 unauza angalau mpaka jioni upate kama mia tatu na hamsini; ile hamsini ndio unajaribu ukapate angalau kiunga kidogo, na sukuma, usukumie wale watoto. Ile mia tatu urudishe kwa mali, leo municipal imekuja kuichukua ile mia tatu, yote wamekukimbiza na wameichukua, mtu kama huyo utafanya nini. Utakua watoto wapata shida, wewe mama unapata shida, hujui sasa ukaibe sijui ukafanye nini. Basi naomba serikali, watu wadogo wadogo kama hivyo wafikiriwe. Muncipal isishughulike kuwakimbiza watu kama hawa, maanake hua ni maskini, lakini hawataki kwenda barabarani kuomba. Wanantaka watoe jasho lao, ndio wapate hicho kitu kidogo. Mtu anaona aibu kwenda kukaa barabarani, anyoshe mkono, aombe ombe. Lakini uwezo hana, anajisaidia na ile biashara ndogo. Huku municipal wanakuja wanawakimbiza. Kwa hivyo serikali pia, ifikirie watu kama wao; kazi hawana, biashara hawana, watafanya nini, na watakula nini? Ndio hapo uhalifu usije ukazidi kuongezeka. Hilo ni jambo la kwanza.

La pili, naomba hiyo Katiba pia ifikirie sana kuhusu hao watoto wanaitwa machokora. Hao watoto machokora hua wanazunguka mitaani; wengi wao ni hizo shida tunazosema. Majumbani, watoto kama wale saa nyingine hua hakuna chakula, watoto wanazungukazunguka. Ama wazazi wao wameshindwa na yale malezi wakakimbia wale watoto. Watoto wanazunguka, na tena wamekua wengi. Tangu tuliposikia machokora, tulikua tukisema ni urongo, mpaka huku kwetu sasa, wamekua tunawaona, tunahakikisha kwamba ni kweli; na wanazidi kua wengi. Sasa wakiaciliwa hivyo kuzungukazunguka na wale machokora wanakua wengi, hao hao ndio baadaye wakikua wakubwa, ndio wanakuja kua majambazi. Serikali ifikirie watoto kama hao, waweze kuwajengea mahali, vituo vituo kila sehemu, watoto kama hao wawe wanachukuliwa, wanakwenda wekwa wanapewa msaada wa chakula na malezi; kufundishwa kazi. Mtoto kama yule anarekebishwa tabia, akiwa mkubwa anaweza akili yake ikawa inajua mimi nilifundishwa kazi hii, na ninakwenda fanya, anajisaidia. Hapo twaweza kupata sehemu tukaokoa maisha ya wale watoto, na maisha ya sisi pia, ambao hatuna wale watoto. Maanake hiyo ni hasara kwa watoto na hata sisi ambao hatuna wale watoto, baadaye watakuja kutushika koo, watakuja kututia kabari, na uhalifu utazidi kua mwingi, katika nchi yetu. Kwa hayo machache nasema asanteni.

**Com. Salome**: Kuna mtu mwenye swali kwa mama? Mimi ninaswali moja. Wale watoto mitaani wakati huu, ni vizuri, na naona kua serikali inaweza kufanya mipango ya kuwasaidia. Lakini kinga ni nini, watoto wasiende mitaani? Kwani serikali haiwezi kua nangoja tuwache. Lakini wenye kuwaleta wanaendelea kuleta watu wanazidi inavyozidi kua wengi wanaendelea kuleta wengi zaidi mitaani. Waona kama kinga ni kitu gani, ndio watoto wasiendelee kuja mitaani?

**Fatuma Mwinyi**: Kinga ni hiyo serikali ikisha jenga vile vituo pale mitaani; pia kutakua kuchaguliwe kamati. Kamati itajua kua hao watoto wanafanya hivi, kwa sababu kuna shida kadhaa na kadhaa. Maanake pale mitaani, kila mtaa lazima inajulikana mtoto huyu anafanya hivi, kwa sababu hii na hii. Sasa yule mtu akishathibitisha kwamba huyu mtoto anafanya hivi; kweli nyumbani kwao kuna shida, ama kwao hakuna shida ni uhalifu tu. Lakini kuna watu kweli ambao kwao wanashida, sasa tunachagua vikamati katika mitaa.

**Com. Salome**: Asante sana. Nani mwingine anataka kuzungumza. Karimi si ulishaenda kwa vijana, kumefanyika nini tena? Hebu ngonja mwenzangu azungumze kwanza.

**Pamela Atieno**: Kwa majina naitwa Pamela Atieno. Na mimi ni mlemavu. Mwanzo ningependa kuongea ya kua, walemavu wawe wanasoma bure. Wapate elimu ya bure. Maanake, vile elimu ni ya pesa, unakuta wengi wa walemavu wanafichwa manyumbani: maanake wanaona ni mtu ambaye hata si wa kawaida.

Ya pili, ningependa mimi walemavu wawe mchanganyiko wale watoto ambao sio walemavu. Maanake wakiwekwa peke yao, wakikutana mahali kama hapa, hawawezi wakazungumza maanake wanaona uoga; kwa kua walikua wamezoena walemavu tupu, sasa wakiwa kama sisi hivi hawawezi wakaongea.

Walemavu nao wapate wanaume kama watu wengine. Maanake unakuta mwanaume anaweza kupatia mlemavu mimba, na anamtupilia mbali, anasema sasa huyu ni mtu wakuchukuliwa. Saa zingine una sura nzuri lakini kwa kua wewe ni mlemavu unatupiliwa mbali. Mimi ningependa tu walemavu wapata wanaume, kama watu wa kawaida.

Mimi ningependa walemavu wenzangu wakienda hosipitalini watibiwe bure. Maanake unakuta mwingine hana hata kazi, hana hata biashara, atakufa mle mle nyumbani, maanake hana pesa. Lakini kama wanaweza kutibiwa inaweza kua ni bora; maaanake mpaka tuwaangalie wao pia. Wamechukuliwa kamawatu ambao hawana maana.

Mimi ningependa mijengo ikijengwa, maanake unaweza kukuta mjengo umejengwa una stairs, ambayo mlemavu hawezi akapanda. Kuna nchi zingine, ambazo mtu akiwa ni mlemavu, anaweza hata kwenda na wheelchair yake; na hii yetu ya Kenya, pengine unataka kitu kwa gorafa ya nne utangojea utume mtu, ama pengine unaambiwa ngonjea yule unayemtaka atakuja huko. Badala ya wewe kwenda pole pole na ukaongea na yule mtu ambaye unamtaka. Mimi ngeomba watunjengee tu mahali ambapo hata tukiwa na wheelchair, tukiwa na hizi clutches tunawezakupanda na tukaenda.

Kunawalemavu wengi ambao wamesoma vizuri, na unakuta wanaweza kwenda kwa hao wakubwa angalau watutafutie makazi, unaabiwa hakuna. Na ujuzi unao akilini, na,unaambiwa hakuna, kwa kua wewe ni mlemavu huwezi ukapata kazi, unarudi tu. Mara unaambiwa nenda urudi sasa hii serikali yetu, mimi upande wangu naona wana,ubaguzi kwa walemavu.

La mwisho; mimi ningeomba hivi vifaa kama wheelchairs na clutches ningependa zikiagizwa kutoka ng'ambo, tuletewe bure; maanake bila pesa, mimi siwezi nikainuka na hizi. Unakuta kama hauna pesa, ukienda kuchukua unaambiwa, mpaka utoe pesa, ndio utembee. Na huku unaweza kusimama na hii mkongojo na unaiona iko pale huna pesa, unaambiwa, mpaka ununue. Sasa mimi naomba, kama ingewezekana, wangetupatia bure. Wheelchair na hizi clutches, na kuna caliper, kama wanaweza. Ni hayo tu.

**Com. Salome**: Kuna mtu mwenye swali? Mimi ninaswali, unaswali kwake?

**Question:** Mini nauliza anataka wajengewe nyumba mfano gani, ili waweze kupanda?

**Com. Salome**: Hiyo nitamjibia, ni kazi ya wachoraji . Hiyo ni technical question; yakuhakikisha kila mtu anaweza kuingia kwa hiyo nyumba. Kwa hivyo sita mpa nafasi kujibu hilo swali. Mimi nina swali langu kwake. Wewe umesema walemavu wapate maBwana na mabwana, hawawezi kwenda kwa Katiba ati wanaambiwa kila mwanamme aoe bibi mmoja mlemavu ama kila wanaume kumi, wawili wawe wameoa walemavu. Ili Jamba kwani Katiba ni sheria unaona kama sheria ingesema nini ili wanawake walemavu wasaidiwe. Nyuma na hiyo swali umeleta juu na kua mama mlemave, ningependa pia upendezekeze zaidi juu ya shida zingine za kua wewe ni mama, kwa hivyo unashida za kimama. Na pia wewe ni mlemavu, kwa hivyo unashida za mama na za ulemavu. Mimi mwenyewe ni mama kwa hivyo naonea akina mama huruma, nataka kuwahusisha na mimi pia ni

mama mwenye ulemavu; kwa hivyo pia nataka kuwahusisha, wa mama wenye ulemavu. Ningetaka ujieleze zaidi.

**Pamela:** Nilikua nasema tu, mlemavu ni binadamu kama binadamu mwingine, ana mahitaji, ana needs, ana feelings, kama yule mwingine. Sasa ikija kwa mambo ya kupendana kati ya Bwana na bibi, nafikiri hiyo ni kitu kati ya binadamu wenyewe. Katiba kwenye inaweza kusaidia ni labda kusema kama, ukipata mimba, unawachwa na huo mzigo. Hapo ndio kitu kinaweza fanywa kwa Katiba, kitusaidie kama mama yule mwingine; pia mwenyewe anaweza patwa na taabu kama hiyo.

**Question:** Mimi kusema kweli, upande wangu; mimi ni mama, na ningependa kama serikali yetu, inaweza kutuangalia zaidi. Maanake sisi akina mama hua saa zingine tunadharauliwa. Sasa mimi ningependa mwanamke, awe na sauti kama mwanaume: maanake unakuta, pengine una Bwana nyumbani, na wewe ni mama, anakuuliza wewe unaongea kama nani? Sasa mimi ningeomba mwanamke awe sawa na mwanaume.

**Com. Salome**: Asante sana, ndio mara yangu ya kwanza kusikia mama kutoka Pwani, ni mama na ana ulemavu. Sema jina lako kwanza.

**Hadija Ali:** Kwa jina naitwa Hadija Ali, swali langu ningependa kuuliza hivi.

**Com. Salome**: Tafadhali, ningependa kuwaomba tuwe na mkutano moja hapo nyuma ambayo tunashika moja.

**Hadija:** Swali langu ni ili, kama sisi walemavu, kuna wengine walisoma, wengine hawakusoma; wengine biashara zao walikua wakiendesha, kama hivi vibanda, biashara za nje nje. Sasa kama hivi vibanda vimevunjwa, hakuna mahali pa kuweka. Ukienda mahali hivi ukiuliza kazi hauwezi ukapata, na ukiangalia hakuna mtu yule unamtegemea, hata kama una mtu yule unategemea una mahitaji yako. Sasa ningependa serikali, ituwezeshe kututafutia mahali, pia sisi tuweze kujiendelesha na kazi zetu, kama wengine. Tuwe na uwezo hata sisi.

**Com. Salome**: Kuna shida kua mama wa Kislamu, kua mlemavu, na kua kijana. Una miaka ngapi?

**Hadija**: Miaka kumi na nane.

**Com. Salome**: Kumi na nane, kwa hivyo wewe ni msichana, wewe ni kijana , wewe ni mwanamke na wewe ni mlemavu. Unaona kama kuna shida ambazo huletwa na kua na hayo mambo yote, na kama kuna jambo ungalitaka tulifanye?

**Hadija:** Shida zaidi ni upande wa kazi. Ukipata Bwana ni sawa, haukupata mwenyewe wajua wajiendeleza na kazi yako.

**Com. Salome**: Basi wataka Katiba ifanye nini?

**Hadija:** Ningependa Katiba ituendeleze kama wengine, vile vile wanavyoendelea. Hata kama ni kazi, hata sisi tuweze pia kupata kazi, zile ambazo tunaweza kufanya.

**Com. Salome**: Endelea.

**Joyce Awino**: Jina langu naitwa Joyce Awino, mimi si mlemavu, Bwana si mlemavu, na nimezaa mtoto mlemavu; na huyu mtoto, mimi mwenyewe sina kazi, Bwanangu ni kibarua. Sasa huyu mtoto, nikijaribu kumpeleka shule, katika hizi shule zingine wananiambia mtoto huyo ana shule yake. Special school. Hiyo special school mwenyewe sijui ni wapi. Mtoto huyu anakaa hapo hapo, sina njia yeyote naweza kufanya; mwishowe ni kija shtuka naambiwa, sijui ni wapi, ambao nimefanya juu na chini, akapata skuli Kwale. Huko kwale ni pesa. Kwenda ni pesa, kurudi ni pesa. Kufika kule ni maelfu. Nilienda Port Reitz nikaambiwa elfu kumi. Mimi mwenyewe sina kazi, nilikua na kibanda kimebomolewa, jamani, sasa mtoto kama huyu naweza kumsaidia vipi? Elfu kumi sina uwezo wa kupata.

**Com. Salome**: Mtoto wako amelemaa upande gani?

**Hadija:** Amelemaa upande wote hivi. Pande moja.

**Com. Salome**: Anaona?

**Hadija:** Anaona, anazungumza, lakini hatamki matamshi mazuri, ulimi in mzito.

**Com. Salome**: Sasa maoni yako. Unaona unaweza kusaidika?

**Hadija:** Maoni yangu naonelea, hao walemavu pia, nao wapate nafasi, kama ni kusoma wasome bure. Wapate kua wanaweza kusoma bure. Ombi langu ni hilo tu.

**Com. Salome**: Na waende skuli hizo za special school, ama wasome shule hizo za kawaida.

**Hadija**: Wasome shule hizo zao waambiwa ni special school, lakini iwe wanasoma bure kwa vile hizi zingine ukipeleka hawakubaliwi. Unaambiwa wana shule yao, shule yao hiyo ukienda, ni maelfu. Utafanyaje?

**Com. Salome**: Unajua ikiwa mtoto anasoma bure, lakini bado hasomi shule iliyoko karibu na wewe, ikiwa utampeleka shule na urudi, sio pia itakua ni pesa?

**Hadija**: Nikipata shule ya bure, siwezi kushindwa kumpeleka shuleni.

**Com. Salome:** Mimi nakuuliza, kama saa hizi mtoto anakua lazima aende zile shule za kipekee; na wewe hauna pesa, kama angekua akienda shule karibu na iwe ni ya bure ingesaidia zaidi wazazi, ama ingekua tu hali moja na kuambia lazima apelekwe shule ya bali.

**Pamela**: Sasa shule ya karibu ndio hatuna sisi.

**Com. Salome**: Lakini tuko kwenye kutengeneza katiba yenye itatuhusu (inaudible) Katiba yenye itasaidia huyu mtoto wako. Je hii katiba mpya, unataka ifanye nini, juu ya hii shule ya karibu na mtoto wako? Hiyo shule ya karibu na mtoto wako.

**Hadija:** Mimi haja yangu naomba tu, mtoto asome.

**Com. Salome**: Asante sana Awino. Kuna mtu mwenye swali kwa Awino?

**July Oguthi**: Nilikua nataka kujua huyu mtoto wake ni umri gani. Jina langu ni July Oguthi. Nilikua nataka kujua huyu mtoto mlemavu ni wa umri gani? Kama katiba ingefanya skuli zote, ziwe na special section, ya kuchukua watoto walemavu. Yaani kila sukuli hiwe na section ya special education. Ulemavu wowote, hiyo ingesaida wazazi wengi sana. Sijui kama yeye kama mzazi angefikiria kitu kama hicho. Awino sijaelewa hilo swali lako. Sija elewa vile ameuliza.

**Com. Salome**: Na mimi ningetaka kuuliza ni wa kike ama wakiume?

**Hadija**: Ni wakiume, miaka kumi na tatu.

**Com. Salome**: Asante sana Bi. Awino.

**Lucia Karimi**: Mimi kwa majina naitwa Lucia, ni mwalimu wa elimu ya uraia. Na maoni yangu kwa Tume ya kurekebisha Katiba ni haya yafuatayo. Kwanza ningependa sisi wanawake tuweze kuwakilishwa vizuri katika nyanja mbali mbali. Kwa mfano tukiangalia mbungeni, tuna wanawake wanane, mswada wowote ukija kuhusu wanawake, wale wanawake hawana nguvu. Kwa hivyo tuweze kuwakilishwa vizuri, katika bunge letu.

Jambo langu la pili ni kuhusu hao wabunge na madiwani ambao tunawachagua. Ningependekeza raia wapewe uhuru wa kuwaondoa wale wabunge, ama madiwani ikiwa hawatutumizii mahitaji yetu. Kwa sababu tunaona tunachagua mbunge, anapofika bungeni, hata nyumba yake kijijini anaihama, anaenda mbali; Inakua hakuna kazi ambayo anafanya. Kwa hivyo, wananchi wapewe uhuru, na uwezo wa kuwaondoa, wale wabunge, na kuchagua wengine ambao watawasaidia.

Pia, wabunge na madiwani kabla mtu kuchaguliwa, tabia yake iweze kuchunguzwa. Napendekeza kuwe na kamati maalum, ambayo itachunguza tabia za wale ambao wanataka kusimama bungeni, ndio tuweze kujua maishani yao yaliopita yalikua vipi. Sababu tunaona tunachagua wabunge ambao pengine walikua katika mashirika mbali mbali, wameyaangusha, tunakuja tunawachagua kama wabunge, na bado wanaenda kutuangusha, kwa sababu tabia yao sio nzuri.

Jambo la tatu, ni mambo ya labour laws, ambayo ningependa iangaliwe vizuri na Katiba. Kwa sababu siku hizi haitekelezwi ipasavyo. Mfano nikitoa pengine, wanawake wamekubaliwa katika Katiba wasifanye kazi wakiwa wamesimama. Lakini siku hizi tunaona unaenda unasimama karibu masaa kumi na mawili, hakuna overtime, umechoka, na hakuna kitu ambacho kinafanywa, na ni mambo ambayo yanajulikana.

Pia jambo muhimu ambayo napendekeza, hii Katiba tunaitengeneza, lakini je? Wananchi wataifikia vipi hii Katiba? Mimi nafundisha watu wengi kuhusu mambo ya Katiba, lakini unashangaa hata hawaijui iko vipi; hawajaiona, na sijui kwanini wanaambiwa wairekebisha, kwa sababu hawaijui; na mtu hawezi kurekebisha kitu ambacho haja kiona wala hajui kimeandikwa nini. Kwa hivyo ningeomba, hii katiba inapoandikwa iwe ni rahisi, kila mwananchi kuinunua, sio tuambiwe tukainunue Nairobi peke yake ilihali sisi wenyewe hata chakula cha jioni, pengine hauna, unaambiwa enda Nairobi ukanunue Katiba. Iweze kua hata katika bookshop, zenye ziko katika mtaa yetu, pia tuweze kupata ile katiba, ndio tuweze kujua zile sheria. Kwa sababu hatuwezi kufuata zile sheria, kama hatuzijui zinasema nini.

Pia ningeomba katika ugawanyaji wa raslimali za kitaifa; ziweze kua na usawa, sababu tukiangalia sehemu nyingi za nchi, zimekua developed; lakini kuna mahali kwingine ukienda hata barabara yenyewe hakuna. Na hilo ni jukumu la serikali kutengeneza zile barabara, kutoka na zile raslimali ambazo ni za kitaifa. Na watu wengine wana barabara, wana maji, wana vitu vingine, kama hospitali; lakini ukienda sehemu zingine mtu anatembea km zaidi ya thelathini, apate huduma ya afya, na ndio unapata magonjwa mengi ambayo yanaweza kutibiwa, yanaua watu, kwa sababu hizo raslimali muhimu hazigawanyi ipasavyo, ama kwa usawa.

Pia ningependa haki za mwananchi: Katiba zile haki ilizotoa, ziweze kushughulikiwa ipasavyo. Kwa mfano, Katiba yetu saa hizi inakubalia mtu kutembea mahali popote, wakati wowote, lakini ukitembea hata saa moja unusu, washikwa haujafanya kosa lolote Polisi ambayo wanatakiwa walinde usalama wako, ni wao wanakushika na kukushitaki, na hakuna kosa ulilofanya. Pengine umetoka kazini, saa nne ya usiku, unaambiwa warandaranda, unashikwa. Badala ya kuangalia usalama wako unapotoka kazini ufika nyumbani kwako ukiwa salama, unashikwa; na kosa ulilotenda katika katiba, halijulikani kama ni kosa.

Jambo la tatu sisi vijana – kazi. Vijana wamesoma, lakini inapofika wakati wa kupata kazi, hakuna. Unakuta pengine hata mahali pa kazi, ukienda hawangalii hata umesoma umefika wapi. Lazima ujuane na watu wakubwa pale, ama una pesa za kutoa, ndio uweze kupata kazi. Vile viletunasikia elimu yetu ya shule za msingi ni ya bure; lakini sijui ni bure kiasi gani. Kwa sababu

watu wanatoa zaidi hata ya elfu tano, mtoto akiingia standard one. Hata ikiwa ya bure, hiyo ya primary, mtoto akifika standard eight bado hakuna kazi kwa watu wa standard eight. Ningeomba serikali iweze kuanzisha hazina ambayo itashughulikia watoto ambao ni werevu waweze kusoma, ingawa wanatoka katika jamii masikini. Iweze kuwasomesha mpaka hata chuo kikuu, ndio waweze kusaidia wazazi wao, na pia waweze kuondoa ule umasikini. Kwa sababu tusiposoma, umasikini hatutaweza kuupunguza, wala kuuondoa.

Maswala ya ardhi: watu wengi, kwa mfano katika mkoa wa Pwani ni masquatter na tukisikia masquater wamezaliwa mahali pale. Baba yako alizaliwa mahali pale. Babu yako na babu yake, wote walizaliwa mahali pale. Lakini inakua je wewe ni squatter, na umekaa hapo hata zaidi ya miaka arubaini. Ile shamba ni la nani? Na tunaona mtu ambaye ana pesa atakuja, ile shamba atauziwa, kwa sababu wewe hauna kibali chochote cha kusema hilo shamba ni lako. Anakuja kwa sababu yeye ana pesa, pengine ni Mhindi au mtu mwingine wa gazi za juu, katika jamii. Anauziwa lile shamba, na nyinyi masikini mnatimuliwa kutoka shamba lenu. Mmeishi kwa miaka kama arubaini mwaabiwa nyinyi ni squatters kwa sababu hamna cheti. Unaodolewa katika lile shamba, linapewa mtu mwingine. Kwa hivyo napendekeza watu ambao wana mashamba ya mababu zao, ama ya baba zao wapewe vyeti, wawe salama wajue wakikaa hapo hawawezi kutimuliwa wakati wowote.

Jambo lingine kuhusu wanaume ambao wanatabia za kuwanajisi wasichana. Hukumu yao iongezwe. Kwa sababu hii inavunja moyo sana, ukiona mtoto wako amenajisiwa mkienda mahakamani, baada ya siku mbili pengine ametozwa faini ya elfu tano, na anakua huru tena. Na anaanza kuringa kabisa, ulinipeleka nilifanywa nini. Na hiyo tabia yake haitaweza kurekebishwa, hata ndio ataendelea kufanya hivyo zaidi. Jambo hilo linatunyanyasa, sisi kama wanawake.

La mwisho, nikiongea kama mwanamke: ningependekeza Katiba iweke kue ni hatia, mme kumpiga bibi yake, kwa sababu kila mtu ni mkosaji. Je kama wanawake ukikosa wewe wapigwa na Bwanako, na yule Bwana naye akikosa mbona isiwe pia ninaweza kumpiga pia? Kwa hivyo ni hatia, na Katiba isimamie jambo ili, ya kua mwanamke asipigwe kwa sababu ya kufanya kosa lolote. Mwanadamu yeyote anaweza kufanya kosa. Ni hayo tu nilionayo.

**Com. Salome**: Asante sana bi. Lucia. Kuna mtu mwenye swali? Mimi nina maswali kadhaa Bi Karimi. Kwanza umesema kua kina mama vile wanavyoshughulishwa kwenye uongozi haitoshi. Hawasimamii vilivyo. Ungetaka kuona wangapi katika bunge na katika udiwani, ndio kina mama wawe wamesimamiwa vilivyo? Umesema kua watoto wale wametoka jamii masikini, na wana akili nyingi, waweza kusoma, watengewe pesa kiasi fulani ndio iwasomesha. Je nina yule mtoto masikini lakini si mwerevu, si pia angetaka kusoma? Kwani kama angekua wa tajiri hata awe si mwerevu, bado angesukumwa mpaka amalize shule. Huoni hii kua ni haki ya mtoto? Umesema pia watu wakishakaa muda mrefu pahali, wapatiwe cheti cha kuonyesha kua hiyo ni ardhi yao, ili wasije wakatimuliwa, ungetaka kama muda mgani hivi? Ndio tuweke kwa Katiba. Ukisema tu hii iangaliwe haitusaidii sana. Na ya mwisho umesema kua adhabu ya watu wenye kunajisi wasichana iongezwe. Iongezwe kutoka wapi mpaka wapi?

**Lucia**: Nafikiri nikijibu kwa upande wa masomo, nimependekeza elimu ya msingi iwe ni ya bure. Lakini ile elimu ya shule ya upili, wale wanaojimudu kifedha, walipe. Wale ambao masikini, na hawawezi kwenda zile shule za upili; kuna vyuo mbali mbali, kama polytechnic, ambapo wanaweza kutafutiwa ujuzi mbali mbali, ambao unaweza kuwasaidia, kama cherahani, ujenzi na wa nyumba. Kwa upande wa ardhi pengine ningependekeza kama watu wamekaa mahali kwa muda wa miaka kumi, na pale pahali hapana mwenyewe, waweze kupewa kile cheti cha kuonyesha ile shamba ni yake, na kabla hawajapewa kuwe kumetolewa idhini ya watu kutetea ikiwa kuna mtu anayedai pale ni pake. Kesi yake, ndio kama hakuna mwenyewe, iweze kua yule mtu atapewa pale pahali.

Katika hukumu ya hao wenye kunyanyasa wanawake, ningependekeza afungwe miaka ishirini ashike adabu, na hataweza kufanya mambo kama yale tena. Na kama ni mambo ya kutoa faini, hiyo faini iondolewe kabisa, kwa sababu hiyo ndio inazidisha mambo haya. Kwa sababu ikiwa anatoka katika jamii ya tajiri, hata akiitishwa laki moja, atatoa bila shida yeyote, na lile kosa atalirudia kwa vile anajua jamii yake wataweza kumtoa. Sijui swali lako lingine lilikua lipi?

**Com. Salome**: Ni moja ilikua juu ya namba ya wamama ungetaka kuwaona kwenye bunge ndio usikie kina mama wamesimamiwa vizuri.

**Rukia**: Kina mama pengine ningependekeza; katika nchi yetu twaambiwa kina mama ni 52%. Kwa hivyo sijui kwa nini wanaume wawe wengi katika uongozi ilihali sisi katika population ndio wengi. Kwa hivyo 50% iwe wanaume 50% ikuwe wanawake, ndio hata kama kuna mswada, itakua ni rahisi akina mama kujiwakilisha wenyewe.

**Com. Salome**: Asante sana. Sema majina yako kwanza.

**Zubeda Sumba**: Nilikua nauliza, amesema a tuwe na kamati za kuchunguza hao wagombeaji viti, kabla ya kusimama; sasa hizi kamati zitaundwa na akina nani?

**Rukia:** Hizo kamati zitaundwa na wananchi wenywe, kwa sababu wao ndio wanaowakilishwa, na wao ndio watajua yule mtu anafaa kuwawakilisha ama hafai.

**Com. Salome**: Asante sana Bi. Karimi. Nani mwingine ana maoni? Sema majina yako, halafu utoe ni maoni.

**Afua Faki:** Jina langu ni Afua Faki, ningetaka tu kuongezea juu ya viti za kina mama bungeni. Kwa kweli ni kwamba, wakati wa uchaguzi, kina mama tuko wengi; lakini hata iwapo mama amesimama, pengine kuna wanaume watatu na mama mmoja. Utapata kua mwanamme amechaguliwa na huwezi ukasema kitu, na ni sisi kina mama ambao tumechagua wanaume, pengine ni kwa sababu fulani ambazo hauwezi ukaziepuka. Inaweza kua yule mama ni mgeni katika ile constituency ama anything ambao itakua ina overrule. Kwa hivyo tukitaka akina mama wawe wengi bungeni, kuwekwe percentage, ambao ni lazima kina mama,

hiyo percentage ni viti vyao, wamepangiwa. Wata-contest wamama kwa mama. Viti hivyo vitakua ni kina mama peke yake. Hapo ndio tutapata nafasi akina mama kuwa wengi. Hata kama 40%, I think it is a good number.

**Com. Salome**: Asante sana. Kuna mtu mwingine ambaye angetaka kutoa maoni yake?. Julie njoo.

**Julie:** Utaniongoza kama nimekosea, lakini katika Constitution ilivyo hivi sasa, kuna section inayosema: mtu yeyote anaye pigania kiti cha bunge, lazima awe able bodied. Kuna kitu kama hicho? Yaani kitu kinachopinga mlemavu, asipiganie kiti cha udiwani, ama cha bunge.

**Com. Salome**: Mtu yeyote anaweza kupigania kua mbunge, na anaweza kuteuliwa kua mbunge, isipokua awe hajiwezi, awe kipofu, ama kwa hali kama hiyo. Mara nyingi tukizungumza na Bwana Attorney General ametwambia kua, sisi ndio hatuelewi maana ya kifungu hiki kwani haikua iwe hivyo. Lakini wewe tupe maoni vile unavyo kielewa wewe mwenyewe, ikiwa kinahitaji kurekebishwa, ili kikaeleweka na kila mtu vilivyo.

**Julie**: Mimi binafsi kwa ajili mambo haya ya Kikatiba yana tatiza sana; section kama hiyo inyoleta confusion, afadhali iondelewe kabisa, ili mtu yeyote aweze kupigania kiti cha bunge ama cha udiwani. Na ninge-recommend affirmative action, ikipewa akina mama ipewe pia na walemavu. Kama viti fulani vinatengewa akina mama, na pia viti fulani vitengewe walemavu. Ikiwa hivyo tunaweza kupata mama wengi sana tunaingia bunge kwa kua mama na kua mlemavu.

**Com. Salome**: Tunasema iwekewe kina mama na walemavu ambaoe ni kina mama. Hapo amefunikwa na pazia mbili, ya umama, na ya ulemavu; ukimwondelea ya ulemavu basi unabaki na akina mama peke yao. Nani mwingine angetaka kutoa maoni yake. Unataka kuongezea? Hebu mpe huyu mama, najua anasimamia viziwi.

**Pamela Atieno**: Kwa majina naitwa Pamela Atieno. Mimi ningependa serikali yetu, ikatalie haya majina ya kiwete, kiguru, kipofu, maanake unakuta saa zingine natembea pale nimeguza mtu, unasikia ananiambia, angalia huyu kiguru. Sasa hii kiguru, na mimi ni binadamu ambaye ni na pumua kwa nini naitwa K, hii K inatoka wapi? Kiguru, kipofu , kiwete. Haya majina siyataki. Sasa mimi ningependa serikali yetu mtu tu, ukisikia mtu amekwambia kiguru, mwende mbele, akuelezee hii Kiguru ni nini? Maanake sielewi. Na ningependa tena, kule bungeni kama kutakua na uchaguzi, mmoja awe mlemavu, awe akitutea. Maanake tukiwa hivi hivi hakuna atatutetea, tumesumbuka ya kutosha. Sasa kama kutakua na mmoja wa walemavu wa kututetea itakua ni afadhali. Asanteni.

**Com. Salome**: Kuna mtu mwingine angetaka kuchangia?

**Com. Pastor Ayonga**: Mwidani. Kama nimesema jina lako vibaya, wewe unajua ni nani. Ni wewe? Basi si mzee uje hapa utoe maoni? Endelea.

**Mohamed Mwidani**: Shukrani sana Bwana Kamishena kunipatia nafasi hii. Maneno yale nitakayo kuyapendekeza katika Tume hii, ni maneno machache sana. Naitwa Mohamed Mwidani, na mimi nimkaaji wa hapa. KwaShee area, ya hapa Mikindani. Sasa nazungumzia kuhusu mambo ya watu ambao wanafanya kazi kwa serikali, mpaka kumaliza miaka yao; na baadaye kuambiwa kwenda kuchukua haki zao Nairobi. Sasa nilikua napendekeza kwamba, kulingana na serikali yetu hii itakayo kuja ifanye mipango wale watu wa kuretire; pesa zao wawe wakilipwa katika mikoa yao. Ama katika district zao. Kwa sababu watu wanatoka sehemu mbali mbali za mikoa hii ya Kenya na watu wengine Nairobi hawana mahali pa kulala. Mtu anakwenda, na pesa zile alizokwenda nazo anazitumia kule mpaka zinakwisha na pesa hajaalipwa. Ningependekaza watu wawe wakilipwa katika district zao, kama watu wakutoka Kilifi, wawe wakija kupokea pesa zao hapa Mombasa. Watu wakutoka kule Kisumi vile vile, wapokea zao Kisumu. Watu wengi hupata shida ya kwenda kule Nairobi, watu hukaa karibu mwezi mzima, kabla hajalipwa pesa zile, mpaka zile pesa zamwishia, inakua tatizo baadaye. Sina mengi ni hayo tu.

**Com. Pastor Ayonga**: Huu ni mzigo mkubwa uliobeba husumbuka. kama hizo fedha. Alfred Nzai. Alfred unamaandishi? Memorandum? Una point kidogo. Basi endelea kutoa point zako kwa maana dakika zako zinaenda.

**Pastor Alfred Nzai**: Kwa jina naitwa Alfred Nzai kutoka Uzima Baptiste Church, hapa Bangladesh. Nimefurahi kupata nafasi hii ya kutoa maoni yangu, kwa Tume ya Katiba hino ya marekebisho. Maoni yangu ambayo ninayapendekeza, ni mfumo wa kimajimbo ambayo ndio yaweza kufanikisha maendeleo na kusawazisha mamlaka ya mikoa, na wazalendo wa kila sehemu ya Kenya wapate kunufaika. Na aina ya majimbo haya, sio yale majimbo wengi wanayoyafikiria, ama tashwishi nayo. Ni majimbo ambayo yana ruhusu Mkenya kua mahali popote bila passport, ama kwa kufanya biashara ama kwa kufanya maendeleo ya kudumu. Na kila Mkenya kufanya kazi, ama biashara, ama kumiliki shamba, ama plot mahali popote katika Kenya.

Wakuu wa mikoa ama wilaya, tarafa, chifu na manaibu wao, watoke mkoa ni kwao. Wakuu wa serikali, wizara zote za serikali, P.C. District Commissioners na wakuu wa wizara zote, watoke mkoa wao. Wafanya kazi wa serikali, sabini kwa mia, watoke katika mkoa wao.

Na pia ninaona kwamba unywaji wa pombe uruhusiwe, kulingana na azimio la mkoa, unavyopenda. Kama ni vilabu, ama kama ni kunywiwa kwa time Fulani, iweze kua huru. Na pia ninapendekeza kwamba kuwe na polisi wa kuchunga polisi. Kuwe na polisi ambao wanachunga polisi. Katika Kenya Army, kuna Military Police ambayo hukamata askari mwinginge. Na hapa tunaona polisi wamekua huru sana, hawana mtu ambaye anaweza kuwashika kwa makosa yao, huko mitaani. Na kwa hivyo ikiwa kuna department nyingine ya polisi ambayo inatembea tembea kuangalia polisi, wanashika watu kwa njia gani, hii inaweza kusaidia wananchi wanaonyanyaswa na polisi.

Na pia raia waruhusiwe kujilinda na silaha ambazo wanaweza kupata kutokana na wezi na magaidi Na katika upande wa

elimu, ninapendekeza kue kuna elimu ya lazima, hata kwa kama masomo ya sheria. Wanafunzi wanaofundishwa, iwe kuna somo la sheria; mtu apate kujua sheria na haki zake kama mwananchi. Wengi tunashitakiwa, hatujui haki zetu, hatujui hata sheria ile ambayo inaweza kutupatia ufahamu wa haki zetu. Basi hatuwezi kujua tunashitakiwa kivipi, lazima tukodishe wakili ili tuweze kutetewa; maana yeye ndiye anajua sheria, lakini wananchi wote hawajui sheria. Lakini kama wanaweza kufundishwa elimu ya sheria, kutoka secondary, wanaweza wakajua haki zao. Na pia liwe somo lingine, kama elimu ya siasa, pia liweze kufundishwa. Elimu ya jeshi pia iweze kufundishwa katika mashule. Elimu nyingine ni ya kilimo, iweze kufundishwa na iwe ni lazima watu waweze kulila. Elimu ya health (primary health care) iweze kufundishwa na iwe ni lazima watu kuisoma. Katika upande wa elimu ya kilimo ninapendekeza kwamba serikali ilazimishe watu kufanya kilimo, si kusoma tu kujua kulima, lakini walazimishwe kulima. Na kwa sababu kifungu kama kile cha kukataza unywaji wa pombe, kitakua kinaweza kuondolewa, lakini watu waweze kulazimishwa kulima; hata kama ameajiriwa kazi mahali Fulani, lakini aweze kuhakikisha kwamba ana mahali analima. Maana wengi wanapata pesa mishahara mkubwa, lakini ukimfuata hana hata eka moja anaweza kulima, na tunapata upungufu.

Kilimo kiwe kinaweza kulazimishwa. Kwa mfano hata kampuni ambazo zimeweza kujijenga, zinafanya kazi za haina mbali mbali, lakini kampuni nazo ziweze kulazimishwa kupata sehemu ya kulima; ili kwamba chakula kiwe kingi kwa sababu kampuni zina nafasi nzuri zaweza kununua matingatinga na zikafanya kazi ya ukulima. Tunayo ardhi nyingi ambayo ni pori inahitaji kulimwa, ndio

Dini: Uhuru wa kuabudu katika nchi ya Kenya umeruhusiwa na katiba yetu. Lakini serikali ingawa imeruhusu uhuru wa kuabudu haihusiki kusaidia mambo ya kuabudu. Ningelipendekeza kwamba, kuwe kuna wizara ya dini. Wizara hii inaweza kusaidiana na department kama ya social services ikawekwa pale pia religious matters. Na serikali iweze kutoa katika budget yake mapato yake kama 10% ibwage huko kwa hiyo wizara ya religion. Kuna nchi nyingine nyingi, kama kwa mfano, Uarabuni serikali zinagharamikia mambo ya dini, na inatoa percentage kubwa kujenga mambo ya dini. . Kenya, serikali imeruhusu uhuru wa kuabudu, lakini haisaidii mambo ya religion. Kwa hivyo napendekeza serikali itoe fungu la kusaidia mambo ya dini. Hii itaweza kusaidia mambo ya development kama watu masikini, walemavu na watu wengine. NGO's ambao wana social services, ziwe chini ya wizara ile. Nafikiri ili litaweza kutusaidia kuondoa haya mambo ya umasikini, kwa sababu tunapo mtolea Mungu, nafikiri itaweza kua ni baraka. Na muda wangu kwa kua umekwisha, ninapenda kushukuru Mungu kwa sababu ya kupata nafasi hii, na nina shukuru kwa hayo machache, ambayo nimeweza kuyatoa.

**Com. Pastor Ayonga**: Lakini kabla hujatoka nataka nikuulize maswali ili unipe nuru. Kitu cha kwanza ambacho nimeoma unataka tuweke katika katiba ni unywaji pombe uruhusiwe. Na nilidhani nilikusikia vibaya, pengine ni mdomo umeteleza. Lakini pastor unajua kila kitu tunapo sema kifanywe, tunaangalia faida ambazo tutapata? Ama sivyo? Tunaangalia tutafaidika namna gani kama taifa. Kwa sasa najua Kenya yetu kuna watu wanakunywa pombe. Lakini sasa unapo ongeza kwamba hii pombe iruhusiwe, nikana kwamba tunaenda kua taifa la walevi. Na hapo sioni jinsi ambavyo tunaweza kuleta maendeleo, kuleta utajiri au kuzalisha mali. Kwa maana mlevi haendi shambani, tayari umesema serikali ilazimishe watu kulima. Sindio? Si kwamba

watu waambiwe walime, lakini walazimishwe. Sasa hao walevi watalazimishwa saa ngani?

Na kabla hujajibu hiyo kuna kingine pia ambacho limenishutua, lakini pengine ndivyo Wakenya wanataka, raia kuruhusiwa kua na silaha. Na haukutuambia, watakapo kua na silaha nini kitafanyika? Na ni silaha za namna gani? Kwa maana najua kila kabila tuna silaha za ukoo. Kwa mfano pahali ninakotoka mtu katika boma yake ana mkuki, mkuki huo unakaa hapo tu. Ni silaha. Lakini ana rungu ana jembe na ana panga ambao anatumia kufanyia kazi zake. Sasa sikuelewa unaposema kila mtu awe na silaha, ni AK47? Na tena lingine ya mwisho; kulazimishwa watu kulima. Tayari nchi yetu wakulima nimesikia wanalia kwamba wamelima sana, wana mahindi, wana maharangwe, lakini hawana soko. Wanalia kwa kukosa soko. Sasa tena hao watu utawalazimisha walime wafanyie nini? Tafadhali kama unaweza kufafanua hayo machache, useme tu kwa ufupi. Pombe, elimu ya kijeshi, na watu kulazimishwa kulima. Hebu sema tu kidogo juu ya hayo.

**Pastor Alfred**: Kuhusu pombe, nimesema hivyo kwa sababu, pombe imekatazwa katika nchi yetu. Na pombe hii hunwewa zaidi, katika nchi yetu. Na tunaona kwamba mtu anayefaidika, katika mapato ya kuhusu mambo ya pombe, ni polisi peke yake, sio mahakama ya koti kupata faini. Faini tukilinganisha na zile pesa zinazotolewa na wananchi kwa polisi, na zile faini zinazocharge-wa kule, kwa sababu wengi hawafikishi kwa koti. Kwa hivyo ninaona kwamba watu waruhusiwe kunywa, lakini sasa kuwe kuna lazima ya ukulima, polisi wachape watu kwenda kulima, badala ya kuchapa watu kwa sababu wamewashika na pombe.

**Com. Pastor Ayonga**: Na silaha?

**Pastor Alfred**: Silaha - napenda kufafanua upande wa silaha: magaidi wamechukua nafasi ya kupata silaha za nje, wanaziingiza hapa, polisi hawawezi kuzuia hizi silaha kuingia, sijui kwa nini. Lakini wenye biashara, wenye maduka ambao wana pesa, wananyanyaswa na watu ambao wanatumia silaha. Na wao wenyewe hawaruhusiwi kujilinda na silaha. Kwa hivyo si kwamba nimesema kila mwananchi, lakini kuna wananchi ambao wanamali, ambao wanapaswa kuruhusiwa kujilinda na silaha.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante. Lawrence Oseje. Unaweza kutoa maandishi yako na kujiandikisha. Ni jina nimesema vibaya, lakini siangesikia. Joseph Obalo. Rashid Mwambula.

**Rashid Mwambula**: Nachukua nafasi hii kushukuru hao Kamishena, wa hii marekebishwo ya katiba, katika nchi yetu ya Kenya. Mimi naitwa Rashid Mwambula nimzaliwa wa Kwale. Kuhusu mambo ya hii Katiba yetu ya Kenya kwanza nagusia upande wa uchaguzi. Uchaguzi upande wa urais, upande wa ubunge, upande wa udiwani. Napendekeza kwa serikali ijayo, katika Katiba tulionayo, nafikiri mbunge anawakilisha mahali anapowakilisha ki sheria, hakuna mambo ya umri pale, vipindi hakuna kwamba pengine vipindi viwili, hasimami. Ataka pale awakilishe mahali pale, mpaka wananchi watakapo mkataa. Hakuna sheria inayomzuia yeye asisimame tena. Kwa hivyo, napendekeza kwamba Tume yetu ya marekebisho ya Katiba, wabunge waruhusiwe vipindi viwili, mwingine anaingia. Nafikiri hii itakwenda sababe na uchaguzi wa rais. Rais katika Katiba

yetu ndiye anayeenda vipindi viwili. Nikiguzia pia pande wa udiwani, haswa mayors wetu. Mayor wetu wachaguliwe moja kwa moja na wananchi. Na sema hivyo kwa sababu mnaona matatizo mengi katika baraza zetu. Mtu anapokosea kidogo, mayor yule anawakilisha watu elfu kumi, anatolewa na watu wawili; hali kama hiyo inanyima raia wengi haki zao. Kwa hivyo uchaguzi ujao, mayors wachaguliwe na wananchi moja kwa moja.

Tukirudi hapo upande wa uchaguzi. Kama vile mnaona serikali yetu ya Kenya, ndipo kwamba mfumo wa vyama vingi ulipoinga mwaka tisaini na mbili; serikali yetu ya Kenya hii, watu wengi walipokua wanataka mfumo wa vyama vingi, walisema serikali ya Kenya haijafikia kiwango hicho. Chama kiwe kimoja tu, lakini mkileta mambo ya sheria hii itawaweka Wakenya kwenye kimisingi ya ukabila. Kenya kweli tumekwenda uchaguzi vipindi viwili, tushaamaliza, hatukuona tofauti yeyote mbali mahali pa siasa ni siasa. Ili na ili hutokea. Ni wakati sasa Wakenya mfumo ambao kidogo utasawazisha; mfumo wa serikali za mikao. Sisemi hivyo nikimaanisha Wakenya wajinganye kwa misingi ya kikabilia; bali hata wale wanaoelewa mfumo huu, wanaielewa faida yake haswa nini. Kila mkoa ujisimamie wenyewe, mambo ya Pwani, yawe ni Pwani . Mambo ya Nyanza, yawe ni ya Nyanza. Mapato ya mikoa ile, kama vile ambavyo imelewaka, kwamba kiwango cha raslimali, utakuta kwingine kuko nyuma zaidi, kwa mfano mkoa wa Pwani. Mkoa wetu uko nyuma zaidi na raslimali ziko za kutosha. Ni kwa sababu ya mfumo tulio nao, maana mambo ya Pwani mengi, rasilimali itakwenda istawishe sehemu nyingine. Lakini kwa nia nzuri, katika mfumo huu, nadhani uta sawazisha raslimali zile zitakazo tumika kisawasawa. Nashukuru sana na Mwenyezi Mungu atujalie, mambo haya yawe vile Wakenya wanavyotaka. Asanteni.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante sana, unaweza kuja hapa ukajiandikisha. William Mgamdi. William fanya kwa kifupi. Tuambie lile jipya ambalo na wewe ulikua umejiwekea. Wala halijatajwa na yeyote.

**William Mgandi**: Asanteni sana Kamishena ya Katiba ya Kenya, ambao wameshafika hapa Mikindani. Mimi naitwa William Mgandi Kichororo kutoka sehemu za Kwale district. Wazee wa Mijikenda katika Coast Province nzima, kawaida yao wanaitisha mali nyingi, kwa wasichana wao. Sasa nilikua naomba katika hii Katiba ipitishwe katika sheria kwamba: wasichana tuwe tukiweza kuwaoa kwa ng’ombe tano peke yake, badala ya ng’ombe ishirini. Tunapata taabu ya kuoa hao wasichana.

**Com. Pastor Ayonga**: Na unataka hiyo iwekwe katika Katiba. Unajua mambo tunayoweka katika Katiba ni mengine. Wewe ni kupatana na yule babake msichana. Sasa tutaandika wazee wangapi?

**William:** Sasa wavulana wa sehemu hii, hawawezi kulipa hiyo gharama ya ng’ombe.

**Com. Pastor Ayonga**: Basi muongee nyumbani, msikilizani.

**William**: Rais yule atakayechaguliwa mwaka ujao apunguziwe uwezo wa kutawala hii nchi. Asiwe na sheria zake za kujipendekezea yeye mwenyewe. Pesa za wale wafanya kazi wote ambao wamefanya kazi ziwe zinapatikana haraka

iwezekanavyo. Kama mtu ameshafikisha miaka hamsini, awe anaweza kulipwa pesa zake za uzeeni, na vijana wengine wachukuliwe katika kazi hiyo waendelea.

Pombe katika sehemu yetu ya Pwani hii, ndio uchumi wetu, kwa hivyo tunaomba serikali ituruhusu kuendelea kuuza pombe. Polisi yeyote awe barua kutoka kwa chifu, yakumruhusu kuingia nyumba ya mtu na kumchukua: lakini si kushika watu ovyoovyo saa yeyote, hata kama umetoka nje umeenda dukani kununua sukari, unashikwa.

Sheria zote ambazo zitatungwa katika Kenya nzima, tunaomba ziwe zikitangazwa kwenye maredio, ama kwenye magazeti; ili watu wote wa Kenya wapate hizo habari haraka iwezekanavyo. Na naona mengine, pengine mkitupatia nafasi tuweze kuendelea kuwapatia maoni, pengine mwezi ujao, kama itawezakana

**Com. Pastor Ayonga**: Hayo ni ya Mungu, ya mwezi ujao hatuyajui. Alexious Munge. Sema majina yako na endelea.

**Alexious Munge**: Kwa majina mimi naitwa Alexious Munge, na mimi ni mkaaji wa hapa Pwani, lakini asili yangu ni kutoka kule Bara. Lakini mimi nikiwa hapa, najisikia huru, kwa sababu niko hapa karibu miaka kumi na miwili. Na maoni yangu ni kama ifuatavyo. Kwanza ningeomba Rais wa Kenya asiwe wa chama chochote. Awe anachaguliwa na watu ambao wako independent. Kwa maelezo kidogo na sema, tumeona tangu Kenya ilipojinyakulia uhuru, tumekua tukiongozwa; lakini tukakuta Rais ambaye ako katika vyama, anaongoza kundi ndogo katika jamii zetu. Kwa mfano anakuja Pwani anachukua watu watatu, anafanya ndio wasemaji wake. Anaenda kwa kabila nyingine, anachukua watatu, kwa hivyo kabila nyingine wanabaki kua masikini. Na kama wanataka kitu, wanaenda kupigia magoti wale watu waliochaguliwa kutoka kule juu.

Maoni yangu ya pili Ministers katika serikali yetu wawe wakichaguliwa na bunge. Hii ni kuwafanywa wawe huru katika kufanya kazi zao bila kuingililiwa. Sio kumfanyia mtu fulani kazi, lakini awe anafanya kazi akijua anafanyia raia. Kwa kua atakua namamlaka kamili ya kuweza kuendeleza nchi yetu.

Kutoka hapo nitakuja katika elimu. Elimu ni nguzo muhimu sana katika nchi yeyote inayoendelea. Lakini serikali yetu ni kama haioni maana ya elimu. Sababu kila siku wanaeleza watu, watoto wasome, watoto wasome. Lakini hii leo ningeomba katiba hii inayoudwa ihakikishe kila mtoto ambaye anatoka skuli anapata kazi. Kwa mfano, baba na mama wanajitahidi wanauza ng' ombe, wanauza kuku, wanauza paka, wanauza ubwa, mpaka wengine inawabidi kuuza wasichana wao wadogo; kusudi watoto wengine wasome, lakini wakitoka; hakuna kazi. Kwa hivyo naomba katiba hii iweze kufanya vile itawezekana, mpaka wakitoka skuli waweze kupata kazi ili wawe taa kwa wale wako nyuma. Kwa sababu hii tunaona, watoto wengi wakisoma wakikosa kazi, hao wengine wanasema fulani alisoma, lakini tuko naye hapa, sasa inasaidia nini? Kwa hivyo hiyo ndio naomba.

Ya pili: naomba serikali yetu, Katiba itakayokuja iweze kuwalipa wasomi wetu vizuri. Tunakuta kuna wasomi wetu wanatoka

wanaenda ng'ambo kutafuta kazi huko, na wakiambiwa warudi hapa, hawawezi kulipwa vizuri sasa wanaenda kupeana masoma ambayo ingesaidia vizazi vyetu, na watoto wetu wanaenda nje: sasa tunawadhulumu. Kwa hivyo inaonekana kwamba kama wangekua hapa, tungekua na watu ambao wanapatia watoto wetu elimu ya kutosha, na ambao inafaa zaidi.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante sana mzee, sasa mtoto akienda huko ng'ambo, na akapata kazi akalipwa vizuri, sina wewe unafaidika. Mzee kuna ubaya gani?

**Alexious:** Na mimi nataka kusema hivi, unajua sisi kama Waafrika; Mzungu akija Kenya akiona mtoto wako ni mwerevu sana, hataki sisi Waafrika tuendelea. Anataka kumnyakua ampeleke kule. Kulingana na vile walijua sisi ni watu wa hali ya chini. Kwa hivvyo watoto wetu tuwaache hapa, na tuwalipe vizuri wataelezea hao watoto wengine, na sisi tunazidi kukua. Kwa hivyo hatuwezi kukua ikiwa mtoto muerevu akierevuka hapa, anapelekwa ng'ambo, tunapata taabu.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante una lamwisho?

**Alexious**: La mwisho kabisa ni makao. Makao ni kitu ya maana, kwa hivyo naomba sheria ya Kenya ihakikishe ya kwamba, neno squatter haliko Kenya. Kuna nchi kubwa sana kutoka hapa mpaka hata Nairobi, na sehemu zingine hazina watu. Serikali iweke maji ipunguze wanyama. Wanyama wa pori, sio watu kufa Mathare, na sehemu nyingine kama Moroto. Wapewe mashamba huko na waweze kuyaendeleza, na waweze kukua. Poverty is the best incentive to creativity. Kwa hivyo tukiwa wengi ndio tutasaidika.

**Com. Pastor Ayonga**: Thank you so much, thank you so much. Njoo ujiandikishe hapa mzee. Kuna Lukas Adams. Na wa mwisho atakua Ismael Babala. Wewe ni Ismael? Sawa.

**Lukas Adams**: Asante sana Bwana Chairman. Mimi kwa jina naitwa Lukas Adams. Ningependa kuzugumzia juu ya youth employment opportunities. As many of us are now aware our economy is now lagging far behind it's potential for providing jobs for adults, and young people. Our elementary and secondary education systems, have failed to provide the education each Kenyan child deserves. Our 8.4.4 system of education can actually 66 argued to be child abuse; and I hope that our new Constitution will do away with the 8.4.4 system of education, and cost sharing. For sometimes we have had very many children not going to school, because there is a condition of cost sharing. Many are aware that in this country 56% of kenyans are leaving below poverty level. This type of persons have nothing to share in education with the government. Therefore the government should provide for education.

I begun in 1992, to preach about the need to provide for a youth employment opportunity act. Such an act could save lives, and natural resources and of course the money that we spend on prisons for the young people who do not have anything to do. The act is even more vital today, when almost 70% of the youth are out of employment.

The youth employment opportunity act, would provide a system to thousands and thousands of young people who have been victimized by the problem of laggish economic growth the, inadequate education system and social disorientation. It may not offer solutions to the basic unemployment crisis which we must look for other ways to deal with. But it will be a means for restoring our young people productivity and meaningful lives; and for alleviating the impact of unemployment on individuals or society at large. The act may establish a youth conservation corps to protect school drop outs, and youngsters who have failed to acquire basic education, and those who have failed to locate permanent employment. This are the youth, who should have high hopes of their generation, but instead have become prisoners of their environment, and discouragement. We have seen that quite a number of youth now are actually drug addicts. We should take this as an emergency because the youth are the majority in this country. Some of the activites are the ones that have encouraged the increase of HIV in this country.

Therefore the new Constitution should address the issues of the youth. If it does not do that, then it will have no meaning to the majority of Kenyans, in this country. We have roads, we have forests on which we spend a lot of money calling for people from outside to come and conserve, We could use the youth to conserve the forests, to build institutions like schools and pay the same money we have been borrowing from foreign banks and spend of the same on foreigners. There is need for sure to look at our ways of doing things, more so government policies on employment and education.

Today, perhaps when you are driving to Mikindani, you will reach a corner there, nearly a 100 youths are idle there, making noise, some fighting, we call them touts; but I do not think they are touts. These are people who have nothing to do, and infact most of the time they do wrong things. If the Constitution has to have any meaning in this country, it has to address the issue of youth.

Another problem, that perhaps, we may not be taking the right decisions, is on HIV. There is a big number of Kenyans, who are now affected by HIV, and the Ministry of Health is now spending billions of shillings you have seen people driving big cars, talking of prevention of HIV and so forth. And yet those who have already been affected; nobody is providing free medicine, and even if possible, provide food. Many of our people are now dying because of poverty, not of HIV only, because we are told by experts, without propery feeding, someone affected by HIV cannot live longer. So there is need while we address the issue of poverty, to look at those who have been affected already by HIV to provide free medicine for them, and these we should put in our plans, it should not be just a slogan, we will get money we will give to what and what. It should be put in the new Constitution. Other countries have taken the necessary measures, against this disease. Take for example Uganda, we are told that, the number of people affected by HIV, are now fewer; because of education, and free medicine given to the victims.

Many of our problems really cannot be addressed by the Constitution, we also need to change our culture. Quite a number of our children now do not even know who they are; they cannot identify with this country, and for some of us who have been lucky to travel outside, Kenyans will prefer to be called Nigerians, even in the foreign countries. You ask someone where do

you come from? I come from Nigeria in Africa. There is need for each of us to belioeve in ourselves, and this can be done, if those who are leading us, believe in this country. To believe in this country I mean, why should we do a lot of import of sugar, why should we import even clothes while our industries are dying. There is need to put a restriction on imports. There is need also, like Americans did, not to allow few Kenyans to own a lot of property. These property, sometimes is used agaist the state. They can buy guns from outside, to overthrow the government, they can even control our prices, by just conspiring to bring maize. For example, I was brought up in Kitale myself. Last year I had 150 bags of maize. Now we can not sell it for a thousand shillings, we can not recover what we used for planting, just because few businemen have actually imported maize without paying duty; so our local production has no market, and this kills the economy. So there should be, I think in America it is called anti-trust. We know as we said in the morning, there is free enterprise. But free enterprise cannot be at the expensive of killing your own economy. You can not ask someone earning 1000 shillings to buy bread for 100 shillings, and yet he can not afford it. So there is need for anti-trust laws; not to allow someone to own almost all industries in the country. There is need to encourage local ownership in this country. Thank you.

**Com. Pastor Ayonga**: I want to thank you very much for your contribution. Could you come this way and sign, if you can leave us with the material. Okay no problem but you can sign. Wewe ndio mtu wa mwisho? Basi toa machache, yale makubwa makubwa. There is just this young man, who has just come in, let me get his name. Is there Dominic Okelo. Dominic nataka ufike hapa mwisho, ili yule mzee akiacha microphone itakua yako.

**Ismael Mbabala**: Jina langu naitwa Ismael Mbabala. Mimi ni mkaaji wa hapa Mikindani, Kwamwanzia. Mimi ningependa kuchangia kuhusu habari ya Katiba. Kitu muhimu ambayo imenileta hapa, ni kujua habari ya Katiba. Kwa maana habari ya Katiba yetu, inasonga tu, leo inasemwa tunairekebisha, kesho inarekebishwa. Inarekebishwa mpaka lini? Tunataka tujue mambo ya Katiba, tujue, itarekebishwa lini, na tutakua na uchaguzi lini?

**Com. Pastor Ayonga**: Hebu nikwambie mzee. Sitakujibu swali lako, na pia hatukuja hapa utuulize maswali. Umekuja hapa utupe maoni, ya vile vitu unavyotaka vifanyike. Mimi sitakwambia uchaguzi utakua lini, mimi sitakwambia ni kwanini Katiba inageuzwa. Nimekuja leo utwambie tuende tuandike, na maneno ya kugeuza geuza utwambie yafanyike hiyo tu.

**Ismael Mbabala**: Asante sana mwenyekiti. Hapa tumekuja turekebishane. Usidhani nikisema hivyo ati nimesema kwa ubaya. Tunataka sisi wananchi wa Kenya, au wananchi wenzangu, tujue kitu gani ambayo imetushikilia habari ya katiba. Kwa maana hata kwenye radio, kwenye vyombo vya habari, tunasikia Katiba bado inaendelea. Kwa hivyo, sidhani nikikuuliza hivyo nimekuliza makosa. Mimi nimeuliza kua, nchi yangu pia nipate kuvunia, jinsi Katiba yetu itakua imeendelea. Kwa hivyo maoni yangu, nataka wale tuliowateua wabunge, ndio wangekua hapa, watueleze ati habari ya Katiba tumetengeza kihivi na kihivi. Lakini wale wabunge wetu ambao tumewateuwa, sijui wameshidwa na nini kule kuzungumza kwenye bunge, na kurekebisha hii habari ya Katiba; natupe kujua Katiba itakua siku fulani, na Katiba imerekebishwa. Sisi tunataka kujua Kenya

yetu inaenda kivipi.

Kuna vitu vingi ambavyo sisi Wakenya hatuhudumiwi, na hatuzipati, na tunaziona tu hivyo hivyo. Mambo ya utwala inadhoreka, sasa mambo mengi inadhoreka katika Kenya yetu hapa. Sasa ndio unasikia ati Katiba ikirekebika. Kwa hivyo ndugu mwenyekiti, nilikua naomba, kama wewe mwenzangu umejua maoni yetu jinsi tulivyo, waturekebishie hayo mambo inafanya sisi tuwe chini kila siku.

Na tuwe mfano kama nchi zingine. Na ya mwisho hawa watu wa upinzani. Mzee wetu hangeajiri watu wengi ambao wengine hawajulikani. Wakipata kazi, hakuna kitu wanatuendeleza katika constituency zetu, nikwenda tu kwenye bunge pale, na kuongea sijui wanaongea nini, na hakuna kwenda kwenze constituency, waende warekebishe zile ambazo zimeharibika, kama njia, vitu zingine, hizi mambo za education, warekebishe, watutembelea mashule, wajue ati mjumbe wetu leo ametutembelea. Hakuna mjumbe ambao amewahi kutembea katika constituency yake akarekebisha. Wakienda Nairobi, ndio kikomo chao.

**Com. Pastor Ayonga**: Twambie tufanye nini. Tuweke nini kwa Katiba ili tusuluhishe hayo mambo?

**Ismael Mbabala**: Hiyo katiba mkisha tatua ndio mtarekebisha mambo, ndio mambo hayo yatakua sawa, kila mtu atajua akienda pahali pake pa constituency yake ataenda kurekebisha yale ambao yamechafuka.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante sana mzee, unaweza kuja hapa uweke kidole. Huyu ni Dominic Okello. Dominic toa majina yako, na halafu utoe maoni.

**Dominic Okello**: Asante sana Bwana mwenyekiti, mimi naitwa Dominic Okello. Na kwa sababu nimekuja hapa leo, nilisikia ya kwamba watu wakubadilisha Katiba wanakuja hapa Mikindani Social Hall. Kuna mambo mengi katika Kenya ambayo imeharibika. Mambo ya kwanza, ni mambo ya mahospitali. Mahosipitali hatuna matibabu ya kisawasawa. Inaonekana watu wanaangamia kwa ajili kwa kukosa madawa. Na mahosipitali Kenya. Sasa hatuwezi kuelewa hii hospitali kazi yake ni nini na tunataka serikali iangalie vile mahospitali zinaweza kuwa na madawa. Ikienda hospitali, mtu anaweza kukaa katika foleni, na hakuna kitu ambacho anapata, kama matibabu. Unaweza kwenda pale, ukae siku nyingi, kama siku tatu bila matibabu. Mara unaambiwa daktari anakuja. Kenya hakuna daktari mara sijui dakitari bado hajaona mgonjwa, huku nyinyi mnakaa tu, lakini hamuoni hata madawa. Sasa hiyo ni kitu moja ambayo inafanya sisi tupate shida sana katika hii nchi. Inatakikana serikali iangalie sana katika sheria ya Katiba hii.

Pili, upande wa elimu; elimu inatakina serikali ingalie watu wa hali ya chini, wanapata taabu sana upande wa elimu. Unaweza kuona mtoto anafukuzwa shuleni kwa sababu ya school fees. Akienda nyumbani ukimrejesha shuleni, saa hiyo saa hiyo unaona mtoto amerudi nyumbani. Shule inafunguliwa leo, kesho mtoto yuko nyumbani. Hiyo sijui tunaweza kufanya namna gani. Na hiyo sheria inataka iangaliwe, mtoto akifukuzwa ni kumvunja. Hawezi kua na raha ya skuli. Hujui mapatao ya mzazi wake iko

namna gani. Watu wa hali ya chini, wanapata taabu sana kwa watoto wa shule. Zamani tulikua tunaona ya kwamba, mtoto ikiwa hajalipa school fees, mwalimu anaandika barua anampa mtoto anapelekea mazazi. Siku hizi hakuna kitu kama hiyo, mtoto akienda shuleni, anachapwa viboko kwa sababu hajalipa school fees. Na mambo kama hayo, sisi tunaona, yale mtu anaweza kuulizwa mambo ya school fees, in mzazi. Na kwa nini mtoto anapigwa kiboko kwa sababu ya school fees. Hiyo sheria kama hiyo inatakikana iangaliwe sana. Mara ingine tunaona ya kwamba mtu kama umekosa, mtoto amekosa kulipa school fees anahangaishwa huku na huku, na serikali inasema elimu ni kama school fees inatakikana, watoto waangaliwe vile wanaweza kusoma. Hiyo mimi naona kama ni kitu muhimu sana katika nchi.

Upande wa walemavu, mimi naona kuna mambo ambayo ni mzigo mkubwa sana. Inatakikana iwekwe sheria ambayo inalinda walemavu. Unaweza kuona mtu barabarani, mimi niko na baisikeli yangu na niko pahali pabaya. Unaona dereva anakuja na gari, anapiga honi huko nyuma, na ukiangalia upande hakuna mahali unaweza kuepuka. Sasa mambo kama ayo inatakikana pia ingaliwe kabisa. Barabara ikitengenezwa inatakikana iwekwe upana na sehemu ambayo watu walemavu kama sisi, tunaweza kupata nafasi ya kutembea. Hapo tunaona watu wanatudhulumu. Kwa sababu akikuona mbele na anajua ukiepa ukienda kona ya barabara unaweza kuanguka, Hajali anakuja tu anapiga honi. wewe ukijaribu kuhepa na barabara ni kuna shimo unakuta umeingia mtaroni, na ukianguka huko, yeye anaenda hajali. Mamabo kama hayo, katika sheria ya Katiba, inatakikana iangaliwe. Na sio kwa sisi walemavu peke yake, hata wenye baiskeli. Barabara inatakikana iwekwe sheria, ambayo inalinda watu wote, sana walemavu. Hapo mimi nimeona kuna jambo.

**Com. Pastor Ayonga**: Asante sana Bwana Okello, na tunamshukuru Mungu kwamba hao watu wote baada ya kufanya hayo, kukupigia honi, Mungu amekutunza. Na tunataka watu walio na utu, watu wanaojali wengine. Na hayo mambo yataangaliwa. Tumesikia mambo mengi kutoka kwa walemavu. Ingawa wewe umekuja saa ya mwisho, tumekua na walemavu wengi, kutoka asubuhi juzi na siku ile nyingine; na mambo yote tumeyasikia. Asante sana kwa kuja, ingawa umekuja late, lakini tumekupatia nafasi. Mpelekee kitabu. Hiki kitabu chetu, yeyote ameongea, lazima aweke kidole. Nataka kuwashukuru kwa kuvumilia kua nasi hapa. Tulikuja hapa asubuhi, tunaona jua limekwenda kwingine; kwa hivyo tutafunga mkutano wetu, na kesho tutakua Changamwe Social Hall. Hapa huu ndio mwisho. Tulipoanza mkutano wetu saa ya asubuhi, tulimuomba Mwenyezi Mungu atutunze, atupe baraka, kwamba maongezi yetu yaweze kua ya maana, kwamba maneno ambayo mtatoa yawekwe maanani, na Mungu amejibu maombi yetu. Ametubariki tumeona mwisho wa siku ya leo, na kwa hivyo tunapotoka hapa pia, lazima tumshukuru aendelea kutubariki. Ningaliwaomba nyote tusimame, na tutaomba.

**Prayer: Com. Pastor Ayonga**: Mungu Mwenyezi Baba wetu aliyebinguni, tunakushukuru kwa siku ya leo. Tumekua na ndugu na dada wa hapa Mikindani, wametwambia mambo mengi sana ya maana. Juu ya uchumi, juu ya maisha, juu ya mazingara magumu, na juu ya mambo kadhaa ambayo hayako sawa. Ambayo wanataka kwamba tunapoangalia mambo ya Katiba tuyamulikie hayo mambo. Mungu tunajua wewe unatupenda sisi zote. Sisi ni wana na binti zako, na wewe huna choyo. Tunaomba kwamba utusaidie kila mmoja wetu, kwa taabu tulizo nazo, ugumu, umasikini, hata na utajiri tulio nao. Hebu wale tulio matajiri tufikirie wasio kua navyo. Wale tulio na chakula tufikirie wale ambao wamelala njaa. Wale ambao mili yetu

mizima hatukulemaa pahali popote. Hebu na tuangalie wenzetu ambao wanaulemavu. Lakini zaidi ya yote, tuwe na utu, tunapomuona mwenzetu. Walio na haja, tunapoweza Mungu tusaidie ili tuweze kuwatimizia haja zao. Na sasa tunapomaliza kazi yetu ya siku ya leo, tunaomba kwamba baraka zako, iende na kila moja ambaye alikuja hapa, arudi nyumbani kwake salama. Utupe usiku mwema, na kesho ikiwa ni mapenzi yako, utupe nafasi ingine ya kuona wengine, ili tuweze kupokea maoni yao. Maisha yetu tumeweka mikononi mwako, na mapenzi yako yatendeke kwa kila mmoja wetu. Tunaomba hayo yote tukikwamini, kwani wewe ni Mungu wetu. Amen.

**Com. Pastor Ayonga**: Na Mungu na awabariki muende nyumbani salama salamini, na muobee katiba yetu.

**Interjection:** Inaudible

**Com. Pastor Ayonga:** Songa, songa nisikie mzee. Hiki ni kipindi cha Mikindani kesho ni kipindi cha wale, pengine hukuweko.

Meeting ended at 5.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**